# Miaka 60 ya Ofisi ya Makamu wa Rais

1964-2024



KIMECHAPISHWA NA:
Mkuki na Nyota Publishers Ltd,
S.L.P. 4246,
Dar es Salaam, Tanzania.
www.mkukinanyota.com

Kwa ajili ya:
Katibu Mkuu,
Ofisi ya Makamu wa Rais,
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba,
S.L.P 2502,
40406 DODOMA.
www.vpo.go.tz

© Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2024

ISBN 978–9987–417–84–1

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli, kurekodi au kubadili sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa njia, namna au mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais.

# YALIYOMO


Vifupisho vya Maneno 02

Tamko 03

Dibaji 06

Shukrani 08

**UTANGULIZI 09**

Chimbuko la Ofisi ya Makamu wa Rais 09

Dira, Muundo na Majukumu ya OMR 14

Utekelezaji wa majukumu ya OMR 23

Madhumuni ya Kitabu 29

**MUUNDO, UONGOZI NA MAJUKUMU 30**

Mheshimiwa Sheikh Abeid Amani Karume 31

Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa 45

Mheshimiwa Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi 53

Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi 63

Mheshimiwa Sheikh Idris Abdulwakil 71

Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba 77

Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma 83

Mheshimiwa John Samwel Malecela 89

Mheshimiwa Cleopa David Msuya 95

Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma 101

Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein 107

Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal 117

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan 127

Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango 141

**VIONGOZI WALIOHUDUMU KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS NA KUPATA NYADHIFA ZA JUU** 160

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan 161
Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi 169
Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi 173
Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi 175
Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine 177
Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba 179
Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa 181
Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein 183
Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa 185
Mheshimiwa Anne Semamba Makinda 187
Mheshimiwa Gertrude Ibengwe Mongella 189
Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu 191

**MUZIKI WA DANSI NA TAARAB ULIVYOIMARISHA MUUNGANO** 193

Hitimisho na Matarajio 200
Rejea 202
Hati ya Makubaliano ya Muungano Kati ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar 203
Kamati Iliyoandaa Kitabu Cha Miaka 60 ya Ofisi ya Makamu wa Rais 208

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AAZ | African Association of Zanzibar |
| ACP | The African, Caribbean and Pacific Group of States |
| ASDP | Agricultural Sector Development Programme |
| ASP | Afro–Shirazi Party |
| ASPYL | Afro–Shirazi Party Youth League |
| AZISE | Asasi Zisizo za Serikali |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BIZANJE | Shirika la Biashara za Nje Zanzibar |
| BLW | Baraza la Wawakilishi |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| COSTECH | Tanzania Commission for Science and Technology |
| CPCT | Cleaner Production Centre of Tanzania |
| CUF | Civic United Front |
| EEC | European Economic Commision |
| eGA | e–Government Authority |
| EPZ | Export Processing Zone |
| ESAMI | Eastern and Southern African Management Institute |
| GBS | General Budget Support |
| HADO | Hifadhi Ardhi Dodoma |
| HASHI | Hifadhi Ardhi Shinyanga |
| HIMA | Hifadhi Mazingira–Iringa |
| IDM | Institute of Development Management |
| JKT | Jeshi la Kujenga Taifa |
| JNHPP | Julius Nyerere HydroPower Project |
| JWTZ | Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania |
| LAMP | Land Management Programme (Babati) |
| MACEMP | Marine and Coastal Environmental Management Project |
| MCA (T) | Millenium Challenge Account–Tanzania |
| MIVARF | Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance |
| MKUHUMI | Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa Kutokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MTAKULA | Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula |
| NDC | Nationally Determined Contribution |
| NEMC | National Environment Management Council |
| NRC | National Radiation Commission |
| OAU | Organisation of African Unity |
| OMPR | Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Zanzibar) |
| OMR | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| PADEP | Participatory Agricultural Development Programme |
| PAYE | Pay As You Earn |
| SA | Shirazi Association |
| SCAPA | Soil Conservation and Agro–forestry Programme in Arusha |
| SECAP | Soil Erosion Control and Agro–forestry Project |
| SELF | Small Entrepreneur Loan Facility |
| SJMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TPH | Total Petroleum Hydrocarbons |
| TAM | Tathmini ya Athari kwa Mazingira |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company |
| TANU | Tanganyika African National Union |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TRAT | Tax Revenue Appeals Tribunal |
| TSN | Tanzania Standard Newspapers |
| UNEP | United Nations Environment Programme |
| VPO | Vice President's Office |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Corporation |
| ZECO | Zanzibar Electricity Corporation |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority |
| ZNP | Zanzibar Nationalist Party |
| ZPPP | Zanzibar and Pemba People's Party |
| ZRB | Zanzibar Revenue Board |

# TAMKO



## Dkt. Philip Isdor Mpango

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ndugu Watanzania wenzangu, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa amani na utulivu wa Taifa letu. Hali hii ni matokeo ya juhudi za dhati zilizofanywa na Serikali za Awamu zote za uongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza na kudumisha utaifa wetu.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waasisi wa Taifa letu: Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zao za kuasisi na kudumisha Muungano wetu.

Kwa namna ya pekee, niwashukuru Marais wa Awamu zote katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa hekima na busara zao zilizowezesha Taifa letu kuwa imara na kudumisha udugu wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kipekee, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Nane, kwa kuendelea kudumisha Muungano.

Pia, nawashukuru kwa dhati viongozi wetu wote waliohudumu katika nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa

kuanzia, napenda kutoa shukrani kwa viongozi waliohudumu katika nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1964–1972); Mheshimiwa Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1972–1984); Mheshimiwa Al–hajj Ali Hassan Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1984–1985); Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985–1990); Mheshimiwa John Samwel Malecela, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1990–1994); na Mheshimiwa Cleopa David Msuya, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1994–1995).

Vilevile, nawashukuru waliohudumu katika wadhifa wa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu (1964–1977); Mheshimiwa Sheikh Idris Abdulwakil, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1985–1990); na Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1990–1995).

Hali kadhalika, nawashukuru waliohudumu katika nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1995–2001); Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2001–2010); Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2010–2015); na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2015–2021).

Viongozi hao wameweka msingi imara wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambao umeniwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba ya kuwa Msaidizi Mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na majukumu maalumu ya kuratibu masuala ya Muungano; kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano; na usimamizi wa uhifadhi wa mazingira.

Mchango wa viongozi hao umewezesha Muungano wetu kudumu kwa zaidi ya nusu karne na kuwa wa kipekee barani Afrika, na wenye mafanikio makubwa ya kujivunia. Hali ya amani, utulivu, ulinzi na usalama ndani ya nchi na kwenye mipaka yetu, imeendelea kuimarika. Misingi hiyo imeimarika kutokana na mwamko wa wananchi kuunga mkono Muungano na uelewa mkubwa wa dhana ya uwajibikaji na utashi wa kisiasa kwa viongozi wa ngazi zote. Pia, uchumi umeimarika kutokana na juhudi ya Watanzania, mazingira na mahusiano mazuri ya kibiashara na uwekezaji kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, pamoja na kuimarika kwa miundombinu, hususan ya uchukuzi, mawasiliano na huduma za jamii ikiwemo afya, maji na elimu.

Kwa upande wa usimamizi wa mazingira, sote tunafahamu kuwa uhifadhi, utunzaji na usafi wa mazingira ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku na kwa uhai wa kila kiumbe. Juhudi zimeendelea kufanyika katika awamu zote za uongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo takribani asilimia 40 ya eneo la nchi limehifadhiwa kisheria.

Nitumie fursa hii, kuwashukuru Makamu wa Rais wastaafu na familia zao kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika upatikanaji wa taarifa mbalimbali, zilizowezesha kukamilisha uandishi wa Kitabu hiki.

Rai yangu kwa Watanzania wote tunapoadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni kusoma Kitabu hiki "Miaka 60 ya Ofisi ya Makamu wa Rais, 1964–2024" ili kuendelea kukuza uelewa kuhusu majukumu ya kikatiba ya Ofisi ya Makamu wa Rais na majukumu mengine.

**Tudumishe na kuimarisha Muungano, tusimamie na kuyatunza Mazingira.**

**Mungu Ibariki Tanzania**



**Dkt. Philip Isdor Mpango**
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Aprili, 2024

# DIBAJI



**Dkt. Selemani S. Jafo (Mb.)**
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)

Maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yanatukumbusha historia ya Ofisi ya Makamu wa Rais, hasa tukitafakari majukumu maalumu ya Ofisi hii ya kuratibu Masuala ya Muungano na Usimamizi wa uhifadhi wa Mazingira. Ofisi ya Makamu wa Rais imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Toleo la 2005) Ibara ya 47(1) (a). Aidha, Tangazo la Serikali Na. 619A la tarehe 30 Agosti, 2023 limeainisha majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo yanajumuisha: uratibu wa masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano; na usimamizi wa shughuli za uhifadhi wa mazingira nchini.

Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Alhaji Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa uongozi wao makini uliotuwezesha kufanikisha uandishi wa Kitabu hiki.

Napenda pia, kutumia nafasi hii kutoa shukrani za kipekee kwa Mawaziri 32 na Naibu Mawaziri 12 waliohudumu kwa awamu na vipindi tofauti katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mchango wao katika kumsaidia Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba ya kuimarisha Muungano na majukumu mengine yaliyoainishwa kisheria ikiwemo uhifadhi wa mazingira nchini.

Nawashukuru Mawaziri wastaafu walitenga muda wao kutoa taarifa na kumbukumbu kuhusu utekelezaji wa majukumu yao katika Ofisi ya Makamu wa Rais, zilizochangia kufanikisha uandishi wa Kitabu hiki.

Kitabu hiki ni rejea adhimu ya maandishi na picha kuhusu historia ya Ofisi ya Makamu wa

Rais; mwenendo wa mabadiliko yaliyojitokeza katika majukumu, muundo na uongozi; na mafanikio yaliyopatikana.

Nawasihi Watanzania wote hususan vijana kusoma Kitabu hiki ili kupata uelewa kuhusu miaka 60 ya Ofisi ya Makamu wa Rais na hivyo, kuamsha ari ya kuulinda, kuutetea na kuudumisha Muungano, pamoja na kuhifadhi mazingira.



# SHUKRANI

**Mary N. Maganga**
Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais

Uandishi wa Kitabu hiki umetokana na mchango na juhudi za Viongozi na Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, watumishi kutoka Wizara mbalimbali pamoja na wadau wengine.

Kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Selemani S. Jafo (Mb.); Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), na Mheshimiwa Khamis H. Khamis (Mb.) Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa mwongozo wao thabiti ambao umewezesha kukamilisha Kitabu hiki. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote waliohudumu tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 1964 kwa utekelezaji thabiti wa majukumu yao. Pia, nawashukuru waliotoa taarifa na kumbukumbu zilizochangia kufanikisha ukamilishaji wa Kitabu hiki.

Ningependa pia, kutoa shukrani kwa Ofisi ya Rais, Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais–Zanzibar; Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; Idara ya Habari (MAELEZO); Shirika la Utangazaji Tanzania; Shirika la Magazeti ya Serikali ; Mpigachapa Mkuu wa Serikali; Maktaba Kuu ya Taifa; Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar; Shirika la Utangazaji Zanzibar; Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu–Zanzibar; Idara ya Habari (MAELEZO)–Zanzibar; na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha upatikanaji wa kumbukumbu na taarifa mbalimbali zilizofanikisha uandishi wa Kitabu hiki.

Mwisho, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Timu ya Wataalamu walioshiriki kuandaa Kitabu hiki. Aidha, nawashukuru watumishi wote waliohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais tangu kuanzishwa kwake mwaka 1964, kwa mchango wao katika mafanikio ya Ofisi hii.

# UTANGULIZI

## 1.1 Chimbuko la Ofisi ya Makamu wa Rais

Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR) ni matokeo ya Muungano wa nchi mbili zilizokuwa huru za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, uliofanyika tarehe 26 Aprili, 1964. Msingi wake kisheria ni Hati ya Makubaliano ya Muungano (Hati ya Muungano) iliyosainiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika na Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Ikulu Zanzibar, tarehe 22 Aprili, 1964.



▲
*Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar (kushoto), akimkaribisha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika, alipowasili Uwanja wa Ndege wa Zanzibar kwa ajili ya kutia saini Hati ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, tarehe 22 Aprili, 1964.*



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika aliyekaa kushoto) na Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar (aliyekaa kulia) wakisaini Hati ya Makubaliano ya Muungano. Baadhi ya wanaoshuhudia ni Mhe. Oscar Kambona (aliyesimama wa tatu kutoka kushoto), Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanganyika na Mhe. Abdalla Kassim Hanga (aliyesimama wa tatu kutoka kulia), Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Ikulu-Zanzibar, tarehe 22 Aprili, 1964.*

▼



Hati ya Muungano iliridhiwa rasmi na mamlaka za kutunga sheria za Zanzibar na Tanganyika, yaani Baraza la Mapinduzi na Bunge la Tanganyika mtawalia Jumamosi tarehe 25 Aprili, 1964. Baraza lilifanya kikao chake asubuhi, Ikulu ya Zanzibar na kushuhudiwa na mjumbe maalumu wa Mwalimu Nyerere, Mhe. Oscar Kambona (Waziri wa Mambo ya Nje); na Bunge lilikaa jioni katika Ukumbi wa Bunge wa Karimjee–Dar es Salaam, na kushuhudiwa na mjumbe maalumu wa Sheikh Karume, Mhe. Salim Rashid (Katibu wa Baraza la Mapinduzi).

Ibara ya iii (b) ya Hati ya Muungano inaeleza kuwa, kutakuwa na Ofisi mbili za Makamu wa Rais, ambapo mmoja wa Makamu wa Rais atakuwa na Ofisi yake Zanzibar na atakuwa ndiye kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Msaidizi Mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano katika kutekeleza majukumu yake yanayohusu Zanzibar. Aidha, Ibara ya vi(a) ya Hati ya Makubaliano ya Muungano inamtaja Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika, kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, akisaidiwa na Makamu wa Rais wawili ambao ni Sheikh Abeid Amani Karume kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano (Ibara ya vi(b)) na Makamu wa Pili wa Rais, ambaye anatajwa tu kwenye Hati ya Muungano kwa wadhifa wake huo, na siyo kwa jina lake (Ibara ya iii(b) na vi(a)).

Hivyo, kwa mujibu wa Hati ya Muungano na Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Na. 22 ya mwaka 1964 (Kifungu cha 5(c)), Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwateua Sheikh Abeid Amani Karume kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Rashidi Mfaume Kawawa kuwa Makamu wa Pili wa Rais, tarehe 27 Aprili, 1964.

Siku hiyo hiyo ya uteuzi, Makamu hao wawili wa Rais na wajumbe watano wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar (Mhe. Abdalla Kassim Hanga, Mhe. Abdulrahman Mohamed Babu, Mhe. Hassan Nassor Moyo, Sheikh Idris Abdulwakil Nombe, na Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi) waliapishwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na baadaye wabunge hao watano wakateuliwa kwenye Baraza la Mawaziri la kwanza la Jamhuri ya Muungano. Wajumbe 17 wa Bunge la Jamhuri ya Tanganyika walioteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ni; Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa, Mhe. Asanterabi Nsilo Swai, Mhe. Lawi Nangwanda Sijaona, Mhe. Bhoke Munanka, Mhe. Jeremiah Kasambala, Mhe. Clement George Kahama, Mhe. Paul Lazaro Bomani, Mhe. Oscar Kambona, Mhe. Said Ali Maswanya, Mhe. Tewa Said Tewa, Mhe. Job Malecela Lusinde, Mhe. Solomon Nkya Eliufoo, Mhe. Derek Noel Bryceson, Mhe. Michael Kamaliza, Mhe. Austin Kapere Shaba, Mhe. Sheikh Amri Abedi Kaluta na Mhe. Amir Habib Jamal.

*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (wa nne kutoka kushoto mbele), akiwa na Makamu wake wawili ambao ni Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais (wa kwanza kushoto kwa Mwalimu) na Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa, Makamu wa Pili wa Rais (wa kwanza kushoto kwa Karume), katika picha ya pamoja ya Baraza la Kwanza la Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, pamoja na baadhi ya wabunge na viongozi wengine wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, mara baada ya kuapishwa Ikulu Dar es Salaam, tarehe 27 Aprili, 1964.*

▼



Baraza la Kwanza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano lilikuwa na jumla ya Mawaziri 22 wafuatao:

**Ofisi ya Rais, Masuala ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo**

| | | |
|---|---|---|
| Waziri wa Nchi<br>**Mhe. Asanterabi N. Swai** | **Waziri wa Nchi**<br>**Mhe. Abdulrahman M. Babu** | **Waziri wa Nchi**<br>**Mhe. Amir H. Jamal** |

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

| |
|---|
| Waziri wa Nchi<br>**Mhe. Aboud M. Jumbe** |

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais**

| | |
|---|---|
| Waziri wa Nchi<br>**Mhe. Lawi N. Sijaona** | Waziri wa Nchi<br>**Mhe. Bhoke Munanka** |

**Wizara**

| | | |
|---|---|---|
| Wizara ya Ulinzi na Ujenzi wa Nch<br>**Mhe. Rashidi M. Kawawa** | Wizara ya Biashara na Ushirika<br>**Mhe. Jeremiah Kasambala** | Wizara ya Usafirishaji na Ujenzi<br>**Mhe. Clement G. Kahama** |
| Wizara ya Fedha<br>**Mhe. Paul L. Bomani** | Wizara ya Mambo ya Nje<br>**Mhe. Oscar S. Kambona** | Wizara ya Afya<br>**Mhe. Derek N. Bryceson** |
| Wizara ya Ardhi, Makaazi na Maji<br>**Mhe. Tewa S. Tewa.** | Wizara ya Kilimo, Misitu na Wanyama<br>**Mhe. Said A. Maswanya** | Wizara ya Viwanda, Madini na Umeme<br>**Mhe. Abdalla K. Hanga** |
| Wizara ya Elimu<br>**Mhe. Solomon N. Eliufoo** | Wizara ya Mambo ya Ndani<br>**Mhe. Job M. Lusinde** | Wizara ya Kazi<br>**Mhe. Michael Kamaliza** |
| Wizara ya Maendeleo na Mila<br>**Mhe. Sheikh Amri A. Kaluta** | Wizara ya Tawala za Mitaa na Nyumba<br>**Mhe. Austin K. Shaba** | Wizara ya Habari na Usafiri wa Kutalii<br>**Mhe. Idris Abdulwakil** |
| | Wizara ya Sheria<br>**Mhe. Hassan N. Moyo** | |

Uteuzi huo wa Baraza la Mawaziri ulikuwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa Hati ya Muungano katika kuunda vyombo vya utendaji wa shughuli za mamlaka ya nchi na mgawanyo wa mamlaka na madaraka baina ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar.

Katiba ya Muda ya Tanzania ya mwaka 1965 iliyotungwa kwa kuzingatia masharti ya Hati ya Muungano (ii)(iii)(iv) na (v) ilikasimu mamlaka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano, pia juu ya mambo yote yahusuyo Tanzania Bara. Aidha, ilikasimu mamlaka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo ya Muungano yahusuyo Zanzibar.

## 1.2 Dira, Muundo na Majukumu ya OMR

Kuanzia mwaka 1964 hadi 2024, Ofisi ya Makamu wa Rais imeongozwa na Makamu wa Rais 14, watano kutoka Tanzania Bara na tisa kutoka Tanzania Zanzibar, miongoni mwao akiwemo mwanamke mmoja. Dira, muundo na majukumu ya OMR yamepitia marekebisho ya kisera, kisheria, miundo na miongozo kwa kuzingatia mahitaji, vipaumbele vya wakati husika na maslahi mapana ya muda mrefu ya Muungano kikatiba.

Majukumu makuu ya Makamu wa Rais yaliainishwa kwenye Hati ya Muungano ya mwaka 1964 (kama ilivyoelezwa hapo juu), baadaye kwenye Katiba ya Muda ya Tanzania ya mwaka 1965 (ibara ya 9 & 13) na sasa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 47(1) (a), (b) na (c) ambayo kimsingi ni: kumsaidia Rais katika kufuatilia utekelezaji wa siku hata siku wa mambo ya Muungano; kufanya kazi zote zinazoagizwa na Rais; na kufanya kazi zote za Rais kama Rais hayuko kazini au yuko nje ya nchi.

Muundo huo wa OMR (ulioelezwa na nyaraka hizo za Kikatiba) pamoja na dira na majukumu yake, vilizingatia Sera na Maelekezo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Katiba ya Muda ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1965 ilitoa ufafanuzi wa wazi zaidi chini ya Ibara ya 13(2) & (3) kuwa Rais ataanzisha, pale inapobidi, Ofisi nyingine za Mawaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa Hati (instruments) na Makamu wa Rais na Mawaziri watahusika kwenye maeneo yatakayoainishwa na Rais. Aidha, Ibara ya 14 ilimpa Rais wa Jamhuri ya Muungano madaraka ya kuteua Mawaziri Wadogo[1] wa kuwasaidia Mawaziri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kiserikali.

1. Kwa sasa wadhifa huo unajulikana kama Naibu Mawaziri

## a) Tangazo la Serikali Na. 235 la tarehe 28 Aprili, 1964

Tangazo hili la kwanza baada ya Muungano, liliitambua Afisi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwataja viongozi watatu walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano kuwa wasaidizi wakuu wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri. Viongozi hao ni: Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Waziri wa Nchi; Mhe. Abdulaziz A. Khamis, Waziri Mdogo; na Mhe. Abdalla S. Mugheiry, Katibu Msaidizi Mkuu. Kwa kuwa Afisi ya Rais wa Zanzibar iliongozwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi (KBM), wasaidizi hao wakuu wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano walitekeleza majukumu yao kwa ushauri na ushirikiano wa karibu na KBM. Idadi ya wasaidizi wa Makamu wa Rais ilibadilika kuendana na majukumu.

Tangazo hilo lililodumu hadi mwaka 1970, halikutoa maelekezo yoyote ya ziada kwa Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu majukumu yake, pamoja na kwamba yeye na Waziri wake wa Nchi walitumia muda mwingi Tanzania Bara na Zanzibar kuutangaza Muungano na kuwaelezea wananchi chimbuko lake na faida zake.

Kwa kuzingatia maoni ya busara yaliyopatikana kutoka kwa viongozi wengi wastaafu wakati wa kuandika kitabu hiki, ushahidi mwingi wa mdomo na wa kimazingira unathibitisha maoni yao kwamba: Mwalimu alimheshimu sana Sheikh Karume, kwanza kama kaka yake kiumri na pili, kwa msimamo wake uliokuwa hautetereki katika kutetea maslahi, haki na uhuru wa Mwafrika. Mwalimu aliamini fika kuwa ni msimamo imara wa umajumui wa kiafrika wa Sheikh Karume, uliochangia sana kwa muda mfupi ukamilishaji wa mchakato wa kuunganisha Tanganyika na Zanzibar.

Kwa muktadha huo, Mwalimu Nyerere alimchukulia Sheikh Karume kama mwasisi mwenza wa Muungano na Rais mwenza wa Jamhuri ya Muungano. Alishauriana naye kwa karibu kuhusu masuala ya uendeshaji wa Jamhuri ya Muungano na kuheshimu utambulisho mahsusi wa Zanzibar (identity) ndani ya Muungano na uhuru wa maamuzi/kujiendesha wa Zanzibar (autonomy) kwa masuala yasiyo ya Muungano. Mwalimu alimpa Sheikh Karume muda zaidi kutibu madonda ya kihistoria ya Zanzibar na hakika Sheikh Karume alifanya hivyo. Lilikuwa ni jambo la kawaida kwa viongozi hao wawili kupokea wageni kwa pamoja na kukagua gwaride kwa pamoja kutoa ujumbe kwa wahafidhina kwamba Zanzibar haijamezwa na Tanganyika na kwamba Tanzania ni Muungano wa nchi mbili, ndoto ya umajumui wa kiafrika iliyotimia. Hali ilikuwa hivyo mpaka mauti yalipomkuta Sheikh Karume tarehe 7 Aprili, 1972.

Tangazo hilo la Serikali Na. 235 la tarehe 28 Aprili, 1964 lililojadiliwa hapo juu, vilevile lilihusisha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwataja viongozi wanne walioteuliwa na Mwalimu Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muun-

*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (mstari wa pili kulia), akiwa na Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (mstari wa pili kushoto) na mgeni wao Mfalme Haile Selassie wa Ethiopia (wa kwanza kulia mstari wa mbele) walipokuwa wanakagua gwaride la heshima alipokuja mjini Zanzibar kuwapongeza kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, tarehe 1 Desemba, 1965.*



gano, kuwa wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa, Makamu wa Pili wa Rais. Viongozi hao ni: Mhe. Lawi Sijaona, Waziri wa Nchi; Mhe. Bhoke Munanka, Waziri wa Nchi; Mhe. Aaron Mwakang'ata, Katibu Msaidizi Mkuu na Bw. Bernard Mulokozi, Katibu Msaidizi Mkuu. Idadi ya wasaidizi wa Makamu wa Pili wa Rais ilibadilika kuendana na majukumu.

Tangazo halikuishia hapo, likataja majukumu yote ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (ambaye vilevile alikuwa Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni) kuwa ni: Mambo yote ya Ulinzi; Majeshi ya Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania pamoja na Jeshi la Anga; Mambo yote ya Jeshi la Kujenga Taifa; Idara ya Kupiga Chapa; Vijana; Wakimbizi; Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nyaraka za Kale.

## b) Tangazo la Serikali Na. 293 la tarehe 20 Novemba, 1970

Kwa mujibu wa Tangazo hili, majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, yaliainishwa upya na kuongezeka kuwa ni: Ulinzi; Jeshi la Kujenga Taifa; Jumuiya za vijana; Mahakama; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Bunge; Mrajisi Mkuu (Registrar General); Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali; Uhamisho wa Wahalifu/Watuhumiwa (Extradition); Hati za Makubaliano (Deeds of Arrangements); Usajili wa vizazi na vifo; Ndoa; Uasili (Adoption); Muunganiko wa Wadhamini (Trustees Incorporation); na Wakimbizi.

## c) Tangazo la Serikali Na. 40 la tarehe 24 Februari, 1972

Kwa mujibu wa Tangazo hili majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni yafuatayo: Haki; Mahakama; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Bunge; Kabidhi Wasii; Uhamisho wa Wahalifu (Extradition); Hati za Makubaliano (Deeds of Arrangements); Usajili wa vizazi na vifo; Ndoa; Uasili (Adoption); Muunganiko wa Wadhamini (Trustees Incorporation); Tawala za Mikoa; Maendeleo Vijijini; Kuhamasisha Vijiji vya Ujamaa; Serikali za Mitaa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Utoaji wa leseni za Vileo; Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; Kituo cha Mafunzo cha Serikali za Mitaa; Maendeleo ya Jamii; Chuo cha Kivukoni; Vituo vya Mafunzo vya Wilaya; Kituo cha Elimu Kibaha; na Sherehe na Maadhimisho.

## d) Tangazo la Serikali Na. 10 la tarehe 9 Januari, 1976

Kwa mujibu wa Tangazo hili majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais ni: Bunge; Tawala za Mikoa; Maendeleo Vijijini; Kuendeleza Vijiji vya Ujamaa; Serikali za Mitaa; Mamlaka za Mitaa; Utoaji wa leseni za vileo; Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; Kituo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa; Maendeleo ya Jamii; Chuo cha Kivukoni; Vituo vya Mafunzo vya Wilaya; Kituo cha Elimu cha Kibaha; Sherehe na Maadhimisho; na Vyama vya Ushirika.

Mwaka 1977 hadi 1985, muundo wa Ofisi ya Makamu wa Rais ulibakia na wadhifa wa Makamu wa Kwanza wa Rais bila wadhifa wa Makamu wa Pili wa Rais ambapo Mawaziri Wakuu walioteuliwa hawakupewa wadhifa wa Makamu wa Pili wa Rais. Mawaziri Wakuu hao ni Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine (1977–1980 na 1983–1984), Mheshimiwa Cleopa David Msuya (1980–1983) na Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim (1984–1985).

Kwa mujibu wa viongozi wengi waliohojiwa, utofauti huo kiuteuzi ulitokana na unyambulikaji (flexibility) katika tafsiri ya Katiba ya Muungano kwa kuzingatia, pamoja na mambo mengine, maslahi ya msingi ya pande zote mbili za Muungano.

Kufuatia mabadiliko hayo, majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yalihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, wakati huo ikiongozwa na Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi.

## e) Tangazo la Serikali Na. 16 la tarehe 6 Februari, 1981

Kwa mara ya kwanza tangu Muungano, Serikali iliainisha kwa kina, majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Tangazo la Serikali Na.16 la tarehe 6 Februari, 1981 ambayo ni: Sera ya Uchumi; Mpango wa Maendeleo wa Taifa; Bajeti ya Maendeleo; Sekretarieti ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Mawaziri; Mipango, Utekelezaji na Udhibiti; Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Takwimu na Tafiti

za Uchumi; Tume ya Uchumi ya Afrika; Baraza la Utafiti wa Sayansi Tanzania; Sekretarieti ya Tume ya Mipango ya Taifa; na kundi la Nchi za Afrika, Carribean na Pacific/Tume ya Kiuchumi ya Nchi za Ulaya (ACP/EEC).

## f) Tangazo la Serikali Na. 205 la tarehe 17 Aprili, 1987

Kwa mujibu wa Tangazo hili, majukumu yaliyoainishwa ni: Uratibu wa Shughuli za Serikali Bungeni; Tawala za Mikoa; Huduma ya Habari na Utangazaji; Uchapaji na Uchapishaji wa Serikali; Huduma za Filamu; Magazeti ya Serikali; Maadhimisho na Sherehe; na Mashirika ya Umma na Miradi iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais.

## g) Tangazo la Serikali Na. 489 la tarehe 30 Novemba, 1990

Kupitia Tangazo hili, majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais yaliainishwa kuwa: Uratibu wa Shughuli za Serikali (Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa shughuli katika Wizara zote); Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni; Kiungo baina ya Chama na Serikali; Kujiandaa kukabiliana na Maafa; Sherehe na Maadhimisho; Haki; Mahakama; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Uandaaji wa Miswada; Uendeshaji Mashtaka; Sheria ya Madai na Sheria za Kimataifa; Amri za Uhamisho na kusaidiana katika masuala ya kijinai; Mfilisi; Kabidhi Wasii; Hati za Makubaliano; Usajili wa Vizazi na Vifo; Kuasili; na Muunganiko wa Wadhamini, Marekebisho ya Sheria, Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais.

Tangazo hili pia liliainisha majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, yafuatayo: Uratibu wa masuala ya Muungano na kiungo baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar kwa masuala yasiyo ya Muungano. Kwa kipindi hiki, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilikuwa Zanzibar.

## h) Tangazo la Serikali Na. 720 la tarehe 28 Novemba, 1995

Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yaliainishwa upya kupitia Tangazo hilo la Serikali Na. 720 la tarehe 28 Novemba, 1995 kama ifuatavyo: kusimamia masuala ya Muungano na kuwa kiungo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano; kushughulikia Sera ya Mazingira, Uhifadhi na Usafi wa Mazingira; kuzuia mmomonyoko wa udongo katika maeneo ya fukwe za bahari, pamoja na kusimamia Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; kushughulikia Mkakati wa Kupambana na Umaskini, Uratibu na Ufuatiliaji wa programu mbalimbali za kisekta za kupambana na umaskini katika sekta mbalimbali, pamoja na kusimamia Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE); kusimamia Wakala za Serikali chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais; uendelezaji wa Rasilimali Watu katika Ofisi ya Makamu wa Rais; na kusimamia miradi katika Idara zinazojitegemea na mashirika ya umma katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kutokana na mageuzi makubwa ya kiuchumi na kisiasa duniani yaliyotokea miaka ya 1990, Tanzania ilirejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, ambao ulifutwa mwaka 1965. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ilifanyiwa marekebisho mwaka 1994 ili kuandaa mazingira stahiki ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu mwaka 1995 chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Hivyo, utaratibu wa kuwa na Makamu Wawili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliodumu kwa miaka 31 kuanzia mwaka 1964 hadi 1995 ulifanyiwa mabadiliko kwa kumtaka kila Mgombea Urais awe na Mgombea Mwenza, ambaye atakuwa Makamu wake wa Rais. Mabadiliko hayo yaliweka bayana kuwa, endapo Mgombea Urais atatoka Tanzania Bara, Mgombea Mwenza atatoka Zanzibar, na endapo Mgombea Urais atatoka Zanzibar, Mgombea Mwenza atatoka Tanzania Bara. Hivyo, mabadiliko hayo yaliondoa utaratibu wa kuwa na Makamu wawili wa Rais.

## i) Tangazo la Serikali Na. 468 la tarehe 1 Desemba, 2000

Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yaliyoainishwa kupitia Tangazo hili ni: kuratibu Masuala ya Muungano; kuwa kiungo baina ya SJMT na SMZ katika masuala yasiyo ya Muungano; kuandaa Sera ya Mazingira na kusimamia utekelezaji wake; ufuatiliaji na uratibu wa shughuli za Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira; kuondoa umaskini; sera na mikakati; uratibu na ufuatiliaji wa programu za kuondoa umaskini katika sekta mbalimbali; uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; uendelezaji wa rasilimali watu katika Ofisi ya Makamu wa Rais; na shughuli za Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma na miradi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na kusimamia Wakala zilizo katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

## j) Tangazo la Serikali Na. 2 la tarehe 13 Januari, 2006

Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yaliyoainishwa kupitia Tangazo hili ni: kuratibu masuala ya Muungano; kiungo baina ya SJMT

Mabadiliko ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yaliyofanyika mwaka 1994, yalianzisha utaratibu wa wagombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na wagombea wenza (Makamu wa Rais watarajiwa). Aidha, yalikuja na mabadiliko katika uapishwaji wa viongozi wakuu wa nchi ambapo Rais na mgombea mwenza wanaapishwa na Jaji Mkuu. Utaratibu uliokuwepo awali, uliruhusu Rais peke yake kuapishwa na Jaji Mkuu. Makamu wa Rais (wote wawili) waliapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

na SMZ katika masuala yasiyo ya Muungano; kuandaa Sera ya Mazingira na kusimamia utekelezaji wake; kufuatilia na kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na kuboresha utekelezaji na kuendeleza Rasilimali Watu katika Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Shughuli za Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma na Miradi katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

## k) Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba, 2010

Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yaliyoainishwa kupitia Tangazo hili ni: kuratibu masuala ya Muungano; kuratibu ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano; kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira; kusimamia na kuendeleza watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais; kuratibu na kusimamia shughuli za Idara na Wakala zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais; na kufuatilia na kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

## l) Tangazo la Serikali Na. 143 la tarehe 22 Aprili, 2016

Tangazo hili liliainisha majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yafuatayo: Kuratibu Mambo ya Muungano; Kuimarisha Ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Masuala Yasiyo ya Muungano; Kusimamia Hifadhi ya Mazingira nchini; na Kusimamia shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

## m) Tangazo la Serikali Na. 534 la tarehe 2 Julai, 2021

Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yaliyoainishwa katika Tangazo hili ni: Sera ya Mazingira na Utekelezaji wake; Uratibu wa Masuala ya Muungano; Ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano; Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi; Kuhamasisha Uzalishaji unaozingatia Hifadhi ya Mazingira endelevu na Uchumi wa Kijani, Uhifadhi wa Mazingira na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira; Maboresho na uendelezaji wa Rasilimali Watu ya Ofisi ya Makamu wa Rais; na Shughuli za Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Wakala, Programu na miradi katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

## n) Tangazo la Serikali Na. 619A la tarehe 30 Agosti, 2023

Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yaliyoainishwa katika Tangazo hili ni: Sera ya Mazingira na Utekelezaji wake; Uratibu wa Masuala ya Muungano; Ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano; Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi; Kuhamasisha Uzalishaji unaozingatia Hifadhi ya Mazingira endelevu na Uchumi wa Kijani, Uhifadhi wa Mazingira na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira; Maboresho na uendelezaji wa Rasilimali Watu ya Ofisi ya Makamu wa Rais; na Shughuli za Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Wakala, Programu na miradi katika Ofisi ya Makamu wa Rais.



▲

*Mwalimu Julius Kambarage, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika (wa kwanza kushoto), akiwa na Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, wakikagua gwaride la heshima, baada ya Sheikh Karume kuwasili Dar es Salaam kwa ajili ya Kubadilishana Hati ya Muungano, tarehe 26 Aprili, 1964.*

## 1.3 Utekelezaji wa majukumu ya OMR

Jukumu la msingi la Kikatiba la Ofisi ya Makamu wa Rais la kuratibu Masuala ya Muungano limedumu kwa miaka 60 kuanzia mwaka 1964 hadi 2024. Jukumu hilo maalumu limeendelea kuratibiwa na OMR hata baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992 ulioleta mabadiliko katika muundo wa Ofisi na kuwa na Ofisi moja ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sambamba na jukumu hilo maalumu, Serikali imetoa Matangazo 12 (kama yalivyoainishwa katika aya 1.2) kuipa OMR majukumu mbalimbali ikiwemo uhifadhi wa mazingira, ambalo limekuwa sehemu ya majukumu ya OMR kwa kipindi cha miaka 29 tangu mwaka 1995.

### 1. Uratibu wa Masuala ya Muungano

Tarehe 19 Agosti, 1994, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipokea, lilijadili na kupitisha taarifa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuhusu Kuondoa Vikwazo vya Muungano (Kamati ya Shellukindo). Kupitia taarifa hiyo, Bunge lilielekeza kutekelezwa kwa maoni na mapendekezo yaliyotolewa, ikiwemo: kufanya Marekebisho ya 11 na 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kuweka bayana Masuala ya Muungano katika Nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kuanzisha Sekretarieti ya Masuala ya Muungano kwa lengo la kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa masuala ya Muungano.

Mwaka 1998, Serikali ilitekeleza maelekezo ya Bunge kwa kuanzisha Sekretarieti ya Muungano iliyowekwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na baadaye kupewa hadhi ya Idara mwaka 2005 na kutambulika kama Idara ya Muungano. Majukumu ya Idara hiyo ni: kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mambo yasiyo ya Muungano.

Vilevile, Idara ya Muungano ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa mambo 22 ya Muungano, ambapo awali yaliorodheshwa mambo 11 katika Hati ya Muungano ambayo ni: Katiba ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano; Mambo ya Nchi za Nje; Ulinzi na Usalama; Polisi; Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari; Uraia; Uhamiaji; Mikopo na biashara ya Nchi za Nje; Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano; Kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika; Ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha; Bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu.

Mambo ya Muungano yaliongezeka kutoka 11 hadi 22 kutokana na mabadiliko mbalimbali yaliyotokea nchini na kwenye ukanda wa Afrika Mashariki.



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, wakipungia wananchi wakati wa sherehe za Muungano zilizofanyika Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 1965.*

Mathalani, kufuatia kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1964, ilibidi kila nchi mwanachama ikiwemo Tanzania, isimamie yenyewe mambo yake yahusuyo sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti), mabenki (pamoja na mabenki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabenki, na fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusu fedha za kigeni. Hivyo, Serikali zote mbili zilikubaliana kuwa masuala hayo yashughulikiwe na Serikali ya Muungano.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheikh Abeid Amani Karume, wakati huo akikaimu Urais wa Jamhuri, aliidhinisha Muswada wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1965 na hivyo kuruhusu mambo ya Muungano kuwa 12.

Nyufa zilipoongezeka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, masuala mengi zaidi yaliyokuwa yakiendeshwa na Taasisi za Jumuiya yakahamia kwa nchi wanachama. Tarehe 11 Agosti, 1967 masuala yaliyoongezwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano ni: Leseni ya Viwanda na Takwimu (Jambo la 13); na Elimu ya Juu (Jambo la 14).

Mwaka 1968, suala la maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa, na Gesi Asilia, liliongezwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano kuwa Jambo la 15.

Kadhalika, kufuatia kuvunjika rasmi kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 na kutungwa kwa Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Orodha ya Mambo ya Muungano iliongezeka kwa kuingizwa: Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo (Jambo la 16), Usafiri na usafirishaji wa anga (Jambo la 17), Utafiti (Jambo la 18), Utabiri wa Hali ya Hewa (Jambo la 19) na Takwimu (Jambo la 20).

Kutokana na kuvunjika kwa Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki, mwaka 1979 suala la Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano nalo liliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano na kuwa Jambo la 21.

Jambo la 22 la uandikishaji wa vyama vya siasa na mambo mengine yanayohusiana nayo, liliongezwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano kutokana na mapendekezo ya Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa Tanzania ya mwaka 1991 (Tume ya Nyalali) iliyopendekeza kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini[2].

Uratibu wa masuala ya Muungano uliendelea kuimarishwa kwa kuanzishwa kwa utaratibu wa vikao vya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2006. Jitihada hizo ziliendelea hadi mwezi Februari, 2008 ilipoundwa Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

Mwongozo wa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano uliandaliwa mwezi Februari, 2019 ili kuongeza ufanisi wa uratibu wa vikao na ufuatiliaji wa maagizo, maelekezo na maamuzi yanayotolewa katika vikao hivyo. Vikao hivyo viko katika ngazi tatu: Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ambacho Mwenyekiti wake ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ cha Kujadili Masuala ya Muungano ambacho Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza wake ni Waziri wa Nchi, OMR (SJMT) au Waziri wa Nchi, OMPR (SMZ), kutegemea na mahali kikao kitakapofanyika; Kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ cha Kujadili Masuala ya Muungano ambacho Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza wake ni Katibu Mkuu Kiongozi, (SJMT) au Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi (SMZ), kutegemea na mahali kinapofanyika kikao. Aidha, zipo Kamati Ndogo zilizoundwa kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi hoja zinazohitaji utatuzi wa haraka, ambazo ni: Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara; na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Vikao vya Kamati ya Pamoja huratibiwa na Sekretarieti inayojumuisha wajumbe kutoka SJMT na SMZ. Tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa vikao vya kujadili hoja za Muungano baina ya SJMT na SMZ mwaka 2006, jumla ya Hoja 25 ziliwasilishwa na kujadiliwa. Kati ya hizo, Hoja 22 zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa katika orodha ya Hoja za Muungano.

2. Maelezo ya kina kuhusu ongezeko la mambo ya Muungano yanapatikana kwenye Kitabu: Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo, Chapisho la Ofisi ya Makamu wa Rais, Mkuki na Nyota, 2022, Ukurasa wa 72–75.

Jukumu jingine la Ofisi ya Makamu wa Rais ni kuratibu ushirikiano wa pande zote mbili za Muungano baina ya Wizara, Idara na Taasisi za SJMT na SMZ. Serikali zote zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano. Vikao hivyo vya Kisekta hufanyika katika ngazi ya Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalamu. Lengo la kufanya vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano kwa manufaa ya Watanzania. Vikao hivyo vimekuwa vikijadili masuala ya kisekta, kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu kupitia mafunzo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa. Ushirikiano huu ni muhimu kwa kuwa unasaidia kuzitafutia ufumbuzi kwa haraka na kwa ufanisi changamoto za Muungano na za kisekta zilizopo na zinazojitokeza. Tathmini inaonesha Wizara za Kisekta zinapokutana, changamoto za Muungano zinapungua na Muungano unazidi kuimarika.

Elimu kwa umma kuhusu Muungano imekuwa ikitolewa kupitia vipindi vya redio na televisheni, makala magazetini, Semina, warsha, makongamano, maonesho ya Kitaifa, ziara za viongozi, machapisho mbalimbali na mitandao ya kijamii. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa kitabu kinachoelezea historia, chimbuko, misingi, na maendeleo ya Muungano ambapo nakala za Kitabu zimesambazwa kwa wananchi na Taasisi za Serikali na kuwekwa katika tovuti za Ofisi ya Makamu wa Rais (SJMT) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) ili kurahisisha upatikanaji wa kitabu hicho. Vilevile, kitabu hicho kimepata ithibati kwa ajili ya kutumika kama kitabu cha ziada kwa shule zote za Sekondari za Tanzania Bara na Zanzibar.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushirikiana katika kuandaa na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi hii imewezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira za muda kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Utekelezaji wa miradi hiyo umefanikisha kuinua hali ya wananchi, kukuza uchumi, kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii wa pande zote mbili za Muungano.

Hivyo, katika kipindi cha miaka 60 (1964–2024), Muungano umeendelea kuimarika ambapo Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu masuala yote ya Muungano kwa mujibu wa Katiba na Sheria.

## 2. Usimamizi wa Uhifadhi wa Mazingira

Katika kipindi cha mwaka 1964 hadi 1990, masuala ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira yalisimamiwa na Wizara za kisekta. Kutokana na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ya ardhi na misitu, Serikali ilianzisha programu na miradi mahsusi ya uhifadhi. Programu na miradi hiyo ilisimamiwa na Wizara yenye dhamana ya Maliasili ikiwemo Hifadhi Ardhi Dodoma (HADO, 1973) na Hifadhi Ardhi Shinyanga (HASHI, 1986). Vilevile, Wizara ya Kilimo ilisimamia Mradi wa Hifadhi Mazingira Iringa

(HIMA, 1989), Programu ya Kilimo–Mseto na Kudhibiti Mmomonyoko wa Udongo Lushoto (SECAP, 1984), na Programu ya Hifadhi ya Ardhi na Kilimo–Mseto Arumeru (SCAPA, 1989). Pia, Halmashauri ya Wilaya ya Babati ilisimamia Programu ya Usimamizi wa Mazingira (LAMP, 1992). Kwa ujumla, lengo la programu na miradi hii lilikuwa ni kuhifadhi ardhi, kuboresha kilimo na ufugaji, na kudhibiti mmomonyoko wa udongo.

Tangazo la Serikali Na. 293 la tarehe 20 Novemba 1970, lilianzisha Wizara ya Maliasili na Utalii kwa lengo la kuimarisha juhudi za Serikali katika hifadhi ya mazingira, ambapo msisitizo uliwekwa katika kusimamia maliasili zilizohifadhiwa kisheria zikiwemo misitu, wanyamapori, uvuvi na hifadhi za Taifa.

Katika kuendelea kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira, mwaka 1983 Serikali iliunda Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983. NEMC ilianza kazi rasmi mwaka 1986 ikiwa ni Taasisi ya Umma inayosimamiwa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nyumba na Maendeleo Mijini. Jukumu la NEMC lilikuwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira.

Katika kuimarisha zaidi uratibu na usimamizi wa masuala ya Mazingira nchini, mwaka 1992, Serikali ilianzisha Idara ya Mazingira katika Wizara ya Utalii, Maliasili na Mazingira kwa lengo la kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya hifadhi ya mazingira nchini.

Serikali iliendelea na jitihada mbalimbali za kuhifadhi mazingira, ikiwa ni pamoja na kuungana na jamii ya kimataifa katika kupanga na kutekeleza mipango na mikakati ya pamoja ya kuhifadhi mazingira. Hivyo, Tanzania ilishiriki Mkutano wa Kwanza wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa Uliohusu Mazingira na Maendeleo Endelevu, uliofanyika mwezi Juni, 1972 Stockholm, Sweden. Moja ya maazimio ya Mkutano huo ni kuanzishwa kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Usimamizi wa Mazingira Duniani (UNEP), lenye makao yake makuu jijini Nairobi, Kenya.

Mojawapo ya jitihada za kutekeleza maazimio hayo ni ushiriki wa nchi katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho ya kwanza ya kimataifa ya Siku ya Mazingira Duniani yalifanyika Geneva, Uswisi tarehe 5 Juni, 1973. Aidha, Tanzania ilifanya maadhimisho hayo kwa mara ya kwanza tarehe 5 Juni, 1993, ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Utalii Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Abubakar Mgumia. Lengo la maadhimisho hayo ni kukuza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa mazingira na kuhamasisha jamii husika kuchukua hatua mahsusi za kulinda na kuhifadhi mazingira. Aidha, Tanzania imeendelea kufanya maadhimisho hayo kila mwaka ili kuendelea kukuza uelewa wa jamii kuhusu hifadhi na utunzaji wa mazingira.

Mwaka 1992, Tanzania ilishiriki Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa Mazingira na Maendeleo ulioandaliwa na UNEP ambao ulifanyika Rio de Janeiro, Brazil. Miongoni mwa maazimio ya Mkutano huo, ni kuandaliwa na kusainiwa

kwa: Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi; Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai; na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kukabiliana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa. Aidha, Mkutano huo ulitoa msukumo wa Nchi Wanachama kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira. Mwaka 1994 Serikali iliandaa Mpango–Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira kwa lengo la kutekeleza maazimio hayo.

Kutokana na mazingira kuwa suala mtambuka, mwaka 1995 Serikali ilihamishia Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa lengo la kuipa nguvu ya kiutendaji katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Mwaka huohuo NEMC ilihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 719 la tarehe 28 Novemba, 1995.

Aidha, mwaka 1995, Serikali iliunda Kituo cha Uzalishaji Bora na Hifadhi ya Mazingira *(Cleaner Production Centre of Tanzania–CPCT)*, kwa lengo la kuimarisha juhudi za Serikali katika kuhimiza matumizi bora ya teknolojia za uzalishaji viwandani. Kituo hicho kilihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 1996. Kufuatia maombi ya Kituo hicho kwa Serikali ya kutaka kujiendesha na kujitegemea, mwaka 2005 Kituo hicho kilipata kibali cha kuwa Taasisi isiyo ya Kiserikali.

## 3. Uratibu wa Masuala ya Kuondoa Umaskini

Idara ya Kuondoa Umaskini iliundwa Novemba, 1995 katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kufuatia Azimio la Umoja wa Mataifa katika mkutano wake wa Maendeleo ya Jamii (World Summit on Social Development) uliofanyika Copenhagen, Denmark, mwezi Machi, 1995. Katika mkutano huo, nchi wanachama ziliazimia kuwa suala la kupambana na umaskini ni agenda muhimu. Hivyo, kila nchi mwanachama ilihimizwa iunde chombo mahsusi cha kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa jitihada za kupambana na umaskini.

Majukumu ya Idara ya Kuondoa Umaskini yalikuwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu na huduma kwa wananchi kuhusu masuala ya kupambana na umaskini, ikiwa ni pamoja na kusimamia na kufuatilia juhudi za kitaifa za kupambana na umaskini.

Hata hivyo, Idara ya Kuondoa Umaskini ilihamishiwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji mwezi Januari, 2006 kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais. Mwezi Februari, 2008, Idara hiyo ilihamishwa na kuwa chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi.

### 4. Usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Mara baada ya uhuru, Asasi za Kiraia ziliongezeka kwa kasi na hivyo kulazimu sheria nyingi kutungwa na nyingine kufanyiwa marekebisho kwa ajili ya uratibu wa asasi hizo. Baadhi ya sheria hizo ni: Sheria ya Makampuni Sura 212; Sheria ya Vyama Visivyo vya Kiserikali Sura 337; Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 11 ya mwaka 2005 na Sheria Na. 3 ya mwaka 2019 pamoja na kanuni zinazosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Sheria ya Jumuiya Sura 57; na Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu Sura 27.

Mwaka 1990 Kitengo cha Uratibu wa Asasi za Kiraia kilianzishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ziliratibiwa hadi mwaka 1999. Mwaka 2000, Kitengo hicho kilihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 468 la Tarehe 1 Desemba, 2000 na kiliendelea na shughuli za usajili na uratibu wa Mashirika hayo. Baada ya kupitishwa kwa Sheria Na. 24 ya mwaka 2002, Kitengo hicho kilipewa hadhi ya Idara na kuwa na majukumu ya kusajili, kusimamia, kuratibu na kufuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi mbalimbali. Idara hiyo ilihamishiwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mwezi Januari, 2006.

## 1.4 Madhumuni ya Kitabu

Madhumuni ya Kitabu hiki ni kukuza uelewa wa jamii na kuweka kumbukumbu sahihi kuhusu uongozi, majukumu ya kikatiba, wajibu na mafanikio ya Ofisi ya Makamu wa Rais tangu kuanzishwa kwake mwaka 1964. Aidha, Kitabu hiki kitakuwa rejea muhimu kuhusu masuala ya Muungano, ambayo ni jukumu la kudumu tangu kuanzishwa kwa Ofisi hii, na masuala ya Uhifadhi wa Mazingira.

Umuhimu wa Kitabu hiki unajitokeza zaidi kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, ambayo inaonesha kuwa asilimia 77.3 ya Watanzania ni vijana chini ya umri wa miaka 35 ambao hawakushuhudia uhuru wa Tanganyika tarehe 9 Desemba, 1961, Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 12 Januari 1964 na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 1964. Hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais ina dhamana ya kuhakikisha jamii inapata uelewa sahihi kuhusu Muungano.

# MUUNDO, UONGOZI NA MAJUKUMU

Sura hii inaeleza kuhusu Muundo, Uongozi, Majukumu na utekelezaji wake katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Aidha, inaeleza kwa muhtasari wasifu wa Makamu wa Rais waliohudumu OMR na mchango wao katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kuanzia mwaka 1964 hadi 2024.



# Sheikh Abeid Amani Karume

## Wasifu

Sheikh Abeid Amani Karume, alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1964 hadi 1972 katika kipindi cha uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sheikh Karume alizaliwa tarehe 4 Agosti, 1905 katika Kitongoji cha Pongwe, Kijiji cha Kiongoni, Mwera, Wilaya ya Kati Unguja–Zanzibar. Alikuwa mtoto wa kwanza kati ya watoto watano waliozaliwa katika familia ya Mzee Amani Karume na Bi. Amina binti Kadir (Amina Kadudu). Baba yake mzazi, Mzee Amani Karume, alifariki dunia mwaka 1909, wakati Sheikh Karume akiwa na umri wa miaka minne. Alipata elimu ya awali katika Kijiji cha Mwera.

Familia yake ilikuwa ya wakulima wa kipato cha chini, hali ambayo ilimjengea ari ya kufanya kazi nyingi kuiwezesha familia yake kujikimu. Hali hiyo na historia ya familia yake, vilimjenga kuwa shujaa wa kupigania haki za wanyonge na kuwa kiongozi mwenye dira ya kimapinduzi. Sheikh Karume ana historia ya kisiasa iliyotukuka: Kiongozi wa Jumuiya ya Waafrika (African Association) wakati wa ukoloni; Rais wa Kwanza wa Afro–Shirazi Party (ASP); Kiongozi wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar; Mpigania uhuru na mwana Umajumui wa Kiafrika (Pan Africanist); na Mwasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

## Ajira na Uongozi

Mwaka 1919, Sheikh Karume alipeleka barua ya kuomba kazi ya ubaharia, lakini alikataliwa kutokana na kuwa na umri mdogo wa miaka kumi na nne. Hata hivyo, hakuvunjika moyo. Aliomba tena kazi hiyo akiwa na umri wa miaka kumi na tano na kufanikiwa. Kati ya mwaka 1920 hadi 1938, Sheikh Karume alifanya kazi ya ubaharia wa meli mbalimbali za kigeni zikiwemo Golden Crown, Cheko na meli ya British Indian Steam Navigation Company ya Uingereza. Katika kazi zake za ubaharia, alijifunza mengi kutoka mataifa ya Ulaya na kubaini jinsi mabepari walivyotumia hila na ujanja kuzinyonya nchi za Afrika. Kupitia uzoefu huo, aliona umuhimu wa kuungana na wenzake katika kukabiliana

na hila za mabepari, hivyo kuanzisha Umoja wa Wafanyakazi wa Pwani (Bandarini).

Kwa kuwa wakoloni hawakuruhusu kabisa uanzishwaji wa vyama vya kisiasa, njia pekee ya Waafrika kukutana na kubadilishana mawazo ilikuwa kupitia vyombo vya michezo na burudani. Hivyo, mwaka 1920, Sheikh Karume alijiunga na Timu ya mpira wa miguu ya New Generation ya Zanzibar na pia alikuwa msaidizi wa nahodha wa Timu ya African Sports Club ambazo ziliwakusanya pamoja Waafrika na kuanzisha Jumuiya ya Waafrika (African Association) mwaka 1934. Kuanzishwa kwa Jumuiya hiyo kulifanya Sheikh Karume kuwa miongoni mwa Waasisi wa harakati za kupigania masuala ya kijamii na kiuchumi ya Waafrika. Sheikh Karume alishirikiana na viongozi wa African Association of Zanzibar (AAZ): Bwana Augustine Ramadhani (Rais), Bwana Semi Sindi (Katibu Mkuu) na Bwana William Limo (Mweka Hazina). Mwaka 1938, Sheikh Karume alishika nafasi ya Katibu Mkuu wa AAZ.

Aidha, Sheikh Karume alianzisha Chama cha Dansi cha Waafrika katika Mtaa wa Michenzani, Unguja mwaka 1940 na mwaka 1946, alianzisha Umoja wa Mabaharia na wamiliki wa vyombo vya baharini Zanzibar na akawa mmoja wa viongozi wa umoja huo. Wakati huo, nchi nyingi za Afrika zilikuwa katika harakati za kupigania uhuru wao, hivyo kuwepo kwa asasi za kiraia kama hizo kuliwapa waafrika majukwaa adhimu (yasiyo rasmi) ya kubadilishana mawazo. Mwaka



▲

*Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa ASP (aliyekaa katikati), Sheikh Thabit Kombo Jecha, Katibu Mkuu wa ASP, wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya waasisi wa ASP waliohudhuria uzinduzi wa kuzaliwa kwa ASP, Mjini Unguja, tarehe 5 Februari, 1957.*

1947, Serikali ya Kikoloni ilianzisha Serikali za Mitaa na miaka saba baadaye kulianzishwa Baraza la Mji ambapo Sheikh Karume alichaguliwa kuwa Diwani wa eneo la Ng'ambo, Unguja.

Tarehe 5 Februari, 1957 Jumuiya ya Waafrika (AAZ) na Jumuiya ya Washirazi (Shiraz Association–SA) ziliungana na kuunda chama kipya cha siasa kilichoitwa Afro–Shirazi Party (ASP) baada ya Serikali ya Kisultani kuruhusu shughuli za kisiasa kufanyika rasmi. Sheikh Karume alikuwa ni miongoni mwa viongozi waliofanikisha kuungana kwa AAZ na SA kuunda ASP, ambapo Sheikh Karume alichaguliwa kuwa Rais wa chama hicho. Mwalimu Julius K. Nyerere alikuwa miongoni mwa mashuhuda wa tukio hilo muhimu la kisiasa Zanzibar[3].

Kuanzia mwaka 1957, Sheikh Abeid Amani Karume alikuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria kupitia ASP akianzia Jimbo la Ng'ambo katika uchaguzi wa Kwanza Zanzibar uliofanyika mwaka 1957. Baada ya kuongezwa Majimbo katika uchaguzi wa mwaka 1961 na 1963, Sheikh Karume aligombea na kushinda katika Majimbo ya Jang'ombe na Kwahani, ambapo aliendelea kuhudumu katika nafasi hiyo hadi Desemba, 1963. Sheikh Karume aliwaongoza Wazalendo wa ASP katika Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964, yaliyokata minyororo ya ukoloni mkongwe wa Kisultani kutoka Oman na kutangaza Zanzibar kuwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikaundwa chini ya ASP, ikiwajumuisha viongozi na wafuasi wa chama kidogo cha Umma, kilichoongozwa na Abdulrahman Babu, mwanasiasa wa siku nyingi Zanzibar wakati huo.




*Moja ya mabango ya kampeni ya ASP katika uchaguzi wa mwaka 1963.*

3. Mohamed, A. A., Kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi. TPH, Dar es Salaam, 1979, uk. 4.

Kutokana na Uzalendo wake na ari yake ya Uanamajumui wa dhati wa Kiafrika, Sheikh Abeid Amani Karume alihudumu nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kwa muda wa miezi minne tu baada ya Mapinduzi na tarehe 26 Aprili, 1964 alikuwa mmoja wa Waasisi wa Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.



▲

*Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, akipeana mkono na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, mara baada ya Sheikh Karume kuapishwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kushoto kwa Mwalimu ni Ndugu Joseph A. Namata, Katibu Mkuu wa Rais, Ikulu Dar es Salaam, tarehe 27 Aprili, 1964.*

Tarehe 27 Aprili, 1964 kwa kuzingatia Hati ya Makubaliano ya Muungano Sheikh Abeid Karume aliteuliwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na Mbunge wa Bunge la Muungano. Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lilibadilishwa tarehe 28 Oktoba, 1964 kupitia Sheria ya Muungano, Na. 61 ya mwaka 1964, kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sheikh Abeid Amani Karume aliendelea na wadhifa wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hadi tarehe 7 Aprili, 1972 alipouawa kwa kupigwa risasi.

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (1964–1972)

Chini ya uongozi wa Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1964–1985)

Muundo wa Ofisi mbili za Makamu wa Rais umeelezwa kwa kina kwenye aya ya 1.1 na 1.2 ya Kitabu hiki. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilikuwa Zanzibar, na kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 235 la tarehe 28 Aprili, 1964, Makamu wa Kwanza wa Rais alisaidiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Msaidizi Mkuu katika kutekeleza majukumu ya kisheria na kikatiba ya Muungano.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria wa OMR (1964–1972)

Kipindi cha uongozi wa Sheikh Abeid Amani Karume, kilikuwa cha ujenzi wa misingi imara ya Muungano upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vilevile upande wa wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Kilikuwa kipindi tete kisiasa na kiulinzi kilichotawaliwa na shamrashamra za Muungano na vilevile manung'uniko ya chini kwa chini hususan upande wa Tanzania Zanzibar ambapo Serikali iliyopinduliwa tarehe 12 Januari, 1964 ilikuwa bado na mashabiki wakililia fursa walizopoteza chini ya utawala wa kikoloni wa Kisultani kutoka Oman. Manung'uniko haya yaliandamana na upotoshaji kwa njia ya machapisho mbalimbali, kauli hasi kupitia vyombo vya habari hasa redio na mawasiliano kati ya mtu na mtu ("redio kifua" kama inavyotumika Zanzibar) kuhusu Mapinduzi na Muungano.

Hali hiyo ilihitaji hatua muhimu kadhaa zichukuliwe na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mapema ilivyowezekana kudhibiti uchochezi huo:

1. Kuibua na kutekeleza Sera na mipango inayogusa hisia/maslahi ya wananchi walio wengi ambao walinyimwa fursa/haki mbalimbali kipindi cha ukoloni ili wananchi waone tofauti kati ya kutawaliwa na kujitawala. Mambo matano yakatangazwa na utekelezaji wake ukaanza:

- Ugawaji bure wa ardhi (ekari tatu tatu) kwa wananchi/familia zilizokuwa na uhitaji wa maeneo ya kuishi na kuendeshea shughuli za kujikimu, kikiwemo kilimo. Tarehe 11 Novemba, 1965 Sheikh Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, alizindua zoezi hilo la kugawa ardhi kijiji cha Dole. Hadi mauti yanamfika mwaka 1972, ekari zaidi ya 24,000 zilikuwa zimegawiwa kwa wananchi wenye uhitaji Unguja na Pemba.
- Elimu Bure kwa Wote. Sheikh Karume, alitangaza sera hiyo tarehe 23 Septemba, 1964 kwa kutambua kuwa wakoloni waliwanyima Waafrika fursa za elimu ili waendelee kuwatawala, kuwanyonya, kuwanyanyasa na kuwabagua kwa urahisi. Tangazo hilo la utoaji wa elimu bure liltanguliwa na katazo kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule kutumikishwa mashambani na sehemu mbalimbali za kazi/biashara na upigaji marufuku wa ubaguzi wa rangi katika utoaji wa elimu. Matokeo chanya ya utekelezaji wa sera hiyo yalionekana mara moja: udahili wa watoto wa ki–Afrika kuanzia kidato cha kwanza hadi cha 6 ambao kabla ya Mapinduzi ulikuwa 11.7% ya wanafunzi wote wa sekondari Unguja na Pemba, ulipanda hadi 66.1% ndani ya miaka miwili tu ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Kipindi hicho, Waafrika walikuwa zaidi ya 80% ya wakazi wote wa Zanzibar.
- Matibabu Bure kwa Wote. Ili kufanikisha utekelezaji wa sera hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitaifisha hospitali za binafsi na kupiga marufuku matabaka katika utoaji huduma za afya katika hospitali za Serikali. Kabla ya Mapinduzi, Zanzibar ilikuwa na jumla ya zahanati na vituo vya afya 32 ambavyo viliongezeka hadi kufikia 112 ndani ya miongo mitatu ya Mapinduzi na kuongeza wastani wa mtu kuishi (life expectancy) kutoka miaka 43 mwaka 1963 hadi miaka 48 mwaka 1988.
- Miaka mingi ya utumwa na kutawaliwa na wageni iliwaweka wananchi wengi katika ufukara uliokithiri wa kukosa hata mahali pa kujisitiri. Ndipo uamuzi ukafikiwa mapema mwaka 1964 kujenga makazi bora ya kisasa kwa wananchi waliokuwa na uhitaji wa mahali pa kuishi katika maeneo yafuatayo: Kikwajuni, Michenzani, Kilimani, Gamba, Makunduchi na Bambi Mpapa kwa upande wa Unguja; na Machomanne, Wete, Madungu, Micheweni, Kengeja na Mkoani upande wa Pemba.
- Ili kufuta alama za kitumwa Zanzibar, mikokoteni ya abiria iliyokuwa ikikokotwa na Waafrika kubeba Wazungu, Waarabu na Wahindi ilipigwa marufuku pamoja na biashara ya uwekaji rehani wa vito na vitu vingine vya thamani ambao ilionekana ni kichocheo cha umaskini.
- Pamoja na kuwapatia ekari tatu tatu za ardhi bila malipo, matibabu bure na makazi bora ya bure ya kuishi, Sheikh Karume na wanamapinduzi wenzake waliamua kuwapa wazee wa Zanzibar posho ya kujikimu ya shilingi 50 kila mwezi.

2. Kuanzisha taasisi mbalimbali za kutoa huduma muhimu ndani ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuchochea uchumi nchini kama vile:

- Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ambayo ni benki ya biashara iliyoanzishwa mwaka 1966 na Serikali ya Zanzibar kuhudumia watu binafsi, biashara ndogondogo, za kati na wateja wakubwa, yakiwemo makampuni. Benki hiyo ina matawi sehemu mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) lilioanzishwa mwaka 1969 kutoa huduma bora za bima kwa watu binafsi, makampuni na taasisi za serikali ili kupanua wigo wa biashara Zanzibar na Tanzania Bara. ZIC ina matawi 10 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. Kusainiwa kwa mabadiliko ya nyongeza ya Jambo la 12 katika orodha ya Mambo ya Muungano ambalo ni sarafu, noti, mabenki, fedha za kigeni na usimamizi wa masuala ya fedha baada ya kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1964. Kwa msingi huo, kila nchi mwanachama wa Jumuiya ililazimika kuwa na sarafu na mipango yake ya kusimamia mambo ya kibenki na fedha. Hivyo, SJMT na SMZ zilikubaliana kuwa suala hilo lisimamiwe na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mabadiliko hayo yalisainiwa na Sheikh Karume akiwa Kaimu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania[4] tarehe 10 Juni, 1965.

4. Kuongezwa kwa Mambo mengine matatu ya Muungano kuanzia mwaka 1967 hadi 1968 ambayo ni: Leseni za viwanda na takwimu (Jambo la 13); Elimu ya juu (Jambo la 14); na Maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa, na gesi asilia (Jambo la 15). Mambo yote hayo yaliongezwa kwa makubaliano na kwa kuzingatia masharti ya Katiba.

4. Kwa mujibu wa Ibara ya 9 ya Katiba ya Muda ya Tanzania ya mwaka 1965, Ofisi ya Rais inapokuwa wazi au Rais hayupo nchini wakati wowote ule, shughuli za Ofisi ya Rais zitatekelezwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na kama hayupo, zitatekelezwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.



▲

*Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar akihutubia Mkutano wa Mabalozi wa Umoja wa Nchi Huru za Bara la Afrika (OAU) na wananchi, ambao ulifanyika katika viwanja vya Jangwani, Dar es Salaam kujibu hoja za mabeberu kuhusu mambo mbalimbali ya Afrika, mwaka 1966.*



▲

*Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akikagua shughuli za utoaji wa huduma za afya katika hospitali ya Wilaya ya Pangani, Tanga. Kushoto ni Mhe. Waziri Juma, Mkuu wa Mkoa wa Tanga. Ziara hiyo iilifanyika tarehe 5 Machi, 1969.*



▲

*Wananchi wa Zanzibar wakishiriki katika kusaidia ujenzi wa moja ya nyumba za makazi wakati wa Utawala wa Sheikh Abeid Amani Karume Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika eneo la Michenzani Zanzibar. Picha hii ilipigwa mwanzoni mwa mwaka 1965 ambapo ujenzi huo uliendelea hadi miaka ya 1970.*



◀

*Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (akiwa na fimbo), akiwa katika ziara ya kukagua sehemu ya ujenzi wa Mji Mpya Bambi, Unguja (kwa gharama ya jumla ya pauni za Uingereza £1.4 milioni) kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya wananchi. Wa tatu kulia kwake, ni Aboud Jumbe Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, na kushoto kwake ni Mheshimiwa Edington Kisasi, mjumbe wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, tarehe 16 Machi, 1966.*

*Baadhi ya nyumba za maendeleo za wananchi zilizojengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1966 katika Kijiji cha Bambi, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.*





*Mkokoteni wa abiria maarufu kama rick shaw kipindi cha ukoloni ikionekana Markiti Kuu ya Darajani-Zanzibar. Mikokoteni hii ilikuwa inatumiwa kuwabeba Waarabu, Wazungu na Waasia ikitumia nguvukazi ya Waafrika. Kwa Sheikh Karume na wanamapinduzi wenzake, mikokoteni hiyo ilikuwa kumbukizi ya kudhalilisha utu wa Mwafrika, Septemba, 1953.*

## Anavyokumbukwa

- Alikuwa kiongozi wa kwanza duniani katika karne ya 20 aliyeachia uongozi wa juu katika Taifa lake na kukubali nafasi ya chini ya uongozi ili kuwezesha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Sheikh Karume aliishi ndoto ya muda mrefu ya umajumui wa kiafrika ya kuunganisha Bara zima la Afrika na kuunda Shirikisho la Afrika kwa vitendo.
- Sheikh Karume alipendelea, baada ya kazi rasmi za Serikali, kuvaa kanzu, kofia, baraghashia, vikoi, viatu vya makubadhi na kubeba fimbo. Alijijengea utamaduni wa kuongea moja kwa moja na makundi mbalimbali ya wananchi aliopenda kuwaita "Wana wa Nchi" na kukutana mara kwa mara na wazee wenzake ili kubadilishana nao mawazo na kucheza zumna (dominoes).
- Alijijengea utamaduni katika kipindi chake chote cha uongozi wa miaka minane, kuwasilisha kwa wananchi taarifa ya mapato na matumizi ya SMZ kupitia mikutano ya hadhara.
- Kila alipopata fursa kuongea na wananchi Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara, hakukosa kuwakumbusha kuhusu fedheha na madhila mengine mengi ya kutawaliwa, thawabu ya kupambana kudai uhuru kwa njia nyingi ikiwemo ya kuchukua silaha kama ASP ilivyofanya tarehe 12 Januari, 1964. Aidha, kuwakumbusha umuhimu wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika kuuishi umajumui wa Kiafrika (Pan–Africanism) na ndoto ya vuguvugu hilo ya



▲

*Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia mkutano wa hadhara akiwa katika ziara ya kikazi Wilayani Songea, Mkoa wa Ruvuma. Kushoto kwa Makamu wa Kwanza wa Rais ni Mhe. Edward Barongo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, na kulia kwa Sheikh Karume ni Mhe. Bibi Titi Mohamed, Mwenyekiti wa UWT na nyuma yake ni Sheikh Thabit Kombo (mwenye barghashia), Katibu Mkuu wa ASP, Septemba 1966.*





kuunganisha ya Afrika nzima na hatimaye kuunda Shirikisho la Afrika.

- Alisimamia Mabadiliko ya Katiba ya Muda ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1965 ambayo yaliainisha muundo wa Serikali mbili za Muungano kwa mujibu wa Hati ya Muungano.
- Alikuwa na uthubutu wa kuanzisha miradi mipya ya kisasa katika ukanda wa mashariki na kati wa Afrika, mathalan: kuanzisha kituo cha kwanza cha televisheni ya rangi katika Afrika Mashariki na Kati mwaka 1972; kujenga uwanja wa kisasa wa michezo wa Amaan, Unguja mwaka 1970 wenye taa za kuruhusu kutumika hata nyakati za usiku; na kujenga barabara za kisasa za njia mbili na kuifanya Zanzibar kuwa kivutio kwa wananchi Afrika Mashariki na Kati.
- Alitoa mchango wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la timu ya Young Africans na pia alisaidia ujenzi wa jengo la timu ya Sunderland. Majengo hayo mawili yako Dar es Salaam. Aidha, alishauri kubadili jina la timu ya Sunderland kuwa Simba.



◄ *Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia wananchi, viongozi na wageni katika maadhimisho ya miaka mitatu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika uwanja wa Mnazi Mmoja Zanzibar, tarehe 12 Januari, 1967.*

*Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akisalimia waamuzi na wachezaji wa timu za Mikoa ya Kilimanjaro na Pwani katika fainali ya Kombe la Taifa (picha ya juu) na picha ya chini, Sheikh Karume akiwa sehemu ya watazamaji wa mechi hiyo, Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam, tarehe 6 Julai, 1967.*





## Mauti

Sheikh Abeid Amani Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, aliuawa kwa kupigwa risasi Ijumaa jioni, Makao Makuu ya ASP Kisiwandui Unguja tarehe 7 Aprili, 1972, akiwa na umri wa miaka 67. Alizikwa Jumapili tarehe 9 Aprili, 1972 pembezoni mwa Makao Makuu ya ASP ambayo kwa sasa ni Afisi Kuu ya CCM Kisiwandui–Zanzibar.

Baada ya kifo chake, Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi aliteuliwa kuhudumu nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

# Viongozi waliohudumu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1964 hadi 1972



SHEIKH ABEID AMANI KARUME
Makamu wa kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
(1964-1972)



MHE. ABOUD M. JUMBE
Waziri wa Nchi
Afisi ya Makamu wa kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(1964-1972)



MHE. ABDULAZIZ A. KHAMIS
Waziri Mdogo katika Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar
(1964-1968)



BW. ABDALLA S. MUGHEIRY
Katibu Msaidizi Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar
(1964-1972)



# Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa

## Wasifu

Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa alikuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1964 hadi 1977, chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa alizaliwa tarehe 27 Februari, 1926 katika Kijiji cha Matepwende, Tarafa ya Ligera, Wilaya ya Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma, Tanzania Bara. Mheshimiwa Kawawa alikuwa ni mtoto wa pili katika familia ya watoto watano ya Mzee Fundi Mfaume Kawawa na Bi. Zamaradi binti Chikuse. Baba yake alikuwa ni mtumishi wa serikali ya kikoloni kwa nafasi ya Askari Wanyamapori. Akiwa mwajiriwa wa serikali ya kikoloni, alikuwa akihamishwa mara kwa mara, akiambatana na familia yake na hivyo kupelekea mtoto wake Mheshimiwa Rashidi kulazimika kuhama kutoka Kata ya Lumesule, Mtwara kwenda Kilwa Kivinje na baadaye Liwale, Lindi. Mheshimiwa Rashidi Kawawa alikuwa mtu jasiri, mahiri na mtiifu katika kutekeleza maamuzi na maelekezo.

Mwaka 1935 hadi 1941, Mheshimiwa Kawawa alipata Elimu ya Msingi katika Shule ya Tunduru, mjini Lindi. Aliendelea na Elimu ya Kati (Middle School) katika Shule ya Dar es Salaam African Central School mwaka 1942 hadi 1947. Aidha, alipata elimu ya sekondari katika Shule ya Wavulana Tabora kati ya mwaka 1947 hadi 1949.

Alikuwa Mpigania uhuru; Mwasisi wa Muungano; Waziri Mkuu wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kiongozi wa kwanza kushika wadhifa wa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Katibu Mkuu wa Pili wa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Alikuwa maarufu kwa jina la 'Simba wa Vita' kwa sababu alikuwa na uthubutu wa kusimamia utekelezaji wa maamuzi mazito ya Chama na Serikali.

## Ajira na Uongozi

Akiwa na umri wa miaka 23, Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa aliajiriwa na Serikali ya kikoloni katika Idara ya Kazi za Jamii akiwa

Karani wa Fedha katika Kitengo cha Huduma za Maji. Ajira hiyo ilianza Desemba, 1949 baada ya kuwa amehitimu darasa la kumi na mbili katika Shule ya Wavulana Tabora. Mwaka 1951 alipata uhamisho wa kiidara kutoka Idara ya Kazi za Jamii kwenda Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Maktaba ya Filamu za Sinema.

Kabla ya kuingia katika harakati za kupigania Uhuru, Mheshimiwa Kawawa alikuwa ni miongoni mwa waanzilishi wa Shirikisho la Wafanyakazi wa Tanganyika mwaka 1955, ambapo alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa kwanza wa Shirikisho hilo. Ni katika nafasi hii, ndipo alianza kushiriki kwa nguvu zaidi katika harakati za kupigania Uhuru wa Tanganyika akihamasisha Wafanyakazi. Februari 1956, Mheshimiwa Kawawa aliacha nafasi ya uongozi katika Shirikisho hilo kutokana na kuajiriwa Serikalini, hivyo kutoruhusiwa kujihusisha na siasa.

Mheshimiwa Kawawa aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Tanganyika African National Union (TANU) mwaka 1957 hadi 1960, alipochaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa TANU. Mwaka 1960 hadi 1961, alikuwa Waziri wa Serikali za Mitaa na Nyumba kwenye Serikali ya Madaraka iliyoundwa na Rais wa TANU.

Tarehe 22 Januari, 1962 aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanganyika kufuatia Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kujiuzulu wadhifa huo, kwa lengo la kuimarisha Chama cha TANU. Wakati anachukua wadhifa huo alikuwa Waziri asiyekuwa na Wizara Maalumu. Tarehe 9 Desemba, 1962 Mheshimiwa Kawawa aliteuliwa tena kuwa Waziri Mkuu, baada ya Tanganyika kuwa Jamhuri na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuapishwa kuwa Rais Mtendaji, Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu[5].

Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa alihudumu katika nyadhifa za Makamu wa Pili wa Rais (1964–1972), Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia alikuwa Waziri wa Ulinzi (1972–1977). Katika kipindi cha uongozi huo, alikuwa Mjumbe wa kuchaguliwa wa Baraza la Taifa (Bunge) wa Jimbo la Nachingwea (1962–1975) na baada ya Jimbo la Nachingwea kugawanywa na kupatikana Jimbo la Liwale, alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Liwale (1975–1985). Aidha, baada ya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri ya mwaka 1977, yaliyompa Mhe. Edward Moringe Sokoine kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kawawa aliteuliwa kuwa Waziri wa Ulinzi na aliendelea na dhamana hiyo hadi mwaka 1980. Pamoja na wadhifa huo, aliendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Usimamizi wa Shughuli za Chama hadi Oktoba, 1982. Mhe. Rashidi Kawawa alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kuanzia Novemba, 1982 hadi 1987. Septemba, 1990 Mkutano Mkuu Maalamu wa Chama ulimchagua Mheshimiwa Rashidi Kawawa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM, nafasi aliyohudumu hadi 1993 alipoamua kung'atuka.

5. Uhuru uliopatikana tarehe 9 Desemba, 1961 haukutoa mamlaka kamili ya kuendesha nchi kwani Malkia wa Uingereza bado alikuwa Mkuu wa Nchi na Mwalimu Nyerere alikuwa Mkuu wa Serikali. Hivyo, tarehe 9 Desemba, 1962 nchi ilipata mamlaka kamili ya kujiendesha yenyewe ambapo Ukuu wa Nchi na Ukuu wa Serikali viliunganishwa pamoja.

# Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Chini ya uongozi wa Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1964–1985)

**Mwaka 1964 hadi 1972**

Matangazo ya Serikali Na. 235 la tarehe 28 Aprili, 1964 na Na. 293 la tarehe 20 Novemba, 1970 kama yanavyosomeka katika aya ya 1.2 (a) na (b) katika Kitabu hiki.

**Mwaka 1972 hadi 1977**

Katiba ya muda ya mwaka 1965 ilifanyiwa marekebisho na kumuongezea Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wadhifa wa Waziri Mkuu, hivyo, Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa akawa kiongozi wa kwanza Tanzania Bara kuwa na kofia hizo mbili baada ya Muungano ambapo muundo na majukumu yake yameelezwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 40 la tarehe 24 Februari, 1972 na Tangazo la Serikali Na. 10 la tarehe 9 Januari, 1976 katika aya ya 1.2 (c) na (d) katika Kitabu hiki.

# Utekelezaji wa Majukumu ya OMR Kikatiba, Kisera na Kisheria (1964–1977)

Uongozi wa Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa, ulikuwa na vipindi viwili, kipindi cha kwanza alikuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kipindi cha pili alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kipindi cha uongozi wake, masuala mbalimbali yalijitokeza: Mdororo wa uchumi kutokana na kipindi kirefu cha ukame, Kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1967 kulikosababisha kuongeza gharama kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na kubeba majukumu yaliyokuwa yanasimamiwa na Bodi hiyo na uhaba mkubwa wa wataalamu wa fani mbalimbali katika uendeshaji wa Serikali.

Kutokana na changamoto hizo, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilitekeleza yafuatayo:

- Kusimamia uanzishwaji wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa Sheria Na. 16 ya mwaka 1964 (National Service Act, 1964) ambapo utekelezaji wake ulianza Novemba 1964, kundi la kwanza la vijana 486 liliripoti Mgulani JKT na kuitwa 'Operesheni Maendeleo'.
- Kusimamia uanzishwaji wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania baada ya kuunganishwa kwa Majeshi ya Tanganyika Military Force na Jeshi la Ukombozi la Zanzibar Tarehe 1 Septemba, 1964.
- Kusimamia utungaji wa Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 iliyobadili ile ya muda ya mwaka 1965.
- Kusimamia uanzishwaji wa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) ikiwa Idara ya Wizara ya Habari, Utangazaji na Utalii mwaka 1965 ambapo mwaka huo huo, Sauti ya Unguja ilibadilishwa na kuwa Sauti ya Tanzania Zanzibar. Aidha, RTD ilijiunga na Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) ambapo kila saa 1:00 usiku ili-



◀

*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akimuapisha Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Dar es Salaam. Kushoto kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ni Bw. Timothy Apiyo, Katibu Mkuu Kiongozi, Tarehe 27 Aprili, 1964.*



▲

*Mwonekano wa nyumba za vijiji vipya vya ujamaa vilivyoanzishwa na Serikali katika baadhi ya Mikoa hapa nchini. Hiki ni kijji cha Matamba kilichopo Mkoani Iringa vilivyoanza kujengwa na Serikali kuanzia mwezi Machi, 1973.*



▲

*Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa pili kulia), akihutubia viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Tanzania (FAT) na wachezaji wa timu ya mpira wa miguu ya mkoa wa Pwani kabla ya kukabidhi Kombe la Taifa kwa timu ya mkoa wa Pwani, tarehe 10 Septemba, 1967.*

▶

*Mhe. Rashidi M. Kawawa, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), Mhe. Adam Sapi Mkwawa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia), na Mhe. Aboud Jumbe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania (kushoto) wakiwa katika mafunzo ya wiki mbili ya kijeshi katika kambi ya JKT Ruvu, Januari, 1968.*



tangaza taarifa ya habari ya STZ; na RTD ilijiunga na STZ ambapo kila saa 2:00 usiku, ilitangaza taarifa ya habari ya RTD. Lengo ni kutangaza habari na kukuza uelewa wa wananchi wa pande mbili kuhusu masuala ya Muungano.

- Kusimamia uanzishwaji wa Vijiji vya Ujamaa na utekelezaji wa Azimio la Arusha mwaka 1965 hadi 1975. Hadi kufikia mwaka 1977, asilimia 90 ya wakazi wa Vijijini walikuwa wakiishi katika Vijiji vya Ujamaa.
- Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Kujitegemea ya Mwaka 1967, lengo likiwa ni kubadilisha mtazamo, fikra, uelewa, mazoea ya wananchi na viongozi ili kujenga mfumo wa maisha wa kujitambua na kujitegemea. Sera hiyo ilisisitiza matumizi ya sayansi na teknolojia na kuifanya elimu kuwa na nguvu ya kuendeleza ujenzi wa uchumi wa kijamaa.
- Kusimamia utekelezaji wa Sera ya elimu ya watu wazima ya mwaka 1967 ambapo hadi kufikia mwaka 1970, idadi ya watu waliojua kusoma na kuandika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifikia asilimia 94.

## Anavyokumbukwa

Katika kipindi cha Uongozi wake, Mheshimiwa Kawawa anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Aliwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Muungano wa kutangaza jina jipya la Nchi kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 28 Oktoba, 1964.
- Alisimamia utungaji wa wimbo wa Taifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Desemba, 1964.
- Alisimamia mipango ya elimu ya watu wazima kuanzia mwaka 1964 hadi 1974.
- Alisimamia Azimio la Musoma mwaka 1974 lililoweka mkazo kuhusu elimu ya msingi kwa wote, uchangiaji wa elimu ya juu na kufanya kazi kabla ya kujiunga na chuo kikuu, isipokuwa kwa wasichana waliporuhusiwa kujiunga moja kwa moja.
- Alitoa agizo la kuanzisha Idara ya wafanyakazi ambayo baadae iliitwa Idara ya Elimu na Ushirikishwaji wa wafanyakazi tarehe 2 Mei, 1974.
- Alikuwa na dhamana ya masuala ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa muda wa miaka 15, kuanzia mwaka 1964 hadi 1976 na kuanzia mwaka 1977 hadi 1980, aliteuliwa kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa mujibu wa Ibara ya 85(1) ya Katiba ya Muda ya Tanzania ya mwaka 1965 ilitamka kuwa neno "Waziri" linahusisha Makamu wa Rais lakini halijumuishi Waziri Mdogo[6].

6. Waziri Mdogo ni wadhifa uliotumika chini ya Katiba ya Muda ya Tanzania ya mwaka 1965, wadhifa huo ulifutwa na Katiba ya Kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 iliyoanzisha wadhifa wa Naibu Waziri.



▲

*Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa, Waziri Mkuu na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (aliyeshika fimbo ya kutembelea), akifuatana na Viongozi wa Elimu ya Watu Wazima, TANU na Serikali, wakikagua maendeleo ya Mradi wa Kusoma kwa Ufanisi, Magomeni-Dar es Salaam, tarehe 14 Desemba, 1972.*

## Mauti

Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 83 Alhamisi tarehe 31 Desemba 2009 na kuzikwa Jumamosi tarehe 2 Januari, 2010 kwenye makazi yake katika Kijiji cha Madale, nje kidogo ya Jiji la Dar es Saalam.

# Viongozi waliohudumu Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1964 hadi 1977



MHE. RASHIDI MFAUME KAWAWA
Waziri Mkuu
na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(1964-1977)



MHE. LAWI N. SIJAONA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu
wa Pili wa Rais
(1964-1967)



MHE. BHOKE MUNANKA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa
Rais (Kazi Maalumu)
(1964-1972)



MHE. EDWARD M. SOKOINE
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu
wa Pili wa Rais
(1972-1975)



BW. AARON E. MWAKANG'ATA
Katibu Msaidizi Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
Aprili-Julai 1964



BW. BERNARD MULOKOZI
Katibu Msaidizi Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
(1964-1972)



BW. ERNEST A. MULOKOZI
Katibu Msaidizi Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu
(1972-1973)



# Mheshimiwa Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi

## Wasifu

Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi alishika wadhifa wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia tarehe 11 Aprili, 1972 hadi tarehe 29 Januari, 1984 alipojiuzulu.

Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi alizaliwa tarehe 14 Juni, 1920 Kijiji cha Fuoni, Wilaya ya Magharibi, Unguja Zanzibar. Alilelewa katika Mtaa wa Mkamasini, Unguja. Mheshimiwa Jumbe alikuwa mtoto wa tatu wa familia ya Bwana Jumbe Mwinyi Othman na Bibi Toufah Mustafa Mussa. Familia yake ilikuwa ni ya wakulima.

Mwaka 1930 hadi 1937 alipata elimu ya msingi na ya kati katika Skuli ya Wavulana Mnazi Mmoja, Unguja. Mwaka 1938 hadi 1942 alipata elimu ya sekondari katika Skuli ya Sekondari ya Wavulana ya Mnazi Mmoja, na mwaka 1943 hadi 1945 alijiunga na Chuo Kikuu Kishiriki cha Makerere, Uganda kwa Masomo ya Stashahada ya Ualimu ambapo alisoma na watu mashuhuri akiwemo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Alikuwa mwandishi wa vitabu na maandiko mbalimbali ambapo aliandika jumla ya vitabu 35 vya siasa na dini.

## Ajira na Uongozi

Mheshimiwa Jumbe aliajiriwa kazi ya ualimu katika Skuli ya Sekondari ya Serikali ya Wavulana ya Mnazi Mmoja, kwa sasa Sekondari ya Benbella, tarehe 1 Januari, 1949. Mwaka 1953 hadi 1958, alikuwa Mwalimu Mkuu katika Shule ya King George VI ambayo kwa sasa inajulikana kwa jina la Lumumba High School iliyopo Unguja–Zanzibar. Kwa mujibu wa Sheria ya kikoloni ya Utumishi iliyokataza mtumishi wa umma kujihusisha na masuala ya siasa, tarehe 16 Novemba, 1960 Mheshimiwa Jumbe aliandika rasmi barua ya kuacha kazi ya ualimu na kujiunga na ASP. Katika uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 17 Januari, 1961 Mhe. Jumbe aligombea Jimbo la Fuoni na kushinda nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Kutunga Sheria. Vilevile, aliteuliwa kuwa Mnadhimu wa Upinzani katika Baraza hilo na pia alikuwa Katibu wa Mipango wa ASP, nafasi aliyodumu nayo hadi mwaka 1964.

Mwezi Januari hadi Aprili, 1964 kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na baada ya Mapinduzi, Mheshimiwa Aboud Jumbe aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Waziri wa Ndani wa Zanzibar na baadaye Waziri wa Afya na Ujenzi, nafasi alizohudumu katika kipindi kifupi sana cha miezi minne. Tarehe 27 Aprili, 1964 aliteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuwa Mjumbe wa Taifa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Tarehe 11 Aprili, 1972, kufuatia kuuawa kwa Sheikh Karume, aliteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wadhifa ambao alihudumu hadi tarehe 29 Januari, 1984. Aidha, kufuatia kuunganishwa kwa vyama vya ASP na TANU tarehe 5 Februari, 1977 na kuundwa kwa chama kipya cha siasa–Chama cha Mapinduzi (CCM), Mheshimiwa Aboud Jumbe alichaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya CCM kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho.



▲

*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), akimuapisha Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Dar es Salaam, tarehe 11 Aprili, 1972.*

# Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (1972–1984)

Chini ya uongozi wa Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1964–1985)

Matangazo ya Serikali Na. 235 la tarehe 28 Aprili, 1964 na Na. 16 la tarehe 6 Februari, 1981 kama yanavyosomeka katika aya ya 1.2 (a) na (e) katika Kitabu hiki.



*Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (aliyevaa suti), akimpokea Mhe. Seretse Khama, Rais wa Botswana alipowasili Zanzibar kwa ziara rasmi ya kiserikali. Kulia kwa Mhe. Jumbe ni Brigedia Jenerali Yusuf Himid, mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na anayefuatia ni Edington Kisasi, Kamishna wa polisi na mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, tarehe 6 Septemba, 1973.*




*Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipowasili Beijing-China kwa ajili ya ziara ya kikazi tarehe 11 Desemba, 1976.*



*Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), akimkaribisha Mhe. Samora Machel, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Ikulu-Zanzibar, alipofanya ziara ya kikazi mwaka 1978.*

▼





◄

*Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia), akiwa na Mhe. Michael Somare, Waziri Mkuu wa Papua New Guinea, akitia saini kitabu cha wageni mara tu alipowasili Uwanja wa Ndege wa Zanzibar, tarehe 8 Desemba, 1979.*

# Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (1972–1984)

Katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, masuala mbalimbali yalijitokeza: kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 kulikosababisha Serikali kubeba majukumu yaliyokuwa yanasimamiwa na Jumuiya hiyo; Kuyumba kwa hali ya Uchumi wa Nchi kutokana na athari zilizosababishwa na vita dhidi ya Iddi Amin wa Uganda vya mwaka 1978 hadi 1979 na Kuyumba kwa Uchumi wa Dunia miaka ya 1980 ambapo kulichangia kushuka kwa thamani ya sarafu ya fedha ya Tanzania.

Kutokana na masuala hayo, OMR ilitekeleza shughuli kuu zifuatazo:

- Kusimamia utungwaji wa Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na mambo mengine inayofafanua majukumu ya mihimili mitatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Kusimamia mabadiliko ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yaliyofanyika mwaka 1979 ili kuanzisha Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara baada ya kuvunjika kwa Mahakama ya Rufani ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1978.




▲ *Nakala ya Katiba ya Kwanza ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyotungwa mwaka 1979.*


NDUZI

- Kuanzisha na kusimamia maandalizi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambapo mchakato wake ulianza mwaka 1979 kwa lengo la kukidhi mahitaji ya Kimuungano, ukijumuisha mambo ya msingi ya Haki za Binadamu, Utawala Bora, mgawanyo wa madaraka katika Mihimili Mitatu ya Dola na Uhuru wa kutoa maoni.
- Kusimamia kuundwa kwa Baraza la Wawakilishi Zanzibar mwaka 1980 na kuwa chombo muhimu cha kusikiliza, kuwasilisha maoni ya wananchi na kutenganisha majukumu ya Baraza la Mapinduzi.
- Kufanya ufuatiliaji kwa kutembelea Mikoa yote ya Tanzania Bara na kutangaza fursa na faida za Muungano na wajibu wa Watanzania wote kuulinda na hivyo kuimarisha udugu kati ya pande mbili za Muungano.
- Kusimamia sehemu ya maamuzi ya kuruhusu baadhi ya mambo kushughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano hivyo kupelekea kuongezeka kwa mambo sita ya Muungano kutoka mambo 15 mpaka mambo 21: Baraza la mitihani la Taifa (jambo la 16); usafiri na Usafirishaji wa Anga (jambo la 17) Utafiti (Jambo la 18); Utabiri wa Hali ya Hewa (Jambo la 19); na Takwimu (jambo la 20). Aidha, kufuatia kuvunjika kwa Mahakama ya Rufani ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1978, Jambo la 21 liliongezwa ambalo ni Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (1978–1986). Malengo ya Mpango huo yalikuwa ni kuimarisha uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maendeleo endelevu. Mpango huo unaendana na Mipango ya maendeleo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Kusimamia Mabadiliko ya Sera ya Elimu kwa kuruhusu Wazanzibar kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu Tanzania Bara.
- Kuimarisha huduma ya usafiri wa watu na bidhaa kwa ununuzi wa Meli ya Mafuta ya MT. UKOMBOZI na MV. MAENDELEO iliyotumika kutoa huduma ya usafiri wa watu na bidhaa kwa pande mbili za Muungano, mwaka 1980. Meli hiyo ilisafiri kati ya Mtwara, Dar es Salaam, Unguja na Pemba. Wakati huo usafiri haukuwa wa uhakika.

# Anavyokumbukwa

Mheshimiwa Aboud Jumbe anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Alikuwa ni kiongozi wa kwanza wa kitaifa kutoka Zanzibar aliyetembelea mikoa yote ya Tanzania Bara na kutangaza fursa na faida za Muungano na wajibu wa Watanzania wote kuulinda na hivyo kuimarisha udugu kati ya pande mbili za Muungano.
- Alikuwa ni miongoni mwa Viongozi Wakuu walioshiriki mchakato wa kuunganisha vyama vya TANU na ASP na Kuunda Chama cha Mapinduzi (CCM) tarehe 5 Februari, 1977. Kuunganishwa kwa vyama hivyo kuliimarisha zaidi Muungano na kuchochea ari na nguvu mpya katika kuendesha shughuli za kisiasa kwa Tanzania Bara na Zanzibar, na hivyo kuendelea kuimarika kwa amani, utulivu, usalama, umoja na mshikamano wa kitaifa.
- Alipunguza vizuizi vya usafirishaji kwa kuruhusu watu kusafiri nje na ndani ya nchi kirahisi.
- Alikuwa kiongozi wa kwanza nchini Tanzania kujiuzulu katika wadhifa wa Makamu Kwanza wa Rais na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 29 Januari, 1984.
- Alisimamia ujenzi wa nyumba za Vijiji Unguja na Pemba.




▲

*Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati, aliyeweka mikono mifukoni), akizungumza na wafanyakazi na wananchi wa Lukongo, mkoa wa Pwani mara baada ya kufungua Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, tarehe 5 Juni, 1975.*




# Mauti

Mheshimiwa Aboud Jumbe alifariki dunia Jumamosi tarehe 14 Agosti, 2016 Jijini Dar es Salaam akiwa na umri wa miaka 96. Alizikwa Jumapili tarehe 15 Agosti 2016 nyumbani kwake katika Shehia ya Migombani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.



◄

*Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto kwa muuguzi), akikagua Hospitali ya Mzenga, Mkoa wa Pwani, tarehe 4 Juni, 1975.*

# Viongozi waliohudumu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1972 hadi 1984



MHE. ABOUD JUMBE MWINYI
Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
(1972–1984)



MHE. HASSAN N. MOYO
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(1972–1978)



MHE. ALI M. ALI
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(1978–1979)



MHE. ABOUD T. ABOUD
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(1979-1984)



MHE. ALI HASSAN MWINYI
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(1983-1984)



BW. MOHAMMED F. MOHAMMED
Katibu Msaidizi Mkuu Mwandamizi
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(Muungano)
(1972-1976)



BW. ISSA M. ISSA
Katibu Msaidizi Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(1979-1983)



BW. ZAIDU J. USSI
Katibu Msaidizi Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(Mambo ya Nje na Jamii)
(1973-1979)



BW. MOHAMMED AHMED
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(1983-January 1984)



# Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi

## Wasifu

Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 30 Januari, 1984 hadi Oktoba 1985, katika kipindi cha uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alizaliwa tarehe 8 Mei, 1925 katika Kijiji cha Kivule, Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani, Tanzania Bara. Alikuwa mtoto wa mwisho kati ya watoto watano waliozaliwa katika familia ya Bwana Hassan Mwinyi na Bibi Asha Mwinyi. Aidha, wakati Mzee Ali Hassan Mwinyi akiwa na umri mdogo, familia yake ilihamia Zanzibar.

Mwaka 1933 hadi 1936, alipata elimu ya msingi hadi Darasa la Nne, katika Skuli ya Msingi Mangapwani, Unguja. Aliendelea na elimu ya kati katika Skuli ya Dole kuanzia mwaka 1937 hadi 1940. Mwaka 1941 alisoma darasa la tisa katika Skuli ya Sekondari ya Dole[7] na mwaka 1942 alijiunga na masomo ya darasa la kumi kupitia Rapid Results College ya Uingereza kwa njia ya posta. Mwaka 1943 hadi 1944 alisomea ualimu katika Chuo cha Ualimu Dole, Zanzibar. Mwaka 1945 hadi 1946, Mheshimiwa Mwinyi alikuwa mwalimu katika Skuli ya Msingi Mangapwani, Unguja. Aidha, mwaka 1947 alikuwa mwalimu katika Shule ya Bumbwini. Pia, alijiendeleza kielimu kwa njia ya posta na kutunukiwa Cheti cha Ualimu (General Certificate in Education–GCE).

Mwaka 1961 hadi 1962, alisoma katika Chuo cha Durham University–Institute of Education, Uingereza katika mafunzo ya ualimu kwa vitendo (Tutors' Attachment Course) na kutunukiwa Stashahada ya Ualimu. Baadaye alijiendeleza tena kwa njia ya posta katika Taasisi ya Regent (Regent Institute) iliyopo London,

7. Kabla Mheshimiwa Mwinyi hajaanza Darasa la Kumi, aliyekuwa Mkurugenzi wa Elimu Zanzibar, Bwana R. S. Forster alisitisha masomo hayo ili afanye mageuzi makubwa katika mfumo wa elimu. (Mwinyi, A. H. MZEE RUKHSA: SAFARI YA MAISHA YANGU. Mkuki na Nyota, Dar es Salaam, 2020. uk. 70).

Uingereza na kutunukiwa cheti cha ufundishaji wa lugha ya Kiingereza. Mwaka 1972 hadi 1974 alisoma na kutunukiwa cheti cha lugha ya Kiarabu kutoka Cairo nchini Misri.

Ni kiongozi aliyeshika wadhifa wa Urais wa pande zote mbili za Muungano kwa nyakati tofauti, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1984–1985) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985–1995).

## Ajira na Uongozi

Mwaka 1945 hadi 1950, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alikuwa mwalimu katika Skuli ya Mangapwani na kuwa Mwalimu Mkuu katika Skuli hiyo hiyo kati ya mwaka 1950 hadi 1954. Mwaka 1956 hadi 1961 alijiunga na Chuo cha Ualimu cha Beit el Ras, Zanzibar akiwa Mkufunzi. Mwaka 1962 alipandishwa cheo na kuwa Mkuu wa Chuo cha Ualimu cha Beit el Ras. Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alijiunga kwa njia ya siri na Afro–Shirazi Party (ASP) tangu kilipoasisiwa mwaka 1957 (kwa kuwa chini ya utawala wa kikoloni, watumishi wa umma waliharamishwa kujiunga na ASP), ambapo mwaka 1964 alidhihirisha uanachama wake wa ASP.

Mwaka 1964 hadi 1965, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alikuwa Katibu Mkuu katika Wizara ya Elimu Zanzibar, Mwenyekiti wa Bodi ya Sensa Zanzibar, Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania.

Mwaka 1965 hadi 1970, Mheshimiwa Mwinyi aliteuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (Zanzibar State Trading Corporation–ZSTC) huku akihudumu katika nafasi ya Mweka Hazina Msaidizi katika Tawi la ASP la Makadara, Zanzibar. Pia, mwaka 1972 hadi 1975 alikuwa Waziri wa Afya wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) kuanzia mwaka 1974 hadi 1977.

Alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuanzia mwaka 1975 hadi 1977. Mheshimiwa Mwinyi aliwajibika kwa kujiuzulu wadhifa wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mwaka 1977 kufuatia vifo vilivyotokea Mikoani Mwanza na Shinyanga vya mahabusu kwenye vituo vya polisi. Mwaka huo huo aliteuliwa kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Misri na kutumikia nafasi hiyo hadi mwaka 1982 aliporejea nyumbani na kuteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Mwaka 1983 aliteuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Aidha, katika kipindi chote cha uwaziri, wakati wa mfumo wa chama kimoja, alikuwa mbunge wa kuteuliwa.

Kufuatia kujiuzulu kwa Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi tarehe 29 Januari, 1984 Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi aliteuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM na kuapishwa kuwa Kaimu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania tarehe 30 Januari, 1984. Aidha, baada ya Uchaguzi Mdogo wa Rais Zanzibar uliofanyika tarehe 19 Aprili, 1984 Mhe. Ali Hassan Mwinyi alichaguliwa na kuapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 24 Aprili, 1984. Mheshimiwa Mwinyi alitumikia wadhifa huo kuanzia Januari, 1984 hadi Oktoba, 1985 kabla ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 27 Oktoba, 1985 hadi 23 Novemba, 1995.



▲

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, akiapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anayemuapisha ni Augustino Ramadhani, Jaji Mkuu wa Zanzibar, tarehe 30 Aprili, 1984.*

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (1984–1985)

Chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1964–1985)

Tangazo la Serikali Na. 16 la tarehe 6 Februari, 1981 kama linavyosomeka katika aya ya 1.2 (e) katika Kitabu hiki.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (1984–1985)

Katika kipindi cha Uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Makamu wa Kwanza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, masuala mbalimbali yalijitokeza: uwepo wa mjadala kuhusu muundo wa Muungano; kuvunjika kwa mahakama ya rufaa ya Afrika Mashariki; kudorora kwa uchumi; upungufu wa bidhaa; upungufu wa chakula; kutetereka kwa masoko ya kimataifa ya mazao ya biashara kama karafuu na pamba; kufungwa kwa viwanda kutokana na ukosefu wa malighafi na vipuri; na utekelezaji hafifu wa mashirika ya umma hivyo kupunguza mapato ya Serikali na fedha za kigeni.

Kutokana na masuala yaliyoainishwa hapo juu, OMR imetekeleza yafuatayo:

- Kusimamia Mabadiliko ya Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ili kukidhi mahitaji ya Muungano mwaka 1984, mfano Katiba iliingiza Tamko la kimataifa la haki za binadamu ili kupanua uhuru na haki za msingi za raia.
- Kusimamia uingizwaji wa suala la Mahakama ya Rufaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.
- Kulegeza masharti kwa kuruhusu wafanyabiashara binafsi wenye akiba za fedha za kigeni kuingiza bidhaa muhimu Zanzibar, ambazo Serikali haikuwa na uwezo wa kutosheleza mahitaji ya wananchi. Hatua hiyo, iliwezesha bidhaa kuingia Zanzibar kwa wingi kutoka nchi za kiarabu na kwingineko na wafanyabiashara wa Tanzania Bara kwenda Zanzibar na vilevile baadhi ya wafanyabiashara kutoka Pemba walihamia Tanzania Bara. Hivyo, safari za meli zikaongezeka baina ya pande mbili za Muungano. Hali hiyo ilipelekea kuboresha hali ya kiuchumi kwa wananchi.

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akikagua mradi wa kilimo cha muhogo, katika Mkoa wa Kusini Unguja, mwaka 1984.*



- Kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ziara ya kikazi nchini Bulgaria kwa lengo la kufanya makubaliano ya ujenzi wa kiwanda cha kubuni na kutengeneza mashine mbalimbali (Kilimanjaro mashine Tools manufacturing Company–LTD ) tarehe 7–14 Septemba, 1984 na baadaye kiwanda hicho kilijengwa Moshi–Kilimanjaro.
- Kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majadiliano na makubaliano kuhusu kuanzisha upya maeneo ya ushirikiano kati ya nchi tatu Kenya, Tanzania na Uganda. Makubaliano hayo yaliwezesha kufunguliwa kwa mipaka ya Kenya na baadaye Uganda iliyopelekea kuanzisha safari za Treni kati ya Tanzania na Kenya. Aidha, Safari hizo zilizinduliwa tarehe 15 Februari, 1985.
- Kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ziara nchini China na Korea Kaskazini kwa lengo la kuwekeza kwenye viwanda, redio na kilimo nchini, tarehe 7–23 Aprili, 1985. Ziara hiyo ilipelekea kufufua uzalishaji katika kiwanda cha nguo cha Urafiki (Tanzania and China Textile Company), Tanzania Bara na kiwanda cha sukari Mahonda, Zanzibar, kiwanda cha vifaa vya kilimo na kufanya matengenezo ya minara ya matangazo ya redio kilichopo Dole, Zanzibar.

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa tano kushoto mstari wa mbele) na Ujumbe wake akiwa katika picha ya pamoja na Rais wa Korea Kaskazini Mhe. Kim II-Sung na Ujumbe wake, alipotembelea nchi hiyo mwezi Aprili, 1985.*







Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Ali Hassan Mwinyi, akisaini kitabu cha wageni baada ya kukagua mradi wa kilimo katika Afisi Kuu ya CCM Zanzibar, mwaka 1984.



## Anavyokumbukwa

Katika kipindi cha uongozi wake, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Ni kiongozi aliyewahi kushika wadhifa wa Urais wa pande zote mbili za Muungano kwa nyakati tofauti: Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1984–1985); na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985–1995).
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyehudumu kwa kipindi cha miezi 21 katika historia ya Tanzania.
- Alihimiza umoja na utaifa wa Watanzania wote hasa baada ya machafuko ya hali ya kisiasa Zanzibar, mara tu baada ya Mhe. Aboud Jumbe kujiuzulu.
- Ni kiongozi pekee aliyeteuliwa kukaimu wadhifa wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda wa miezi minne kwa mujibu wa Ibara ya 8 (b) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979.
- Ni kiongozi aliyeshirikisha wananchi wakati wa kuandaa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kwa kuchukua maoni yao.

## Mauti

Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alifariki Alhamis tarehe 29 Februari, 2024 Jijini Dar es Salaam, akiwa na umri wa miaka 99. Alizikwa Jumamosi tarehe 2 Machi, 2024 katika Kijiji cha Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar.



▲

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akifanya mazungumzo na Kiongozi Mkuu wa China, Mhe. Deng Xiaoping wakati wa ziara ya kikazi nchini China, Aprili, 1985.*





Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akitumbukiza kura yake kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 1984.

▼




## Viongozi Waliohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1984 hadi 1985



MHE. ALI HASSAN MWINYI
Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
(1984–1985)



MHE. RAMADHAN A. SHAABAN
Waziri wa Nchi
Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(1984–1985)



BW. MOHAMMED A. MOHAMMED
Katibu Mkuu
Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
(1984–1985)



# Mheshimiwa Sheikh Idris Abdulwakil

## Wasifu

Sheikh Idris Abdulwakil alikuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia tarehe 17 Oktoba, 1985 hadi 25 Oktoba, 1990 kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sheikh Idris Abdulwakil alizaliwa tarehe 10 Aprili, 1925 katika Kijiji cha Kiongoni Makunduchi katika Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar. Alikuwa mtoto wa kwanza kati ya watoto kumi wa Mzee Abdulwakil Nombe Pandu na Bibi Asha Ameir Makame.

Sheikh Idris Abdulwakil alipata elimu yake ya msingi kuanzia mwaka 1936 hadi 1939 katika Skuli ya Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar. Mwaka 1940 hadi 1943, alijiunga na Skuli ya Dole–Unguja na kusoma darasa la tano hadi la nane. Mwaka 1944 hadi 1948 alipata elimu ya sekondari katika Skuli ya Sekondari ya Serikali ya Wavulana ya Mnazi Mmoja–Unguja, kwa sasa inaitwa Skuli ya Sekondari ya Benbella na kutunukiwa Cheti cha Daraja la Pili (School Certificate Grade II). Mwaka 1949 hadi 1951 alikwenda nchini Uganda katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Makerere na kupata mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti, Daraja la Pili, Kundi la Pili (Teachers' Certificate Grade II Group II). Aidha, mwaka 1954, alipata mafunzo ya Stashahada ya Ualimu katika Chuo Kikuu hicho.

## Ajira na Uongozi

Mnamo tarehe 1 Novemba, 1952, Sheikh Idris Abdulwakil aliajiriwa kuwa Mwalimu katika Skuli ya Makunduchi Unguja–Zanzibar, akifundisha somo la Kiingereza. Mwaka 1954, alipandishwa cheo kuwa Mwalimu Daraja la Tatu na aliteuliwa kuwa Mwalimu Mkuu wa Skuli ya Makunduchi. Mwaka 1958 aliajiriwa kuwa Mkufunzi wa Chuo cha Ualimu cha Beit el Ras, Zanzibar. Mwaka 1960, alitunukiwa Tuzo Maalumu ya Mwalimu Bora (American Award for Colonial Teachers) alichokabidhiwa na Mwakilishi Mkaazi wa Uingereza, Sir John Rankine, kwa niaba ya Waziri wa Makoloni ya Uingereza.

Sheikh Idris Abdulwakil alijiuzulu kazi ya Ualimu mwezi Novemba, 1962 na kujiunga rasmi na siasa. Mwaka 1962 aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria wa Jimbo la Mangapwani kufuatia kifo cha Bwana Mohamed Iddi Bavuai aliyekuwa mjumbe wa Jimbo hilo. Julai, 1963 alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria wa Jimbo la Makunduchi kupitia Afro–Shirazi Party (ASP) hadi Januari, 1964 kulipotokea Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Tarehe 12 Januari, 1964, Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar alimteua Sheikh Idris Abdulwakil kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Waziri wa Elimu, Utalii na Utamaduni, nafasi aliyohudumu hadi tarehe 27 Aprili, 1964. Sheikh Idris Abdulwakil aliteuliwa na Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuwa Mbunge na Waziri wa Habari na Utalii, katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, nafasi aliyohudumu hadi tarehe 7 Julai, 1967.

Tarehe 7 Julai 1967, Mwalimu Nyerere alimteua Mheshimiwa Sheikh Idris Abdulwakil, kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ujerumani Magharibi, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 1968. Aidha, mwaka 1969 hadi 1973, Mheshimiwa Sheikh Idris Abdulwakil alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Uholanzi, na mwaka 1973 hadi 1977 alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Guinea. Vilevile, Mheshimiwa Sheikh Abdulwakil alikuwa Mkuu wa Itifaki katika Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 hadi 1979. Hivyo, alikuwa mwanadiplomasia kwa miaka kumi na mbili (12).

Mwaka 1980, Sheikh Abdulwakil alichaguliwa kuwa Spika wa Kwanza wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 1985, Vilevile, mwaka 1984 aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na Mkuu wa Vikosi vya SMZ na Idara ya Usalama.

Tarehe 13 Oktoba, 1985 Sheikh Idris Abdulwakil alichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi baada ya Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa akishika nafasi hiyo, kuteuliwa kugombea nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheikh Idris Abdulwakil alihudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi kimoja cha miaka mitano hadi mwaka 1990.



▲

*Mhe. Sheikh Idris Abdulwakil, akiapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Anayemuapisha ni Mhe. Augustino Ramadhan, Jaji Mkuu wa Zanzibar, mwaka 1985.*



*Mhe. Sheikh Idris Abdulwakil, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa pili kulia), akiwa na Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mara baada ya kilele cha Maadhimisho ya Miaka 22 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Ukumbi wa Lumumba. Wengine katika picha ni Mhe. Seif Shariff Hamad, Waziri Kiongozi wa SMZ (kulia kwa Mhe. Abdulwakil) na Mhe. Ramadhan Abdallah Shaaban, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa pili kulia kwa Mhe. Abdulwakil), tarehe 12 Januari, 1986.*

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1985–1990)

### Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985–1995)

Matangazo ya Serikali Na. 16 la tarehe 6 Februari, 1981 na Tangazo la Serikali Na. 205 la tarehe 15 Aprili, ya 1987 kama ilivyoelezwa katika aya 1.2 (e) na (f) katika Kitabu hiki.



◀

*Mhe. Sheikh Idris Abdulwakil, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akizungumza na Mhe. Hardev Bhalla, Balozi wa India nchini Tanzania, Ikulu ya Zanzibar, Oktoba, 1986.*



▼

*Mhe. Sheikh Idris Abdulwakil, Makamu wa Pili wa Rais na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akisalimiana na Mhe. Joachim Chissano, Rais wa Msumbiji, alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar tarehe 11 Desemba, 1986 kwa ziara ya kwanza ya kikazi nchini. Wengine katika picha ni Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), Mhe. Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati) na Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa, Katibu Mkuu wa CCM (kulia).*

# Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Makamu wa Rais 1985–1990)

Katika kipindi cha Mheshimiwa Sheikh Idris Abdulwakil, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, masuala kadhaa yalijitokeza yakiwamo ushirikishwaji mdogo wa sekta binafsi katika uchumi wa Taifa na uhaba wa chakula.

Kutokana na masuala hayo, OMR imetekeleza yafuatayo:

- Kuanzisha Idara ya Uwekezaji katika Wizara ya Fedha Zanzibar (1986) ikiwa na majukumu ya kusimamia na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi. Katika kipindi hicho, sekta ya utalii ilipewa kipaumbele kuchangia ukuaji wa uchumi wa Zanzibar. Mwaka 1992, Idara hiyo ilipandishwa hadhi kuwa Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA).
- Kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Kilimo cha MTAKULA (Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula, 1985–1990) ambayo ilihusisha mashindano ya bidhaa zenye ubora za kilimo ki–mikoa na kuwawezesha wananchi kujishughulisha na kilimo.

## Anavyokumbukwa

Mheshimiwa Idris Abdulwakil hakugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar kwa kipindi cha pili, licha ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kuruhusu Mgombea wa Urais wa Zanzibar kugombea vipindi viwili mfululizo.

## Mauti

Sheikh Idris Abdulwakil alifariki dunia Jumatano ya tarehe 15 Machi, 2000 akiwa na umri wa miaka 75 katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Zanzibar. Alizikwa Alhamisi ya tarehe 16 Machi, 2000 katika Kijiji cha Kiongoni, Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar.



◀ *Mhe. Sheikh Idriss Abdulwakil, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akisalimiana na Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Zanzibar, Ikulu ya Kibweni, Zanzibar tarehe 17 Oktoba, 1985.*

## Viongozi waliohudumu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1985 hadi 1990



MHE. SHEIKH IDRIS ABDULWAKIL
Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
(1985-1990)



MHE. ALI S. AHMED
Waziri wa Nchi
Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Mipango)
(1985-1988)



MHE. MUHAMMED S. KHATIB
Waziri wa Nchi
Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Muungano)
(1988-1990)



MHE. TAYMOUR S. JUMA
Waziri wa Nchi
Afisi ya Rais (Fedha)
(1989-1990)



BW. MOHAMMED A. MOHAMMED
Katibu Mkuu
Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais
(1985-1990)



# Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba

## Wasifu

Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuanzia tarehe 5 Novemba, 1985 hadi tarehe 9 Novemba, 1990 katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Jaji Warioba alizaliwa tarehe 3 Septemba, 1940 katika Kijiji cha Ikizu katika Wilaya ya Musoma, Mkoani Mara. Alikuwa mtoto wa tatu kati ya watoto saba wa Bwana Warioba Sinde na Bibi Wasato Keremba. Mwaka 1948, alipata elimu ya awali katika Shule ya Awali ya Sarawe, Wilaya ya Musoma. Mwaka 1949 hadi 1952, alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Ikizu iliyoko Wilaya ya Musoma. Mwaka 1953 hadi 1954 alipata elimu ya kati katika Shule ya Kati ya Mwisenge huko Musoma, kabla ya kujiunga na Shule ya Sekondari Bwiru, Jijini Mwanza mwaka 1955 hadi 1960. Alijiunga na Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Tabora mwaka 1961 hadi 1962 alipohitimu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambako alihitimu Shahada ya Sheria mwaka 1966. Aidha, Mheshimiwa Jaji Warioba alipata Astashahada ya Juu (Postgraduate Certificate) katika Fani ya Sheria, Chuo Kikuu cha Sheria za Kimataifa cha The Hague, Uholanzi, mwaka 1970.

Mheshimiwa Jaji Warioba ni Mwanasheria mbobezi, Mwanasiasa na Jaji mashuhuri anayeheshimika Kitaifa na Kimataifa kwa mchango wake mkubwa katika masuala ya Sheria na Utawala Bora.

## Ajira na Uongozi

Mheshimiwa Jaji Warioba aliajiriwa kuwa Mwanasheria wa Serikali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuanzia mwaka 1966 hadi 1968. Alikuwa Mwanasheria wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuanzia mwaka 1968 hadi 1970. Mwaka 1971 hadi 1975 alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Sheria na Taasisi za Kimataifa (Legal and International Organisations Division) katika Wizara ya Mambo ya Nje. Mwaka 1975 hadi 1976 alihudumu wadhifa wa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwishoni mwa

mwaka 1976 aliteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mwaka 1983 akiwa katika wadhifa huo, aliteuliwa kuwa Waziri wa Sheria na mmoja wa wasuluhishi katika mgogoro wa kimataifa wa kugombea mipaka chini ya bahari baina ya nchi za Ufaransa, Japan na iliyokuwa Jamhuri ya Kisoshalisti ya Urusi. Alihudumu katika nafasi ya Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Sheria hadi mwaka 1985 na kuhitimisha kazi ya usuluhishi wa mipaka chini ya bahari mwaka 1986.

Mwaka 1985 aliteuliwa kuwa Mbunge, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wadhifa huo aliutumikia hadi mwaka 1990.



▲

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), akimuapisha Mhe. Joseph Sinde Warioba, kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Dar es Salaam. Katikati ni Balozi Paul Rupia, Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 5 Novemba, 1985.*

# Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (1985–1990)

## Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985–1995)

Tangazo la Serikali Na. 205 la tarehe 17 Aprili, 1987 kama linavyosomeka katika aya ya 1.2 (f) katika Kitabu hiki. Kupitia Tangazo hili la Serikali mabadiliko mengine makubwa katika muundo na majukumu ya OMR yalifanyika chini ya uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*Mhe. Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akimwakilisha Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukabidhi Hati ya Nishani ya Kimataifa ya uongozi, kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Mhe. Nelson Mandela, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini, wakati wa ziara yake nchini Tanzania, tarehe 7 Machi, 1990.*

▼



kufuatia uteuzi wa Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba tarehe 5 Novemba, 1985 kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uteuzi huo ulimrejeshea Waziri Mkuu kofia ya Makamu wa Rais. Hivyo, Mheshimiwa Warioba akawa kiongozi wa kwanza kutoka Tanzania Bara kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (1985–1990)

Katika kipindi cha Uongozi wa Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, masuala mbalimbali yalijitokeza: kuendelea kwa athari za mdororo wa kiuchumi ulioathiriwa na vita vya Iddi Amin wa Uganda; ukame ulioanza nchini tangu mwaka 1981 ambao ulipelekea hali ya uzalishaji na usalama wa chakula kuwa duni; kudorora kwa uhusiano wa kisiasa na kiuchumi baina ya Tanzania na Kenya; kuenea kwa kasi ya ugonjwa wa UKIMWI ulioanza kuingia nchini Novemba, 1983 ambao ulisambaa katika mikoa yote ya Tanzania mwaka 1986 na kuhatarisha nguvu–kazi ya Taifa; utendaji wa mashirika ya Umma ambao haukuwa wa kuridhisha na hivyo kusababisha hasara kwa Serikali; na ukuaji mdogo wa pato la Taifa wa wastani wa asilimia 2 tu kwa kipindi cha mwaka 1980 hadi 1985.

Kutokana na masuala hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais ilitekeleza yafuatayo:

- Kusimamia ubinafsishaji wa mashirika ya Umma yasiyo na tija na kuruhusu uwepo wa soko huria, ambapo Serikali mwaka 1986 ilitunga sheria mbalimbali kwa ajili ya kukuza na kudhibiti ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi wa Taifa, kwa mfano sheria ya BRELA ya mwaka 1986 na Sheria ya Umiliki (Patent Act) ya mwaka 1987.
- Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ushirika ya Uzalishaji Mali Vijijini ya mwaka 1985. Sera hiyo ilikuwa na lengo la kufufua ari ya ujenzi wa ujamaa vijijini kwa pande mbili za Muungano, ambapo ilipendekezwa kila kijiji kiwe na kikundi cha uzalishaji mali.
- Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mipango ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI, ikihusisha ya muda mfupi (1985–1986) na muda wa kati (1987–1991). Hili lilifanywa kwa utoaji wa elimu na kuhusisha Mikoa na Sekta mbalimbali na jumuiya zake.
- Kusimamia ukuaji wa uchumi ambapo kiwango kiliongezeka kutoka wastani wa asilimia 2 mwaka 1986 na kufikia wastani wa asilimia 4 kwa mwaka 1990.

## Anavyokumbukwa

Mheshimiwa Warioba anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Kiongozi wa kwanza kutoka Tanzania Bara kushika wadhifa wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Kiongozi wa kitaifa aliyeendeleza utamaduni aliouanzisha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, wa kufanya midahalo mara kwa mara na Wanafunzi, Wahadhiri na Maprofesa wa Vyuo Vikuu, hususan chuo kikongwe nchini, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuhusu masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, yaliyokuwa yakijitokeza bayana na Umma kudai majibu/maelezo maridhawa kutoka kwa viongozi wa kitaifa.
- Makamu wa Kwanza wa Rais aliyetumika kimataifa baada ya kumaliza muda wake wa Uongozi nchini. Amewahi kushika wadhifa wa Jaji wa Mahakama ya Kimataifa inayohusika na Sheria ya Bahari, iliyopo Hamburg, Ujerumani, na Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki.



▲

*Mhe. Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa pili kushoto) akizungumza na Mhe. Salim Ahmed Salim, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (katikati). Wa kwanza kushoto ni Mhe. Anne Semamba Makinda, Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Pius Chipanda Msekwa, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa kwanza wa Rais (wa kwanza kulia), na Mhe. Balozi Charles Kileo, Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa kwanza Rais, wakiwa Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam kumsindikiza Mhe. Warioba. Mhe. Warioba alikuwa anasafiri kwenda nchini Marekani kuhudhuria mkutano wa maandalizi ya Tume ya Kimataifa juu ya Rasilimali za Bahari tarehe 5 Mei, 1986.*

# Viongozi waliohudumu Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1985 hadi 1990



MHE. JUDGE JOSEPH SINDE WARIOBA
Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(1985-1990)



MHE. GERTRUDE I. MONGELLA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Masuala ya Wanawake)
(1985-1988)



MHE. ANNE S. MAKINDA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(Uratibu wa Shughuli za Serikali na Muungano)
(1985-1990)



MHE. ANNA M. ABDALLAH,
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(Uendelezaji na Ustawishaji Makao Makuu-DODOMA)
(1989-1990)



MHE. AMBASSADOR CHARLES KILEO
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(TAMISEMI)
(1985-1990)



BW. PIUS CHIPANDA MSEKWA
Katibu Mkuu
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais
(1985-1989)



BW. FADHIL D. MBAGA
Katibu Mkuu
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais
(1989-1990)



# Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma

Wasifu

Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma, alikuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia tarehe 25 Oktoba, 1990 hadi Oktoba, 1995 katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Dkt. Salmin alizaliwa tarehe 14 Aprili, 1942 katika Kitongoji cha Kidombo, Kijiji cha Mkwajuni, Wilaya ya Kaskazini "A", Mkoa wa Kaskazini Unguja. Alikuwa ni mtoto wa saba kati ya watoto wanane wa Mzee Amour Juma na Bi. Siza Haji Boji.

Alipata elimu ya msingi na ya kati katika Skuli ya Mkwajuni, Unguja mwaka 1950 hadi 1957 alipohitimu darasa la nane. Mwaka 1961 hadi 1964, alisoma elimu ya Sekondari katika Shule ya Wavulana ya Agakhan, Dar es Salaam, kwa sasa Tambaza. Mwaka 1986, alijiunga na kuhitimu mafunzo ya programu maalumu ya masomo ya Uchumi na Siasa katika Chuo Kikuu cha Karl Marx (kwa sasa Chuo Kikuu cha Leipzig), wakati huo Ujerumani Mashariki.

## Ajira na Uongozi

Mheshimiwa Dkt. Salmin alianza kazi rasmi katika Shirika la Biashara za Nje (BIZANJE) akiwa Afisa Biashara mwaka 1965. Mwaka 1970 hadi 1973, alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara ya SMZ, na wakati huo huo, alikuwa Katibu wa Halmashauri ya Bodi ya Biashara.

Mwaka 1972 Mheshimiwa Dkt. Salmin alikuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya ASP, Idara ya Mipango na Uchumi, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 1973 alipoteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha ya SMZ. Aidha, mwaka 1976 hadi 1977, aliteuliwa kuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi. Mwaka 1977 hadi 1982 aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Kwanza wa CCM (Zanzibar).

Mwaka 1982 hadi 1983 Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour alikuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM akihudumu katika Idara ya Mipango. Mwaka 1984 hadi 1985 Mheshimiwa Dkt. Salmin aliteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wa Serikali ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi tarehe 25 Oktoba, 1985 alipochaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Jimbo la Mkwajuni.

Mwaka 1985 hadi 1990, Dkt. Salmin aliteuliwa kuwa Waziri wa Biashara wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na vilevile alikuwa ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia nafasi tano maalumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

Tarehe 25 Oktoba 1990, Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour alichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na kwa nafasi yake hiyo alikuwa pia Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wadhifa aliohudumu hadi mwaka 1995 ambapo utaratibu wa kuwa na Makamu Wawili wa Rais ulikoma. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Salmin aliendelea na wadhifa wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hadi tarehe 8 Novemba, 2000 alipomaliza muda wake kikatiba.

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akimuapisha Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, Ikulu Dar es Salaam, tarehe 25 Oktoba, 1990.*

▼





▲

*Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar akipongezwa na baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, baada ya kuapishwa kushika wadhifa huo, katika Uwanja wa Amani, Zanzibar. Wa kwanza kulia ni Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 25 Oktoba, 1990.*

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1990–1995)

Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985–1995)

Tangazo la Serikali Na. 489 la tarehe 30 Novemba, 1990 kama linavyosomeka katika aya ya 1.2 (g) katika Kitabu hiki.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (1990–1995)

Mheshimiwa Dkt. Salmin alisimamia utekelezaji wa majukumu kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Wakati wa uongozi wake, masuala mbalimbali yalijitokeza: uchumi ulioathiriwa na mabadiliko ya sera za kiuchumi za dunia; mabadiliko ya kisiasa, demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi; uzalishaji hafifu wa mashirika ya umma na kupunguza uendeshaji wa shughuli za uwekezaji kutekelezwa na Serikali.

Kutokana na masuala hayo, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rai ilitekeleza yafuatayo:

- Kusimamia kutungwa kwa Sheria mbalimbali kwa lengo la kuimarisha uchumi na maendeleo kwa ujumla zikiwemo: Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991 iliyoruhusu ushindani katika shughuli za Kibenki; Sheria ya mwaka 1992 kuhusu fedha za kigeni iliyoruhusu uanzishwaji wa maduka binafsi ya fedha za kigeni, jambo ambalo kabla lilikuwa maalumu kwa Benki Kuu ya Tanzania. Lengo lilikuwa kuongeza ufanisi wa sekta ya fedha kwa pande zote za Muungano.
- Kusimamia mchakato wa kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini mwaka 1992, ambapo SJMT na SMZ, chini ya uongozi wa Mhe. Ali Hassan Mwinyi na Mhe. Dkt. Salmin Amour mtawalia, ziliridhia kutungwa kwa sheria moja ya usajili na uendeshaji wa vyama vya siasa, Sheria iliyoongeza Jambo la 22 katika orodha ya Mambo ya Muungano.
- Kuanzisha na kusimamia Taasisi muhimu za kiuchumi zikiwemo: Kamisheni ya Utalii Zanzibar (1992); na Bodi ya Ukusanyaji wa Mapato Zanzibar–ZRB (1999).
- Kusimamia kuanzishwa kwa Eneo Huru la Uwekezaji kwa Sheria ya Uwekezaji Na. 16 ya mwaka 1992 katika eneo la Fumba; viwanda vidogo vidogo Amani kwa upande wa Unguja; na Micheweni kwa upande wa Pemba.

- Kusimamia uimarishaji wa usafiri wa Bahari baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa kuruhusu sekta binafsi kuingiza vyombo vya kisasa vya usafirishaji.
- Kusimamia uimarishaji wa Kituo cha Televisheni Zanzibar (TVZ) kwa kukipatia vifaa vya kisasa na kuwaongezea ujuzi wafanyakazi ikiwa ni sehemu ya uboreshaji wa usambazaji wa habari kwa wananchi, mwaka 1994.



▲

*Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Omar Ali Juma (katikati), Waziri Kiongozi wa Zanzibar, na Sheikh Idris Abdulwakil (kulia), Rais mstaafu wa Zanzibar, wakibadilishana mawazo katika kilele cha maadhimisho ya miaka 29 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam, tarehe 26 Aprili, 1993.*

▶

*Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma, Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akizindua Mradi wa Maji Safi, Bumbwini, Mkoa wa Kaskazini, Unguja, Zanzibar. Nyuma yake, ni Mhe. Abdulla Rashid, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja, Zanzibar mwezi Januari, 1990.*



## Anavyokumbukwa

Mheshimiwa Dkt. Salmin anakumbukwa kwa mambo yafuatayo;

- Alishiriki uchaguzi wa kwanza katika mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1995 na kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Alianzisha Afisi ya Mufti Mkuu Zanzibar mwaka 1992. Mwaka 2001 ilianzishwa upya kwa sheria ya Mufti Na.9 ya mwaka 2001.
- Alianzisha Mahakama ya Ardhi ya Zanzibar kupitia Sheria Na. 7 ya mwaka 1994.
- Aliimarisha misingi ya uchumi endelevu inayozingatia uzalishaji wa ndani zaidi, badala ya kutegemea zao moja la karafuu na biashara ya uingizaji bidhaa.
- Aliimarisha mazingira ya biashara kwa sekta binafsi kwa kuruhusu maonesho ya biashara kwa Zanzibar.
- Alianzisha Kampeni ya ushindi wa timu ya Taifa ya mpira wa miguu ya Zanzibar katika mashindano ya Challenge kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati, kampeni hiyo iliitwa Saidia Zanzibar Ishinde (SAZI). Zanzibar ilichukua ubingwa katika mashindano hayo mwaka 1995.

## Viongozi waliohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Pili Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1990 hadi 1995



MHE. DKT. SALMIN AMOUR JUMA
Makamu wa Pili Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
(1990-1995)



MHE. TAYMOUR S. JUMA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Fedha)
(1990-1995)



BW. MOHAMMED A. MOHAMMED
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(1990-1995)



# Mheshimiwa John Samwel Malecela

## Wasifu

Mheshimiwa John Samwel Malecela, alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 9 Novemba, 1990 hadi 5 Desemba, 1994 katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Malecela alizaliwa tarehe 20 Aprili, 1934 katika Kijiji cha Mvumi Misheni, mkoani Dodoma. Alikuwa mtoto wa 12 kati ya watoto 13 waliozaliwa katika familia ya Bwana Chilasa Samwel Malecela na Bibi Esther Nyagalu. Mwaka 1941 hadi 1946, alipata elimu ya awali pamoja na elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Mvumi. Mwaka 1947 hadi mwaka 1952, alipata elimu ya sekondari hadi darasa la kumi katika Shule ya Sekondari ya Alliance (ambayo ilibadilishwa jina na kuitwa Mazengo Sekondari na sasa ni Chuo Kikuu cha St. John). Mwaka 1953 hadi 1954 alijiunga na St. Andrew's College (Shule ya Sekondari ya Minaki iliyopo Kisarawe) ambako alihitimu darasa la 12.

Mwaka 1955 alisomea Shahada ya Biashara kwenye Chuo Kikuu cha Bombay–India, ambako alihitimu mwaka 1959. Mwaka 1961 hadi 1962, alisoma na kuhitimu Stashahada ya Masuala ya Fedha na Utawala katika Chuo Kikuu cha Cambridge, Uingereza. Aidha, ana Shahada ya Uzamivu ya Heshima katika Masuala ya Jamii (Ph.D. Honoris Causa–Humanities), ambayo alipata kutoka Chuo Kikuu cha Hardin Simmons Abilene Texas, Marekani mwaka 1977.

## Ajira na Uongozi

Mwaka 1960 hadi 1961 Mhe. John Samwel Malecela alikuwa Afisa wa Wilaya ya Tukuyu (Rungwe), mkoani Mbeya, ambako kazi yake kubwa ilikuwa ni kuanzisha Mabaraza ya Serikali za Vijiji. Mwaka 1962 hadi 1963 alikuwa Afisa katika Ubalozi wa Tanganyika, New York, Marekani na aliporejea nchini, alipangiwa kuwa Afisa Utumishi wa Mkoa wa Mtwara. Mwaka 1963 hadi 1964, Mheshimiwa Malecela aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kanda ya Ziwa Mashariki (ikijumuisha mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Mara).



*Mhe. Balozi John Samwel Malecela, Mwakilishi wa kwanza wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa, akikabidhi Hati ya Utambulisho kwa Mheshimiwa U Thant, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, New York Marekani, tarehe 19 Novemba, 1964.*

Mwaka 1964 hadi 1968, aliteuliwa kuwa Balozi na Mwakilishi wa kwanza wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, New York, Marekani wakati Muungano unaanzishwa mwaka 1964. Aidha, akiwa Balozi wa Kudumu, alishiriki katika tukio muhimu la kuwasilisha taarifa rasmi ya kumjulisha Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bwana U Thant, kuhusu kuungana kwa Nchi za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na kuunda nchi moja iitwayo "Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar" tarehe 30 Aprili, 1964 na pia, alikuwa Balozi wa Kwanza wa Tanzania nchini Canada.

Mwaka 1968 hadi 1969 alihudumu katika wadhifa wa Balozi wa Tanzania nchini Ethiopia na Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU).

Mwaka 1969 hadi 1971, alikuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Utafiti na Huduma za Jamii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mwaka 1971 hadi 1972, Mheshimiwa Malecela aliteuliwa kuwa Waziri wa Fedha na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Fedha la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwaka 1972 hadi 1975, alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwaka 1975 hadi 1980 aliteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwaka 1980 hadi 1982, alikuwa Waziri wa Madini, na mwaka 1982 hadi 1985 alikuwa Waziri wa Mawasiliano, Ujenzi na Uchukuzi.

Mwaka 1986 hadi 1987 alikuwa Mjumbe wa Jopo la Watu Saba Maarufu Duniani wa Jumuiya ya Madola (Commonwealth Eminent

Persons Group), wakiwemo Malcolm Fraser (Australia), Olusegun Obasanjo (Nigeria), Lord Barber of Wentbridge (Uingereza), Dame Nita Barrow (Barbados), Sardar Swaran Singh (India) na Askofu Mkuu Ted Scott (Canada). Jopo hilo lilipewa jukumu la kuhamasisha mazungumzo baina ya pande mbili (Waafrika na Wazungu) nchini Afrika Kusini zilizokuwa zinapigana, ili hatimaye kuunda serikali ya umoja yenye uwakilishi mpana, bila chembe chembe za ubaguzi wa rangi.

Hali kadhalika, mwaka 1987 hadi 1989 alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa. Mwaka 1989 aliteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Uingereza na Jamhuri ya Ireland, ambako alihudumu hadi Oktoba, 1990.

Mwaka 1990 hadi mwaka 2010, alikuwa Mbunge wa Jimbo la Dodoma Vijijini (kwa sasa Jimbo la Mtera). Mwezi Novemba, 1990 aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi Desemba, 1994. Mwaka 1992 aliteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo wa Kwanza wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, wadhifa aliohudumu hadi mwaka 2012.



▲

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akimkabidhi Mhe. John Samwel Malecela, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hati ya Majukumu mara baada ya kuapishwa, Ikulu Dar es Salaam, tarehe 9 Novemba, 1990.*

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (1990–1994)

Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985–1995)

Tangazo la Serikali Na. 489 la tarehe 30 Novemba, 1990 kama linavyosomeka katika aya ya 1.2 (g) katika Kitabu hiki.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (1990–1994)

Katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa John Samwel Malecela, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, masuala mbalimbali yalijitokeza: uchumi ulioathiriwa na mabadiliko ya sera za kimataifa; mabadiliko ya



▲

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia) akizungumza Mhe. John Samwel Malecela, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto) baada ya kilele cha maadhimisho ya miaka 29 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Uwanja wa Taifa Dar es Salaam, tarehe 26 Aprili, 1993.*

kidemokrasia na ushirikishwaji wa wananchi; uzalishaji hafifu wa mashirika ya umma; na uamuzi wa Serikali wa kupunguza uendeshaji wa shughuli za uwekezaji kutekelezwa na Serikali.

Kutokana na masuala hayo, OMR ilitekeleza yafuatayo:

- Kuwasilisha Taarifa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Kuondoa Vikwazo vya Muungano (Kamati ya Shellukindo) katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 19 Agosti, 1994, ambapo Bunge lilipokea, lilijadili na kupitisha taarifa hiyo. Kupitia taarifa hiyo, Bunge lilielekeza kutekelezwa kwa maoni na mapendekezo yaliyotolewa.
- Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Sera ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma ya mwaka 1993, kwa lengo la kupanua mchango wa Sekta Binafsi katika uchumi na kuwawezesha wananchi kumiliki na kuendesha shughuli zao na kuongezeka kwa ajira.
- usimamia mabadiliko ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yaliyofanyika mwaka 1992 na kufuta mfumo wa chama kimoja cha siasa na kurejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa.
- Kusimamia kutungwa kwa Sheria ya Shirika la Posta Tanzania Na. 19 ya mwaka 1993, iliyoipa Shirika la Posta majukumu ya kuwa mhimili mkuu wa utoaji wa huduma za posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuratibu na kusimamia mawasiliano yote ya posta nchini. Aidha, Shirika hilo lilianza kazi rasmi tarehe 1 Januari, 1994. Kabla ya hapo huduma ya posta na simu zilisimamiwa kwa pamoja kupitia Sheria ya Shirika la Posta na Simu Tanzania Na. 15 ya mwaka 1977.

## Anavyokumbukwa

Katika kipindi cha Uongozi wake, Mheshimiwa John Malecela anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kipindi ambacho Bunge lilipitisha Azimio la kuwa na Serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano tarehe 24 Agosti, 1993 kutokana na hoja ya Kundi la Wabunge 55 wa CCM waliojiita G55. Kwa kuzingatia uzito wa suala lenyewe kuwa la kikatiba, utata wa kikatiba wa uamuzi huo kufanyika kwa njia ya Azimio la Bunge badala ya vifungu mahsusi vya marekebisho ya Katiba, na bila kuzingatia vipaumbele katika Ilani ya Uchaguzi, mambo mawili yakafanyika kiserikali na kichama mtawalia:
  a) Hoja hiyo haikuzingatia utaratibu na iliamualiwa iwasilishwe kwa wananchi.
  b) Tarehe 2 Desemba 1994, Mkuu wa Nchi, Mhe. Ali Hassan Mwinyi, akakivunja chombo chake kikuu cha ushauri, yaani Baraza la Mawaziri, na kumteua Mhe. Cleopa David Msuya kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais.
- Alisimamia mageuzi ya kiuchumi na kisiasa kwa kuruhusu mashirika binafsi kuwekeza katika sekta mbalimbali.

# Viongozi waliohudumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1990 hadi 1994



MHE. JOHN SAMWEL MALECELA
Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza
wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(1990-1994)



MHE. EDWARD N. LOWASSA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais
(Sera, Uratibu, Masuala ya Bunge na Uratibu wa Maafa)
(1990-1993)



MHE. ANNA M. ABDALLAH
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais
(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)
(1991-1994)



BW. PETER F. NGUMBULU
Katibu Mkuu
Ofisi ya Waziri Mkuu na
Makamu wa Kwanza wa Rais
(1990-1991)



BW. WILLIAM H. SHELLUKINDO
Katibu Mkuu
Ofisi ya Waziri Mkuu na
Makamu wa Kwanza wa Rais
(1991-1994)



# Mheshimiwa Cleopa David Msuya

## Wasifu

Mheshimiwa Cleopa David Msuya, alihudumu katika wadhifa wa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 5 Desemba, 1994 hadi tarehe 28 Novemba, 1995 katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Msuya, ni kiongozi wa mwisho katika utaratibu wa kuwa na Makamu wawili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Msuya alizaliwa tarehe 4 Januari, 1931 katika Kitongoji cha Chomvu, Usangi, Wilaya ya Mwanga, Tanzania Bara. Alikuwa mtoto wa tano kati ya watoto kumi waliozaliwa katika familia ya Bwana David Mhako Kilenga na Bibi Maria Nzota. Mwaka 1939 hadi 1942, alipata elimu ya Msingi na ya Kati katika Shule ya Msingi Kivindu na mwaka 1943 alihamia katika Shule ya Msingi ya Usangi Native, Mwanga. Mwaka 1944 hadi 1949 alipata elimu ya Sekondari katika Shule ya Wavulana ya Old Moshi. Mwaka 1950 hadi 1951 alisoma Shule ya Wavulana ya Tabora. Mwaka 1952 hadi 1955 alijiunga na Chuo Kikuu Kishiriki cha Makerere, ambako alihitimu masomo ya Sayansi ya Siasa katika Historia na Jiografia.

## Ajira na Uongozi

Mwaka 1956 hadi 1962, Mheshimiwa Msuya alikuwa Afisa Maendeleo ya Jamii katika Wilaya za Same, Moshi Vijijini na Tabora na baadaye kupandishwa cheo na kuwa Kamishna wa Maendeleo ya Jamii mwaka 1962. Mwaka 1964 hadi 1965 alishika wadhifa wa Katibu Mkuu katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Utamaduni. Mwaka 1965 hadi 1967 alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Maendeleo ya Makazi na Maendeleo ya Maji. Mwaka 1967 hadi 1970 alikuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mipango na Uchumi na mwaka 1970 hadi 1972 alikuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha.

Mwaka 1972 hadi 1975 alikuwa Mbunge wa kuteuliwa na Waziri wa Fedha. Mwaka 1975

hadi 1980 alihudumu katika wadhifa wa Waziri wa Viwanda. Mwaka 1980 alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mwanga na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi tarehe 22 Februari, 1983. Mwaka 1983 hadi 1985 aliteuliwa kuwa Waziri wa Fedha. Mwaka 1985 hadi 1990, aliteuliwa kuwa Waziri wa Fedha, Mipango na Uchumi. Mwaka 1990 hadi 1994 aliteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Tarehe 5 Desemba, 1994, Mheshimiwa Msuya aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi Novemba, 1995.

Mwaka 1995, alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mwanga na kuendelea na nafasi hiyo hadi alipostaafu tarehe 29 Oktoba, 2000.



▲

*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa kwanza kushoto), akimuapisha Mhe. Cleopa David Msuya (kulia), kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ikulu Dar es Salaam, tarehe 5 Desemba, 1994. Katikati ni Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Paul Rupia.*

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (1994–1995)

Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985–1995)

Tangazo la Serikali Na. 489 la tarehe 30 Novemba, 1990 kama linavyosomeka katika aya ya 1.2 (g) katika Kitabu hiki.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (1994–1995)

Katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Cleopa David Msuya, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, masuala mbalimbali yalijitokeza: wimbi la wakimbizi kutoka Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo lenye athari za kiusalama; kutowiana kwa sheria za uraia na uhamiaji, na kuendelea kutumika kwa masharti ya uhamiaji, kwa kuwataka Watanzania Bara wanaosafiri kwenda Zanzibar kuwa na Pasipoti; na kutokuwepo sera ya fedha inayozingatia misingi ya soko huria.



*Mhe. Cleopa David Msuya, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto) akizungumza na Mhe. Nelson Madiba Mandela (kulia), Rais wa Afrika Kusini, alipomwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ziara ya kikazi kuanzia tarehe 10 hadi 17 Mei, 1995, Johannesburg, Afrika Kusini.*



◀

*Mhe. Cleopa David Msuya, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akipata maelezo kuhusu utengenezaji wa chupa, alipotembelea kiwanda cha kutengeneza chupa mjini Johannesburg-Afrika Kusini, tarehe 21 Mei, 1995. Kulia ni Mhe. Venance Ngula, Naibu Waziri wa Fedha na wa pili kulia ni Mhe. Kate Kamba, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara.*



▲

*Mhe. Cleopa David Msuya, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizungumza na Mhe. Xie Youkun, Balozi wa China nchini Tanzania (kushoto), alipomtembelea Ofisini kwake jijini Dar es Salaam, tarehe 7 Julai, 1995.*

Kutokana na masuala hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rai ilitekeleza yafuatayo:

- Kusimamia kutungwa kwa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Na. 19 ya mwaka 1994 na kuanzishwa kwa Mikopo ya Elimu ya Juu.
- Kusimamia kutungwa kwa Sheria ya Uraia Na. 6 na Sheria ya Uhamiaji Na. 7, zote za mwaka 1995. Utungwaji wa Sheria hizo ulipelekea kufutwa kwa Sheria zilizokuwa zinasimamia masuala ya Uraia na Uhamiaji za Tanzania Bara na Zanzibar, hivyo kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na haki za Uraia kwa Watanzania kutoka pande zote mbili za Muungano.
- Kusimamia mageuzi ya sekta za fedha na uchumi, ikiwa ni kipaumbele cha Masuala ya Muungano, kwa kufanya mapitio ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Na. 1 ya mwaka 1995 ili kuondokana na majukumu mengi na kuiwezesha Benki Kuu ya Tanzania kujikita katika kusimamia utulivu wa bei na utekelezaji wa sera ya fedha inayozingatia misingi ya soko huria. Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliruhusu kuwepo kwa maduka ya kubadilishia fedha za kigeni na mabenki binafsi, pamoja na kuwekwa kwa mgao wa faida ya Benki Kuu baina ya SJMT na SMZ.
- Kusimamia utungaji wa Sheria Na. 11 ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya Mwaka 1995. .

## Anavyokumbukwa

Katika kipindi cha Uongozi wake, Mheshimiwa Cleopa Msuya anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Alikuwa kiongozi wa mwisho katika utaratibu wa kuwa na Makamu wawili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1994.
- Alikuwa ni Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyehudumu kwa kipindi kifupi cha miezi 11 katika historia ya Tanzania.
- Alikuwa Waziri aliyehudumu katika wadhifa wa Waziri wa Fedha kwa kipindi kirefu zaidi kwa nyakati tofauti (1972–1975, 1983–1985 na 1985–1990).

# Viongozi waliohudumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 5 Desemba, 1994 hadi tarehe 28 Novemba, 1995



MHE. CLEOPA DAVID MSUYA
Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(1994-1995)



MHE. ANNE S. MAKINDA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(Uratibu wa Shughuli za Serikali na Muungano)
(1994-1995)



MHE. ANNA M. ABDALLAH
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)
(1994-1995)



BW. WILLIAM H. SHELLUKINDO
Katibu Mkuu
Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(1994-1995)



# Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma

## Wasifu

Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma, alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 9 Novemba, 1995 hadi tarehe 4 Julai, 2001, katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Dkt. Omar alizaliwa tarehe 26 Juni, 1941 katika Kitongoji cha Wawi, Wilaya ya Chake Chake, Pemba. Alikuwa mtoto wa nne kati ya watoto watano waliozaliwa katika familia ya Bwana Ali Juma Ismail na Bibi Fatma Ali Masoud. Mwaka 1949 hadi 1957 alipata elimu ya msingi na ya Kati katika Shule ya Wavulana ya Chake Chake. Mwaka 1957 hadi 1960, alisoma katika Shule ya Sekondari ya Evan Smith, kwa sasa inaitwa Shule ya Sekondari ya Haile Selassie–Unguja. Mwaka 1960 hadi 1962 alijiunga na Chuo Kikuu cha Taifa–Moscow nchini Urusi, kwa masomo ya maandalizi ya miaka miwili. Mwaka 1962 hadi 1969, alisoma na kutunukiwa Shahada ya Tiba ya Mifugo na Upasuaji katika Chuo Kikuu cha Taifa, Moscow.

Mwaka 1969 alijiunga na Chuo Kikuu cha Cairo, Misri na kutunukiwa Stashahada ya Juu ya Uzalishaji wa Wanyama na Udaktari wa Mifugo *(Animal Production and Veterinary)*. Mwaka 1976 alijiunga na Chuo Kikuu cha Edinburgh, Uingereza, na kutunukiwa Stashahada ya Juu ya Tiba ya Magonjwa ya Mifugo ya Nchi za Kitropiki. Aidha, mwaka 1982 alijiunga na Chuo Kikuu cha Florida nchini Marekani kwa mafunzo ya muda mfupi ya Sayansi ya Mifugo. Vilevile, mwaka 1982, alipata fursa ya kusoma mafunzo ya Siasa katika Chuo cha Chama Kivukoni, kwa sasa ni Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam. Mwaka 1982, alijiunga na Chuo Kikuu cha Reading nchini Uingereza, ambapo alitunukiwa Cheti katika Fani ya Uchumi wa Mifugo.

## Ajira na Uongozi

Mwaka 1967 hadi 1969, Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma alikuwa Afisa Mifugo Msaidizi, Unguja na mwaka 1969 hadi 1970, alihudumu nafasi ya Afisa Mifugo katika kituo cha Pemba. Mwaka

1970 hadi 1971, alikuwa Afisa Mifugo Mwandamizi. Mwaka 1972 hadi 1978, alikuwa Afisa Mifugo Mkuu. Mwaka 1978 hadi 1984, alikuwa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mifugo, na mwaka 1984 hadi 1988 alikuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Zanzibar. Aidha, mwaka 1988 hadi 1995, Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma aliteuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waziri Kiongozi wa Zanzibar.

Mwaka 1995, baada ya Marekebisho ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1994 yaliyoweka mfumo mpya wa kumpata Makamu wa Rais kupitia Mgombea Mwenza, Dkt. Omar alichaguliwa kuwa mgombea mwenza wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, na hivyo kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 2001.



▲

*Mhe. Dkt. Omar Ali Juma, akiapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anayemuapisha ni Mhe. Barnabas Samatta (wa kwanza kulia), Jaji Mkuu wa Tanzania. Kushoto ni Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akishuhudia kiapo hicho Ikulu, Dar es Salaam, tarehe 9 Novemba, 2000.*



*Mhe. Dkt. Omar Ali Juma, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), akisalimiana na viongozi wa OMR mara baada ya kuapishwa. Wa nne kulia ni Mhe. Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), anayesalimiana naye ni Bw. Abubakar Mwingereza Rajabu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, na wa mwisho kulia ni Bw. Christopher Nyirabu, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu, Rais (aliyemaliza muda wake), Ikulu Dar es Salaam, Oktoba, 2000.*

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (1995–2001)

### Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1995–2005)

Matangazo ya Serikali Na. 720 la tarehe 28 Novemba, 1995 na Na. 468 la tarehe 1 Desemba, 2000 kama yanavyosomeka katika aya ya 1.2 (h) na (i) katika Kitabu hiki. Kupitia Matangazo haya, kwa mara ya kwanza suala la uhifadhi wa mazingira, usafi wa mazingira, udhibiti wa mmomonyoko wa udongo kwenye fukwe na Usimamizi wa Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira, linajitokeza miongoni mwa majukumu maalumu ya OMR.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Makamu wa Rais (1995–2001)

Wakati wa Uongozi wake, masuala mbalimbali yalijitokeza: uharibifu na uchafuzi wa mazingira nchini; Watanzania kuendelea kutumia hati ya kusafiria kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine wa Muungano; mabadiliko ya tabianchi; kuenea kwa hali ya jangwa nchini; uharibifu na upotevu wa bioanuai nchini; uvuvi holela wa bahari kuu; kuendelea kwa umaskini nchini; na uratibu duni wa shughuli za vikundi na taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali.

Kutokana na masuala yaliyojitokeza, OMR ilitekeleza yafuatayo:

- Kusimamia na kuiwezesha Tanzania kuridhia Mikataba mitatu ya Rio ambayo ni Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai (1996); Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (1996); na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (1997). Hatua hii iliwezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 198 zilizoridhia mikataba hiyo muhimu. Kuridhiwa kwa Mikataba hiyo kulitoa msukumo kwa Serikali kuandaa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira nchini. Aidha, msukumo uliwekwa Tanzania kuridhia Mkataba wa Rotterdam (1998) wenye lengo la kuweka utaratibu wa kupeana taarifa za biashara ya kimataifa ya Kemikali hatari za viwandani na viuatilifu; na Mkataba wa Ramsar wenye lengo la kuwa na matumizi endelevu ya ardhi oevu (1971) ambapo Tanzania iliridhia mwaka 2000.



*Mhe. Dkt. Omar Ali Juma, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, yaliyofanyika Mkoa wa Morogoro, tarehe 5 Juni, 2000. Kulia ni Bw. Reginald Mengi, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), mkoani Morogoro, tarehe 5 Juni, 2000.*



*Mhe. Dkt. Omar Ali Juma, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto) akiwa na Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Kilele cha Maadhimisho ya miaka 36 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam, tarehe 26 Aprili, 2000.*

- Kusimamia utungaji wa Kanuni za Uraia na Uhamiaji za mwaka 1997.
- Kusimamia maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997. Sera hiyo ilitoa mwongozo wa kushughulikia changamoto za mazingira na kuhamasisha maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi nchini na kuhakikisha hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu ya maliasili.
- Kusimamia utungwaji wa Sheria Na. 14 ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996.
- Kusimamia uanzishaji wa Sekretarieti ya Muungano katika Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 1998, kufuatia mapendekezo ya Kamati ya Shellukindo kuhusu jitihada za kuondoa mambo ambayo ni vikwazo katika kutekeleza shughuli za Muungano.
- Kusimamia uandaaji na ukamilishaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania wa mwaka 1998.
- Kusimamia kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 1 ya mwaka 1998, ikiwa ni miongoni mwa hatua za kuwa na sheria ya Muungano ya kusimamia masuala ya uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu.
- Kusimamia uanzishwaji na utekelezaji wa Chombo cha kutoa mikopo kwa ajili ya Miradi Midogo Midogo *(Small Entrepreneurs Loan Facility–SELF)* mwaka 1998, ikiwa na lengo la kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi maskini wa pande mbili za Muungano.
- Kuanzisha Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji miti Milioni Mia Moja kwa kila mwaka. Aidha, kampeni hii ilizinduliwa na Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 10 Aprili, 1999.

## Anavyokumbukwa

Katika kipindi cha uongozi wake, Mheshimiwa Dkt. Omar anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Makamu wa Rais wa kwanza kuhudumu katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, chini ya utaratibu wa kuwa na Mgombea Mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ulioanza kutumika mwaka 1995. Alikuwa mgombea mwenza wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa.
- Alikuwa Kiongozi aliyependa michezo na kwenda kutazama michezo hasa mpira wa miguu.

## Mauti

Mheshimiwa Dkt. Omar alifariki siku ya Jumatano tarehe 4 Julai, 2001 Jijini Dar es Salaam, akiwa na umri wa miaka 60. Alizikwa Alhamisi tarehe 5 Julai, 2001 katika Kitongoji cha Wawi, Pemba, Zanzibar.

# Viongozi waliohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuanzia mwaka 1995 hadi 2001



MHE. DKT. OMAR ALI JUMA
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(1995–2001)



MHE. BAKARI MBONDE
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(1995–1996)



MHE. MUHAMMED S. KHATIB
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(1996–1997)



MHE. EDWARD N. LOWASSA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(1997–2000)



MHE. DANIEL N. YONA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Umaskini na NGOs)
(2000–2001)



MHE. ARCADO D. NTAGAZWA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(2000–2001)



BW. CHRISTOPHER NYIRABU
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(1995–1996)



BW. PETER F. NGUMBULU
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(1996–2000)



BW. ABUBAKAR M. RAJABU
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2000–2001)



# Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein

## Wasifu

Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 3 Julai, 2001 hadi 5 Novemba, 2010 katika kipindi cha pili cha uongozi wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kipindi cha kwanza cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Dk. Shein, alizaliwa tarehe 13 Machi, 1948 katika Kitongoji cha Chokocho–Likokuu, Wilaya ya Mkoani, Pemba. Alikuwa mtoto wa mwisho kati ya watoto watano waliozaliwa katika familia ya Bwana Mohamed Shein na Bibi Chai Ali. Mwaka 1956 hadi 1964 alipata elimu ya msingi katika Shule ya Wavulana ya Gulioni, Unguja. Mwaka 1965 hadi 1968 alijiunga na Chuo cha Lumumba–Unguja, kwa sasa kinajulikana kama Shule ya Sekondari ya Lumumba.

Mwaka 1969, alijiunga na Chuo Kikuu cha Taifa cha Vorenezh, Urusi kwa masomo ya maandalizi ya mwaka mmoja. Mwaka 1970 hadi 1975 alisoma na kuhitimu Shahada ya kwanza pamoja na shahada ya Uzamili, fani ya Biokemia, katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Odessa, Urusi.

Mwaka 1984 hadi 1989, alihudhuria na kuhitimu Shahada ya Uzamivu katika fani ya *Clinical Biochemistry and Metabolic Medicine* na kuwa mtaalamu wa kuchunguza maradhi ya urithi kwa watoto katika Chuo Kikuu cha Newcastle Upon Tyne nchini Uingereza.

## Ajira na Uongozi

Mwezi Mei, 1969 Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein alianza kazi akiwa Karani katika Wizara ya Elimu, Zanzibar na baadaye alipandishwa cheo na kuwa Msaidizi wa Katibu Mkuu katika Wizara hiyo. Mwaka 1979 hadi 1989, alikuwa Mkuu wa Idara ya Huduma za Maabara ya Patholojia na Mshauri wa Wizara ya Afya–Zanzibar wa Uchunguzi wa Maradhi na Huduma za Maabara. Mwaka 1989 hadi 1995 alikuwa Mshauri wa Idara ya Patholojia na kuteuliwa kuwa Meneja wa Mradi wa Kinga dhidi ya Ukimwi, Zanzibar.

Mwaka 1995, Mheshimiwa Dk. Shein aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, na mwaka huo huo aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya wa SMZ, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 2000. Mwaka huo huo, Mheshimiwa Dk. Shein alichaguliwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mkanyageni, Pemba. Aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Utawala Bora wa SMZ, wadhifa aliohudumu hadi mwaka 2001.

Kufuatia kifo cha Mheshimiwa Dkt. Omar aliyefariki tarehe 4 Julai, 2001, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Mheshimiwa Dk. Shein kushika nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 13 Julai, 2001, wadhifa aliohudumu hadi mwezi Oktoba, 2005.

Mwaka 2005, Mheshimiwa Dk. Shein alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Mgombea Mwenza wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliyekuwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Mheshimiwa Dk. Shein alihudumu katika wadhifa huo hadi mwaka 2010.



▲

*Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, akiapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anayemuapisha ni Mhe. Barnabas Samatta, Jaji Mkuu wa Tanzania (katikati), Kushoto ni Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Dar es Salaam tarehe 13 Julai, 2001.*

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (2001–2005 na 2005–2010)

Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1995–2005) na uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2005–2015)

Tangazo la Serikali Na. 468 la tarehe 1 Desemba, 2000, na Tangazo Na. 2 la tarehe 13 Januari, 2006 kama yanavyosomeka katika aya ya 1.2 (i) na (j) katika Kitabu hiki.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Makamu wa Rais (2001–2010)

Katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, masuala yafuatayo yalijitokeza: kuendelea kwa uharibifu na uchafuzi wa mazingira ya ardhi, bahari, maziwa na mito pamoja na mabadiliko ya tabianchi ilisababisha pia kukauka kwa mabwawa ya kuzalisha umeme na hivyo nchi kuingia gizani; tishio la matumizi ya bioteknolojia ya kisasa isiyo rafiki kwa viumbe hai na mazingira kwa ujumla; tishio la matumizi ya kemikali hatarishi kwa mazingira na afya ya binadamu; kutokuwa na utaratibu mzuri wa kisheria na kitaasisi wa kuratibu masuala ya mazingira; hitaji la kuwa na chombo cha kusimamia shughuli za Takwimu kwa pande mbili za Muungano; na kuendelea kuwepo kwa hoja za Muungano zilizokuwa hazijapatiwa ufumbuzi.

Kutokana na masuala yaliyojitokeza, OMR ilitekeleza shughuli zifuatazo:

- Kusimamia Tanzania kuridhia na kutekeleza mikataba ifuatayo: Mkataba Mdogo wa Kyoto (1997), wenye lengo la kuzitaka nchi zilizoendelea ambazo zinazalisha gesijoto kwa wingi zaidi, kupunguza kiwango cha uzalishaji wa gesijoto kwa asilimia 5 ikilinganishwa na uzalishaji wake wa mwaka 1990, ambapo Tanzania iliridhia Mkataba huo mwaka 2002; na Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika (2003) wenye lengo la kuwa na usimamizi shirikishi wa ziwa hilo baina ya nchi nne ambazo ni Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Zambia, ambao uliridhiwa na Tanzania mwaka 2004.
- Kusimamia Tanzania kuridhia na kutekeleza Mikataba mbalimbali ya Mazingira, ikiwemo: Mkataba wa Rotterdam (1998) unaoweka utaratibu wa kupeana taarifa juu ya Biashara ya Kimataifa ya kemikali hatarishi za viwandani na viuatilifu, ulioridhiwa mwaka 2002; Mkataba wa Stockholm (2001), unaolinda afya ya jamii na mazingira dhidi ya madhara ya kemikali zinazodumu kwa muda mrefu katika mazingira, ulioridhiwa mwaka 2004; na Itifaki ya Cartagena (2002) kuhusu matumizi salama ya Bioteknolojia ya Kisasa iliyoridhiwa mwaka 2004.

- Kusimamia utungwaji wa Sheria ya Nguvu za Atomiki Na. 7 ya Mwaka 2003. Kupitia Sheria hiyo, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) iliundwa ikiwa ni Taasisi ya Muungano na kusimamia matumizi salama ya nguvu za atomiki na usalama wa mionzi kwa mazingira na afya ya binadamu, pamoja na kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia. Kupitia tume hiyo, Serikali imesimamia vyema na kuendeleza matumizi salama ya nguvu za Atomiki katika sekta za Afya, Kilimo, Viwanda, Madini na Nishati (Gesi Asilia).
- Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mikakati ya kitaifa ifuatayo: Mkakati wa Usimamizi wa Mazingira ya Pwani wa mwaka 2003; Mkakati wa Hatua za Haraka za kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na



▲

*Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (aliyeketi katikati) akiwa pamoja na wataalamu wa Mazingira katika Mkutano wa Nchi za Afrika Zinazozungumza Kiingereza, kuhusu usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Kulia kwa Makamu wa Rais ni Mhe. Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, fisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), na kushoto kwake ni Bi. Mary Mushi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais. Mkutano huo wa wiki moja ulifanyika katika hoteli ya Golden Tulip, Dar es Salaam, kuanzia tarehe 9-12 Machi, 2004.*

vyanzo vya Maji wa mwaka 2006; pamoja na Mkakati wa Hatua za Haraka za Uhifadhi wa Mazingira ya Pwani, Bahari, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2008.

- Kusimamia uanzishwaji wa Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) mwaka 2005, kupitia Sheria ya Vyuo Vikuu Sura 346, ikiwa ni utekelezaji wa Jambo la Muungano la Elimu ya Juu kwa ajili ya kudhibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini kwa pande mbili za Muungano. Tangu kuanzishwa kwake, idadi ya Vyuo Vikuu iliongezeka kutoka 23 mwaka 2005 hadi kufikia 37 mwaka 2010. Pia udahili kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu kutoka pande zote mbili za Muungano, uliongezeka kutoka 55,290 na kufikia 139,639.





▲

*Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (pichani kushoto) akizindua jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam. Anayeshuhudia tukio hilo ni Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Aprili, 2009.*

- Kusimamia kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 na utekelezaji wake ulianza tarehe 1 Julai, 2005. Katika Sheria hiyo, NEMC ilipewa Mamlaka ya kisheria ya kusimamia masuala ya mazingira nchini. Aidha, kupitia Sheria hiyo, Taarifa ya Kwanza ya Hali ya Mazingira Nchini iliandaliwa mwaka 2008 kwa mujibu wa Kifungu cha 175(1) cha Sheria hiyo na kuwasilishwa Bungeni ipasavyo. Pia, Sheria hiyo iliweka mfumo wa kitaasisi na kiutawala wa usimamizi wa mazingira katika ngazi zote; kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango ya maendeleo, sera za kisekta, na mipango ya Serikali za Mitaa.
- Kusimamia usajili na uratibu wa Mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotekeleza majukumu yake katika nyanja mbalimbali za elimu, afya, kilimo, utafiti, haki za binadamu na utawala bora mwaka 2004.
- Kusimamia ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais yaliyopo Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam na Tunguu, Zanzibar, mwaka 2009. Uwepo wa Ofisi hizo, ulisogeza huduma kwa wananchi kwa pande zote mbili za Muungano.
- Kusimamia vikao sita vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ambapo tarehe 2 Juni, 2010 hoja mbili za Muungano zilipatiwa ufumbuzi. Hoja hizo zilihusu Utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa upande wa Zanzibar; na Utekelezaji wa Sheria ya Usafiri Majini katika Jamhuri ya Muungano na Uwezo wa Zanzibar kujiunga na Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini (IMO) kama Mwanachama Mshiriki.



◀ *Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa pili kushoto) akiongoza kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano. Kushoto kwake ni Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kulia kwake ni Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi wa Zanzibar, Dar es Salaam, tarehe 19 Mei, 2009.*

- Kusimamia kuanzishwa kwa Programu, Mifuko na Miradi ya Maendeleo, Kiuchumi na Kijamii, iliyotekelezwa pande zote mbili za Muungano, kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Programu ya Usimamizi wa Bahari na Pwani (MACEMP), Mfuko wa kutoa mikopo kwa ajili ya Miradi Midogomidogo (SELF), Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Sekta ya Mifugo (ASDP), Programu za Maendeleo ya Kilimo (PADEP), na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).
- Kusimamia marekebisho ya Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 4 ya mwaka 2007 na kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu mwaka 2010 ambapo Makao Makuu yake yapo Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa utekelezaji wa masuala ya Muungano.
- Kusimamia utungaji wa Sheria mpya ya Takwimu Sura 351 ili kuboresha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu nchini. Kupitia Sheria hiyo, Serikali ilianzisha Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuwa Wakala wa Serikali na kuipa majukumu ya kuendesha Sensa ya Watu na Makazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi ya Taifa ya Takwimu inashirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kwenye masuala yote ya Takwimu yanayohusu Zanzibar. Aidha, uwepo wa Sheria na Taasisi hiyo umesaidia kuondoa vikwazo vya utafiti kwa pande mbili za Muungano.

## Anavyokumbukwa

Mheshimiwa Dk. Shein anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Kiongozi aliyeshika wadhifa wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadaye kushika wadhifa wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Kiongozi aliyehudumu nafasi za juu za uongozi kwa miaka 19 (Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania miaka 9 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi miaka 10).




▲

*Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Afrika yaliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha AICC, Jijini Arusha, tarehe 3 Machi, 2010*



◀

*Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipotembelea Maonesho ya Wiki ya Sekta Binafsi Tanzania. Alioambatana nao ni Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Viwanda na Biashara na Bi. Esta Mkwizu, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania mwaka 2008.*

# Viongozi waliohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuanzia mwaka 2001 hadi 2010



MHE. DK. ALI MOHAMED SHEIN
Makamu wa Rais
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(2001-2010)



MHE. DANIEL N. YONA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Umaskini na NGOs)
(2001-2002)



MHE. ARCADO D. NTAGAZWA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(2001-2005)



MHE. EDGAR M. MAJOGO
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Umaskini na NGOs)
(2002-2005)



MHE. DKT. BATILDA S. BURIAN
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Mazingira)
(2008-2010)



MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Mazingira)
(2006-2008)



MHE. DKT. HUSSEIN A. MWINYI
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano)
(2006-2008)



MHE. MUHAMMED S. KHATIB
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano)
(2008-2010)



BW. ABUBAKAR M. RAJABU
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2000-2003)



BW. RAPHAEL O. S. MOLLEL
Katibu Mkuu Mwandamizi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2003-2005)



BI. MARY I. MUSHI
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2003-2006)



BW. ABUBAKAR M. RAJABU
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2006-2007)



BI. RUTH H. MOLLEL
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2007-2010)



BW. SAZI B. SALULA
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2006-2007)



BW. MBARAK ABDULWAKIL
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2009-2010)



# Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal

## Wasifu

Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 6 Novemba, 2010 hadi 5 Novemba, 2015 katika kipindi cha pili cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Dkt. Bilal alizaliwa tarehe 6 Februari, 1945, Unguja. Alikuwa mtoto wa tatu katika familia ya watoto 22 ya Bw. Gharib Bilal na Bi. Safia Abeid. Alipata elimu ya msingi na elimu ya kati kuanzia mwaka 1951 hadi 1958 katika Shule za Makunduchi (Wilaya ya Kusini), Mfenesini (Wilaya ya Magharibi), Gulioni (Wilaya ya Mjini) na Chwaka (Wilaya ya Kati), Unguja. Mwaka 1959 hadi 1962 aliendelea na masomo ya Sekondari katika Shule ya Beit–el–Ras ambayo kwa sasa ni Kampasi ya Ualimu katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), na baadaye alisoma Shule ya Sekondari Lumumba, Zanzibar.

Kabla ya kuhitimu masomo ya elimu ya juu ya Sekondari, alipata ufadhili wa masomo ya Fizikia katika Chuo Kikuu cha Howard, Washington nchini Marekani na kuhitimu Shahada ya Kwanza katika fani ya Fizikia na Hesabu mwaka 1967. Aidha, mwaka 1969, Dkt. Bilal alipata Shahada ya Uzamili katika Fizikia kutoka Chuo Kikuu cha Berkeley, California–Marekani na mwaka 1976 alihitimu Shahada ya Uzamivu katika Fizikia (Nyuklia) katika chuo hicho hicho.

## Ajira na Uongozi

Mwaka 1976, alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam akiwa Mhadhiri wa Fizikia, na mwaka 1983 alichaguliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Fizikia ya Nyuklia. Mwaka huo huo wa 1983 alishiriki kwenye maandalizi ya kuunda Tume ya Taifa ya Mionzi na kuchangia utaalamu katika utayarishaji wa rasimu ya sheria iliyopelekea kutungwa kwa Sheria ya Matumizi na Udhibiti wa Mionzi ya Nyuklia Nchini Tanzania. Mwaka 1989 aliteuliwa kuwa Mkuu wa

Kitivo cha Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuendelea na wadhifa huo hadi mwaka 1990. Mwaka 1990 hadi 1995 alishika wadhifa wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwaka 1995 hadi 2000, Mheshimiwa Dkt. Bilal alishika wadhifa wa Waziri Kiongozi wa Zanzibar. Mwaka 2010 alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuapishwa tarehe 6 Novemba, 2010. Alihudumu katika wadhifa huo hadi mwaka 2015.

*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, akiapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anayemuapisha ni Mhe. Augustino Ramadhani, Jaji Mkuu wa Tanzania. Anayeshuhudia ni Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (aliyekaa katikati), Ikulu Dar es Salaam, tarehe 6 Novemba, 2010.*

▼



## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (2010–2015)

Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2005–2015)

Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba, 2010 kama linavyosomeka katika aya ya 1.2 (k) katika Kitabu hiki.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Makamu wa Rais (2010–2015)

Katika uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania masuala mbalimbali yalijitokeza: uelewa mdogo wa masuala ya Muungano hususan kwa Watanzania waliozaliwa baada ya Muungano na kupelekea kutoa au kupokea taarifa za upotoshaji kuhusu masuala ya Muungano, uwepo wa Mabadiliko ya Tabianchi na changamoto ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Kutokana na masuala hayo, OMR ilitekeleza shughuli zifuatazo:

- Kusimamia kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura 83 ili kuruhusu taratibu za kuandaa Katiba Mpya.
- Kusimamia kutungwa kwa Sheria ya Takwimu Sura 351 mwaka 2015 inayosimamia masuala ya Takwimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa na lengo la kuainisha majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuweka vyombo vya usimamizi wa Takwimu: Bodi ya Usimamizi wa takwimu ikiwa na wajumbe kutoka pande mbili za Muungano. Sheria hiyo ilifuta Sheria ya Takwimu ya mwaka 2002.
- Kusimamia Maadhimisho ya kihistoria ya nusu karne (Miaka 50) ya Muungano yaliyofanyika tarehe 26 Aprili, 2014 na kutoa mwongozo wa uandaaji wa Kitabu cha Taarifa ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (1964–2014). Maadhimisho na Kitabu hicho ni rejea ya elimu ya Muungano.
- Kuzindua na kusimamia utekelezaji wa Kampeni ya Usafi wa Mazingira Katika Miji na Majiji nchini mwaka 2011. Lengo la Kampeni hiyo ni kuhimiza jamii kushiriki katika usafi wa mazingira kuanzia ngazi ya kaya hadi ngazi ya Taifa.
- Kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa Kimataifa wa kutathmini utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu ya miaka 20 baada ya makubaliano ya Rio ya mwaka 1992.
- Kusimamia kuandaliwa kwa Taarifa ya Pili ya Hali ya Mazingira Nchini mwaka 2014, kwa mujibu wa Kifungu cha 175(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura

191. Taarifa hiyo imeainisha mafanikio na changamoto katika uhifadhi wa mazingira nchini.

- Kuongoza vikao vya kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Muungano vilivyofanyika tarehe 28 Januari, 2012; tarehe 13 Januari, 2013; na tarehe 23 Juni, 2013.



▲

*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia), akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri, kushoto kwake ni Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kulia kwake ni Balozi Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi wa SJMT. Kikao hicho kilifanyika Ukumbi wa Jengo la Mkapa, Dodoma, tarehe 6 Julai, 2012.*




*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia), akisoma ujumbe kuhusu kampeni ya kuhamasisha hifadhi ya misitu, alipotembelea mabanda ya maonesho katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Uwanja wa Majimaji mjini Songea, Mkoa wa Ruvuma, tarehe 1 Juni, 2011.*




*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), akihutubia katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Mataifa kuhusu Tathmini ya Utekelezaji wa Masuala ya Mazingira Endelevu, (RIO+20) alipomwakilisha Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kulia ni Mhe. Fatma Fereji, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (wa kwanza kulia), Mhe. Mahadhi Juma Maalim, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mhe. Dkt. Terezya Huvisa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), jijini Rio de Jenario Brazil, tarehe 21 Juni, 2012.*



▲

*Mhe. Dkt. Mohammed Gharib Bilal (katikati), Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongoza kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano. Viongozi wengine ni Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (wa pili kushoto), Waziri Mkuu, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Seif Ali Idd (wa pili kulia), Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Samia Suluhu Hassan (kushoto), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mhe. Mohamed Aboud (kulia), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, katika Ukumbi wa Hoteli ya Zanzibar Beach Resort, Zanzibar, tarehe 14 Januari , 2013.*



◀

*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akisalimiana na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kilele cha Maadhimisho ya miaka 49 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 2013. Kutoka kulia ni Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Seif Sharrif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.*

# Anavyokumbukwa

Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Alihimiza ujenzi wa maeneo ya kupumzikia abiria ikiwemo vyoo vya kisasa katika barabara zote kuu nchini kwa lengo la kuhimiza usafi wa Mazingira.
- Alihimiza matumizi ya sayansi na teknolojia katika taasisi mbalimbali nchini.
- Alihamasisha uchimbaji wa visima vya maji safi, Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kupata maji safi na salama.



▲

*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), akimsikiliza Bw. Adrian Aloyce, Mwalimu wa Umeme katika Karakana ya mafunzo, wakati akifafanua jinsi Mashine za 'Automatic System' zinavyojiendesha zenyewe, alipotembelea Chuo (kipya) cha TEHAMA cha VETA, Kipawa, jijini Dar es Salaam, tarehe 1 Juni, 2013. Kulia ni Mhe. Said Meck Sadick, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.*




◀

*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akimwakilisha Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano katika mkutano wa 27 wa pamoja wa kimataifa wa watafiti wanasayansi wa Afrika kuhusu magonjwa ya binadamu. Kushoto kwake ni Dkt. Mwele Malecela, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu na kulia kwake ni Mhe. Dkt. Seif Rashid, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii SJMT, uliofanyika jijini Arusha, tarehe 16 Aprili, 2013.*



*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongozana na Balozi. Dkt. Batilda Burian (wa kwanza kushoto kwake), Balozi wa Tanzania Nchini Kenya, na Viongozi wengine wakati alipowasili Jijini Nairobi tarehe 20 Julai, 2013 kwa ajili ya kuhudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali, Ukanda wa Maziwa Makuu.*




*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), akimwakilisha Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Viongozi wa Nchi na Serikali, Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika Jijini Nairobi, Kenya tarehe 31 Julai, 2013.*



*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizungumza na Balozi. Alfonso Lenhardt, Balozi wa Marekani nchini Tanzania aliyemaliza muda wake, ofisini kwake Ikulu jijini Dar es Salaam, tarehe 3 Oktoba, 2013 kwa ajili ya kumuaga.*

## Viongozi waliohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuanzia mwaka 2010 hadi 2015



MHE. DKT. MOHAMMED GHARIB BILAL
Makamu wa Rais
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(2010–2015)



MHE. SAMIA S. HASSAN
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano)
(2010–2015)



MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Mazingira)
(2010–2014)



MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Mazingira)
(2014–2015)



MHE. CHARLES M. KITWANGA
Naibu Waziri
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(2012-2014)



MHE. UMMY A. MWALIMU
Naibu Waziri
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Mazingira)
(2014-Januari, 2015)



MHE. STEPHEN J. MASELE
Naibu Waziri
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(Januari, 2015-Oktoba, 2015)



BW. SAZI B. SALULA
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2011-2015)



BW. MBARAK ABDULWAKIL
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2015)



MHANDISI NGOSI C. X. MWIHAVA
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2010-2013)



MHANDISI ANGELINA E. MADETE
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2014-2015)



# Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

## Wasifu

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 5 Novemba, 2015 hadi 18 Machi, 2021. Ni mwanamke wa kwanza nchini kushika nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Dkt. Samia alizaliwa tarehe 27 Januari, 1960 katika Kijiji cha Kizimkazi, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar akiwa ni mtoto wa tatu katika familia ya watoto 15 ya Mwalimu Suluhu Hassan Haji na Bi. Mwamvua Yussuf (binti Yussuf).

Alipata elimu ya msingi na ya kati katika skuli tofauti zikiwemo: Skuli ya Chwaka–Unguja, mwaka 1966 hadi 1968; Skuli ya Ziwani–Pemba, mwaka 1970 hadi 1971; na Skuli ya Msingi Mahonda–Unguja mwaka 1972. Mwaka 1973 hadi 1976, alisoma Skuli za Sekondari za Ng'ambo na Lumumba, Unguja.

Mwaka 1983, alipata Astashahada ya mafunzo ya Takwimu kutoka Chuo cha Uchumi, Zanzibar. Baada ya kufanya kazi kwenye Wizara ya Mipango na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mwaka huohuo alijiunga na Chuo cha Maendeleo ya Uongozi Mzumbe (IDM) kwa ajili ya masomo ya juu katika Utawala wa Umma na kutunukiwa Stashahada ya Juu mwaka 1986. Aidha, alipata mafunzo mbalimbali katika: Taasisi ya Chuo cha Utawala wa Umma Lahore, Pakistan mwaka 1987; Taasisi ya Eastern and Southern African Management Institute (ESAMI), Arusha mwaka 1991; na Taasisi ya Uongozi ya Hyderabad, India mwaka 1998, kwa ajili ya Astashahada ya Utawala. Mwaka 1992 alijiunga na Chuo Kikuu cha Manchester kilichopo Uingereza na kutunukiwa Stashahada ya Juu ya Uchumi mwaka 1994. Mwaka 2004, alijiunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania katika programu ya pamoja na Chuo Kikuu cha Southern New Hampshire, Marekani, na kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Maendeleo ya Jamii na Uchumi mwaka 2005.

## Ajira na Uongozi

Mwaka 1977 hadi 1983, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa Karani wa Masijala katika Wizara ya Mipango na Maendeleo ya SMZ. Mwaka 1987 hadi 1988, alishika wadhifa wa Afisa Mipango Rasilimali Watu, na mwaka 1988 hadi 1997, alifanya kazi na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (World Food Programme–WFP). Mwaka 2000 hadi 2010 alikuwa Mwakilishi wa Viti Maalumu vya Wanawake katika Baraza la Wawakilishi, Zanzibar na mwaka 2000 hadi 2005 aliteuliwa kuwa Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake, na Watoto, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mwaka 2005 hadi 2010, aliteuliwa kuwa Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mwaka 2010 alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Makunduchi na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 2015. Akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) mwaka 2014, aliteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lililoandaa Rasimu ya Katiba. Mwaka 2015 alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, wadhifa aliohudumu hadi mwezi Machi, 2021.



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayemuapisha ni Mhe. Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu wa Tanzania. Wengine ni Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (aliyeketi kushoto), Mhe. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayemaliza muda wake (aliyekaa katikati) na Balozi Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi (aliyesimama katikati), Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, tarehe 6 Novemba, 2015.*



▶ *Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri, kulia kwake ni Mhandisi Balozi John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi wa SJMT katika ukumbi wa Jengo la Mkapa House, jijini Dodoma tarehe 29 Oktoba, 2019.*



▲ *Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa kwenye kikao na wajumbe wa menejimenti ya OMR na NEMC, katika Ukumbi wa Mikutano wa Kambarage,Treasury Square. Kutoka kulia kwake ni Mhandisi Joseph Malongo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais na Balozi Joseph Sokoine, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, jijini Dodoma, tarehe 6 Juni, 2020.*



Mwaka 2016 hadi 2017, alikuwa Mjumbe wa Jopo la Umoja wa Mataifa kuhusu Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi, akiwakilisha Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Pamoja na kushika nyadhifa mbalimbali, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwahi kuwa Mwanachama na Mwanzilishi wa Taasisi ya Kuchochea Maendeleo ya Wanawake Zanzibar (1991–1994); Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Taasisi Zisizo za Kiserikali Zanzibar (ANGOZA 1995–2000); Mjumbe wa Bodi ya Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (Equal Opportunity Trust Fund–EOTF) (1996–2000); na Mjumbe wa Kamati ya Msamaha wa Wafungwa (Parole Committee, 2001–2010).




▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa kwanza kulia), akihutubia katika mkutano wa kawaida wa 31 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) alipomwakilisha Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nyuma yake ni Mhe. Balozi Dkt. Augustine Mahiga, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, jijini Nouakchott-Mauritania, Julai 2018.*

# Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (2015–2021)

Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2015–2021)

Tangazo la Serikali Na. 143 la tarehe 22 Aprili, 2016 kama linavyosomeka katika aya ya 1.2 (I) katika Kitabu hiki.

# Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria katika Ofisi ya Makamu wa wa Rais (2015–2021)

Katika kipindi cha uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, masuala mbalimbali yalijitokeza: uwepo wa hoja za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi, kutokuwepo kwa utaratibu rasmi wa uendeshaji wa vikao vya kujadili hoja za Muungano, uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya Muungano, faida na fursa zinazopatikana kutokana na Muungano, matumizi ya mifuko ya plastiki isiyo rafiki



▲

*Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika Ukumbi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mtumba-Dodoma, tarehe 7 Agosti, 2020. Kulia kwake ni Mhe. Mussa Azzan Zungu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na kushoto kwake ni Mha. Joseph Malongo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais.*

kwa mazingira, uchafuzi wa mazingira, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji, uvuvi haramu, uwepo wa athari za mabadiliko ya tabianchi na uelewa mdogo wa jamii kuhusu hifadhi ya mazingira.

Kutokana na masuala hayo, OMR ilitekeleza yafuatayo:

- Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji (2006); Mkakati wa Kitaifa wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Pwani, Bahari, Maziwa, Mito na Mabwawa (2008); na Mkakati wa Taifa wa hifadhi ya Bioanuai (2015–2020).
- Kusimamia maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Kupanda Miti (2016–2021) wa mwaka 2016 ikiwa na lengo la kuhakikisha nchi inakuwa ya kijani. Mkakati huu umezingatia kurekebisha changamoto zilizojitokeza katika mikakati ya kampeni zilizopita, ikiwemo motisha na ushiriki wa sekta binafsi katika biashara ya rasilimali za misitu.
- Kumwakilisha Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano katika Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu ulinzi na usalama (Troika) mwaka 2017.
- Kusimamia Tanzania kuridhia na kutekeleza Mkataba wa Minamata wa mwaka 2017 Kuhusu Zebaki, wenye lengo la kupunguza na kuondoa matumizi ya



◀ *Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akipanda mti kwenye Msitu wa asili ulioasisiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuelekea kilele cha Siku ya Mazingira Duniani, Butiama, Mkoa wa Mara tarehe 4 Juni, 2017.*

Zebaki kwa wachimbaji wadogo. Tanzania iliridhia Mkataba mwaka 2020.

- Kuanzisha na Kuzindua Kampeni ya Kuifanya Dodoma kuwa ya Kijani "Kijanisha Dodoma" tarehe 21 Desemba, 2017 yenye lengo la kunusuru Jiji la Dodoma, pamoja na mikoa mingine, dhidi ya hali ya ukame na uharibifu wa mazingira.
- Kusimamia maandalizi ya Mwongozo wa Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano baina ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za SJMT na SMZ na kuzinduliwa mwaka 2018. Lengo ni kuimarisha ushirikiano ambapo vikao hufanyika kujadili masuala ya kisekta, kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu kupitia mafunzo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa. Vikao hivyo vimesaidia kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Muungano na za kisekta zilizopo na zinazojitokeza kwa haraka na kwa ufanisi.
- Kusimamia Tanzania kuridhia Makubaliano ya Paris ya mwaka 2018 kuhusu kushughulikia mabadiliko ya tabianchi hasa upunguzaji wa gesijoto kwa lengo la kudhibiti ongezeko la joto la dunia lisizidi nyuzi joto 2 au 1.5 na kusaidia nchi zinazoendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchochea maendeleo endelevu.
- Kusimamia Miradi na Programu za kuinua hali ya uchumi wa wananchi wa pande mbili za Muungano. Miongoni mwa Miradi na Programu za maendeleo zilizoendelea kutekelezwa katika kipindi hiki ni: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III); Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (MIVARF); iliyolenga: Kuongeza thamani ya mazao; Kuwajengea uwezo wananchi na kuwaunganisha na masoko; na kuwezesha upatikanaji wa huduma za fedha vijijini, Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (ERPP); Mradi wa Udhibiti Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish); Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA); Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR); Mpango wa Kupanua Usikivu Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC); Mradi wa Uboreshaji wa Elimu; Mkakati wa Kudhibiti Sumu Kuvu Tanzania; Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha; na Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.
- Kuboresha/kuweka mfumo rasmi wa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ulioimarisha na kurasimisha utaratibu wa vikao hivyo katika ngazi mbalimbali. Utaratibu huo, ulizinduliwa tarehe 9 Februari 2019, Dodoma.
- Kupiga marufuku uzalishaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki nchini kuanzia tarehe 1 Juni, 2019 na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache katika Bara la Afrika na duniani zilizofanikiwa kuchukua hatua hiyo.



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akikata utepe kuzindua Jengo la Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, tarehe 8 Agosti, 2020. Kulia kwake ni Mhe. Jabir Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Mpwawa, akifuatiwa na Mhe. George Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kushoto kwake ni Mhe. Kapten Geoge Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akikagua ukuta wa ufukwe wa bahari uliojengwa kando ya barabara ya Barack Obama jijini Dar es Salaam. Kulia kwake ni Mhe. January Y. Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), tarehe 5 Juni, 2018.*

- Kusimamia uandaaji wa Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira, Nchini ya mwaka 2019. Lengo la taarifa hii ni kutoa elimu na kuhamasisha jamii, viongozi na watendaji katika sekta ya Umma kuhusu hali ya mazingira nchini na kuchukua hatua stahiki.
- Kusimamia ufumbuzi wa Hoja tano (5) za Muungano na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano tarehe 17 Oktoba, 2020 ambazo ni: Ushirikishwaji wa SMZ kwenye Masuala ya Kimataifa na Kikanda; Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Gharama za kushusha mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwa mizigo inayotoka Zanzibar; Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia; na Utaratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kushughulikia masuala ya Muungano.
- Kusimamia uchumi wa Taifa na kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 6 hadi 7 na kuiwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za kipato cha kati mwezi Julai 2020.




▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akishuhudia tukio la kusaini hati za makubaliano ya kuondoa hoja tano kwenye Orodha ya Hoja za Muungano. Hafla hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Ikulu Dar es Salaam, tarehe 17 Oktoba, 2020.*




▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akimwakilisha Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 33 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Februari, 2020. Nyuma yake ni Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na Mhe. Naimi Aziz, Balozi wa Tanzania nchini Ethiopia na Mwakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Afrika.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa katika picha ya pamoja na Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya hafla ya kuapishwa Mhe. Prof. Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Chamwino Dodoma, tarehe 9 Novemba, 2020. Kulia ni Dkt. Benelith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, akifuatiwa na Mhe. Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania. Kushoto ni Balozi. John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi, Mhe. Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

# Anavyokumbukwa

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anakumbukwa kwa mambo yafuatayo:

- Mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa Makamu wa Rais nchini Tanzania.
- Alikuwa mjumbe wa Jukwaa la Viongozi wa Umoja wa Mataifa la kushughulikia masuala ya kiuchumi na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, kuanzia mwaka 2016 hadi 2017.
- Kiongozi aliyeshika wadhifa wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais na baadaye Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Alikuwa mlezi wa timu za soka za vijana wa kike na kiume chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Girls na Serengeti Boys, ambazo zimekuwa na mafanikio makubwa katika soka ndani na nje ya nchi, mfano Serengeti iliweza kuchukua ubingwa wa COSAFA Desemba, 2018 na Twiga Stars ilifanikiwa kushiriki michuano ya kombe la dunia nchini India, Oktoba, 2022.




*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizindua Mpango Maalumu wa Mafunzo kwa Vitendo katika sehemu ya kazi kwenye Mkutano wa Mawaziri wa Sekta ya Kazi, Ajira na Wadau wa Utatu wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere Jijini Dar es salaam, tarehe 4 Machi, 2020. Kushoto ni Mhe. Jenista Mhagama, Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kulia ni Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Mhe. Mouldine Castico, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongoza kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano, kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kambarage, Treasury Square, Dodoma, tarehe 9 Februari, 2019. Kulia kwake ni Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na kushoto kwake ni Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.*



◀

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizungumza na Balozi Frederic Clavier, Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Ikulu Jijini Dar es salaam tarehe 30 Septemba, 2019.*

# Viongozi Waliohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuanzia mwaka 2015 hadi 2021



MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
Makamu wa Rais
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(2015–2021)



MHE. JANUARY Y. MAKAMBA
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu Rais
(Muungano na Mazingira)
(2015–2019)



MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(Julai 2019–Januari 2020)



MHE. MUSSA A. ZUNGU
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(Januari, 2020–Novemba, 2020)



MHE. UMMY A. MWALIMU
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(Novemba, 2020–Aprili, 2021)



MHE. LUHAGA J. MPINA
Naibu Waziri
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(2015-2017)



MHE. KANGI A. LUGOLA
Naibu Wazir
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(2017-2018)



MHE. MUSSA R. SIMA
Naibu Waziri
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(2018-2020)



MHE. MWITA M. WAITARA
Naibu Waziri
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)
(2020-2021)



BW. MBARAK ABDULWAKIL
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2015-2016)



PROF. FAUSTINE R. KAMUZORA
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2016-2017)



MHANDISI JOSEPH K. MALONGO
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2017-2021)



MHANDISI NGOSI C. X. MWIHAVA
Naibu Katibu Mkuu,
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2015-2017)



BI. BUTAMO K. PHILLIP
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2017-2018)



BALOZI JOSEPH E. SOKOINE
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(2018-2021)



# Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango

## Wasifu

Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 30 Machi, 2021 hadi sasa. Alishika wadhifa huo katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Alifundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa miaka 14. Pia, ni mtafiti katika masuala ya uchumi na fedha, kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Dkt. Mpango alizaliwa tarehe 14 Julai, 1957 katika Kijiji cha Kasumo, Wilaya ya Buhigwe, Mkoa wa Kigoma, akiwa ni mtoto wa saba katika familia ya watoto 11 ya Bw. Isdor Nzabayanga Mpango na Bi. Lusia Mushatsi.

Alipata elimu ya msingi katika shule za: Kipalapala, Tabora mwaka 1964 hadi 1965; Kasumo, Kigoma mwaka 1965 hadi 1967; na Muyama, Kigoma mwaka 1968 hadi 1970. Aidha, alipata elimu ya sekondari kidato cha kwanza hadi cha nne katika shule za: Ujiji Seminari–Kigoma, mwaka 1971 hadi 1973; na Itaga Seminari–Tabora, mwaka 1974 hadi 1975. Mwaka 1976 alijiunga na Shule ya Sekondari ya Ihungo–Bukoba kwa masomo ya kidato cha tano na sita, na kuhitimu mwaka 1977.

Mwaka 1978 alijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria katika Kambi ya Bulombora, Kigoma na Kambi ya Mlale, Songea na kuhitimu mwaka 1979.

Alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1981 na kutunukiwa Shahada ya Uchumi mwaka 1984. Mwaka 1986 alijiunga na masomo ya Shahada ya Uzamili ya Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Alihitimu Shahada ya Uzamili ya Uchumi mwaka 1988.

Mwaka 1990 alijiunga na Chuo Kikuu cha Lund, Sweden kwa masomo ya juu ya Shahada ya Uzamivu ya Uchumi (PhD–Econ) chini ya programu maalumu ya ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuhitimu mwaka 1996.

## Ajira na Uongozi

Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, alipata ajira yake ya kwanza kama Afisa Uhusiano Msaidizi katika Mfuko wa Pensheni wa Taifa (National Provident Fund–NPF) mwaka 1980 na baadaye alijiunga na Shirika la Umma la Elimu (Elimu Supplies) kama Mtafiti Msaidizi wa Masoko hadi mwaka 1981.

Mwaka 1984 aliajiriwa katika Idara ya Kazi akiwa Mchumi. Aliajiriwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Uchumi na Utafiti mwaka 1988 kama Mkufunzi Msaidizi (Tutorial Assistant) na baadaye kupandishwa cheo kuwa Mhadhiri Msaidizi (Assistant Lecturer). Mwaka 1996, aliendelea na kazi ya kufundisha akiwa Mhadhiri hadi mwaka 2002, alipopata likizo ya kitaaluma (Sabbatical Leave) na kufanya kazi Benki ya Dunia katika nafasi ya Mchumi Mwandamizi hadi mwaka 2007.

Mwaka 2007 hadi 2009, Mhe. Dkt. Mpango aliteuliwa kuwa Mshauri wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Masuala ya Uchumi. Mwaka 2010, aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anayesimamia Menejimenti ya Fedha za Umma (Public Finance Management). Mwaka 2010 hadi 2015 aliteuliwa kuwa Katibu Mtendaji, Ofisi ya Rais–Tume ya Mipango ambapo alisimamia maandalizi na utekelezaji wa Mipango yote ya Maendeleo ya Taifa. Baadhi ya Mipango hiyo ni pamoja na: Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12–2025/26); Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2010/11–2015/16); na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17–2020/21) ambayo ililenga kuelekeza upya juhudi za kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Mwezi Desemba 2015, aliteuliwa kuwa Kaimu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na mwishoni mwa mwezi huo huo aliteuliwa kuwa Mbunge na Waziri wa Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 2020. Katika kipindi hicho (mwaka 2015–2020), aliweza kusimamia ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kasi ya wastani wa asilimia 6 hadi 7 na kuiwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za kipato cha kati mwezi Julai 2020.

Mwaka 2020, Mhe. Dkt. Mpango aligombea na kushinda Ubunge wa Jimbo la Buhigwe Mkoani Kigoma na aliteuliwa tena kuwa Waziri wa Fedha na Mipango, nafasi aliyohudumu hadi Machi, 2021.

Kufuatia kifo cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Tarehe 30 Machi, 2021 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuapishwa kushika madaraka hayo tarehe 31 Machi, 2021.



▲

*Picha ya kulia: Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, akiapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anayemuapisha ni Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania. Picha ya kushoto: Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (aliyekaa) akishuhudia uapisho huo, Ikulu Dodoma, tarehe 31 Machi, 2021.*




▶

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), akimwakilisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani uliofanyika Davos nchini Uswisi tarehe 23 Mei, 2022.*

## Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (2021 hadi sasa)

Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2021 hadi sasa)

Matangazo ya Serikali Na. 534 la tarehe 2 Julai, 2021, na Na. 619A la tarehe 30 Agosti, 2023 kama inavyosomeka katika aya ya 1.2 (m) na (n) katika Kitabu hiki.

## Utekelezaji wa Majukumu Kikatiba, Kisera na Kisheria wa OMR kwa kipindi cha (Julai 2021 hadi Sasa)

Kipindi cha Uongozi wa Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, masuala mbalimbali yalijitokeza: kuwepo kwa hoja za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi; kuendelea kuwepo kwa jamii yenye uelewa mdogo kuhusu masuala ya Muungano; kuendelea kuwepo kwa changamoto za uharibifu na uchafuzi wa mazingira; na fursa ya biashara ya kaboni na Uchumi wa Buluu nchini.

Kutokana na masuala yaliyojitokeza, OMR imetekeleza yafuatayo:

- Kusimamia ufumbuzi wa Hoja 15 kati ya 18 za Muungano, ambazo ziliondolewa katika Orodha ya Hoja za Muungano tarehe 26 Agosti, 2021 na 6 Desemba, 2022. Hoja hizo ni: Uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar katika soko la Tanzania Bara; Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA); Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete–Pemba; Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Zanzibar; Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Rufani za Kodi (Tax Revenue Appeals Tribunal - TRAT) kutoka Zanzibar; Uteuzi wa Mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board–DIB) kutoka Zanzibar; Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu; Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano; Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri; Mgawanyo wa Mapato Yatokanayo na Misaada ya Kibajeti (General Budget Support–GBS); Mapato Yanayokusanywa na Uhamiaji kwa Upande wa Zanzibar; Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar Kutozwa Kodi mara mbili; Kodi ya Mapato–(Pay As You Earn–PAYE) na Kodi ya Zuio (Withholding Tax); Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III); na Ongezeko la gharama za umeme kutoka TANESCO kwenda ZECO.




*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akitoa salamu za Tanzania kwa niaba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano maalumu wa miaka 50 ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) uliofanyika jijini Nairobi Kenya, tarehe 3 Machi, 2022.*




*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), akishuhudia utiaji saini wa hati za makubaliano ya kuondoa hoja 11 za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi. Hafla hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Taasisi ya Utalii SUZA, Maruhubi-Zanzibar, 24 Agosti, 2021.*




*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongoza kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kambarage, Treasury Square, Dodoma tarehe 6 Desemba, 2022. Kulia kwake ni Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kushoto kwake ni Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.*

- Kusimamia uandaaji wa kitabu maalumu cha Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ''MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR: Chimbuko, Misingi na Maendeleo''. Kitabu hicho kilizinduliwa tarehe 26 Aprili, 2022 na kupata ithibati mwezi Septemba, 2022 kwa ajili ya kutumika kama kitabu cha ziada kwa shule zote za sekondari za Tanzania Bara na Zanzibar.
- Kusimamia uandaaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 iliyotokana na mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997.




*Kitabu cha "Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo" kilichoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 2022.*



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa tatu kutoka kulia), akizindua Mnara wa Miaka 60 ya JKT, uliopo Makao Makuu ya JKT Dodoma. Kushoto kwake ni Mhe. Innocent Bashungwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Rajabu Mabele, (wa tatu kushoto) Mkuu wa JKT, Mhe. Rosemary Senyamule (wa pili kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, na Mhe. Vita Kawawa (wa kwanza kushoto) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tarehe 01 Julai, 2023.*



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizindua Sera ya Taifa ya Mazingira (2021). Kulia kwake ni Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), jijini Dodoma, tarehe 12 Februari, 2022.*

- Kusimamia uandaaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022–2032), unaolenga kutatua changamoto za mazingira nchini, kwa kuzingatia sehemu na ikolojia husika. Mpango ulizinduliwa tarehe 5 Juni, 2022, na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Kusimamia uandaaji wa Mwongozo wa Udhibiti wa Usimamizi wa Biashara ya Kaboni wa mwaka 2022 na Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2023. Kanuni hizi zilianza kutumika kupitia Tangazo la Serikali Na. 716 la tarehe 6 Oktoba, 2023. Lengo la Kanuni na Mwongozo huo ni kufanikisha nchi kunufaika na fursa zitokanazo na Biashara ya Kaboni, na kutoa motisha kwa jamii ili kuhamasisha hifadhi ya mazingira, hususan katika kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi.




▲

*Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), akimwakilisha Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uzinduzi wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032). Kulia kwake ni Mhe. Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na kushoto kwake ni Zlatan Milisic, Mratibu mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre, Dodoma, tarehe 5 Juni, 2022.*



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongoza zoezi la upandaji miti katika eneo la Ihumwa, Dodoma kusheherekea Maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 2023.*




*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akimkabidhi Mhe. Mwanamvua Mrindoko, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, hundi ya shilingi milioni 230, kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, ikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya biashara ya Kaboni inayofanyika katika vijiji nane vya Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Julai, 2022.*

- Kusimamia maandalizi ya Kampeni Kabambe ya Kitaifa ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira iliyozinduliwa tarehe 5 Juni, 2021, kwa lengo la kuongeza msukumo katika kuhamasisha ushiriki wa jamii na uwajibikaji wa mamlaka za usimamizi katika kuchagiza juhudi za kuimarisha hifadhi ya mazingira na ustawi wa jamii, ili kuchangia maendeleo endelevu.
- Kumwakilisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mikutano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo: Mkutano wa Jukwaa la Uwekezaji Barani Afrika uliofanyika nchini Ivory Coast, tarehe 2–4 Novemba, 2022; Mkutano wa Tano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Idadi ya Watu uliofanyika jijini Budapest nchini Hungary, tarehe 14 Septemba, 2023; Mkutano wa Baraza Kuu la 78 la Umoja wa Mataifa (UNGA) uliofanyika jijini New York tarehe 23 Septemba, 2023; na Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea, uliofanyika Doha Nchini Qatar, tarehe 5 Machi, 2023.




▲

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipomwakilisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wa Tano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Kuhusu Idadi ya Watu uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Museum of Fine Arts Jijini Budapest, nchini Hungary, tarehe 14 Septemba, 2023.*




▲

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa pili kulia) akiwa na Wakuu wa Nchi na Serikali, alipomwakilisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea, uliofanyika Doha nchini Qatar, tarehe 5 Machi, 2023.*



◄

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia kwa niaba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Baraza Kuu la 78 la Umoja wa Mataifa (UNGA) uliofanyika Jijini New York, nchini Marekani, tarehe 23 Septemba, 2023.*



Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (aliyekaa katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi na Watendaji wa OMR. Kulia kwake ni Mhe. Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Kushoto kwake ni Bi. Mary Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais na Bw. Edward Nyamanga, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), kulia kwa Mhe. Dkt. Jafo ni Bw. Abdallah Hassan Mitawi, Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Kikao hicho kilifanyika Mtumba Jijini Dodoma tarehe 23 Machi, 2022.



Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (wa tatu kushoto), Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (wa tatu kushoto) akiweka Jiwe la Msingi la Mradi wa Ujenzi wa Chanzo cha Maji na Kituo cha Tiba ya Maji cha Butimba Nyamagana Jijini Mwanza. Kulia ni Mhe. Jumaa Aweso Waziri wa Maji, Mhe. Adam Malima, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na Mhe. Dkt. Angelina Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tarehe 14 Septemba, 2022.

- Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021/22 –2025/26); na uandaaji wa Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi unaolenga kuiwezesha nchi kuchangia upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto kwa asilimia 30 hadi 35 kupitia sekta za misitu, nishati, usafirishaji na udhibiti wa taka, ifikapo mwaka 2030.
- Kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali inayoendana na mipango ya bajeti, mfano utekelezaji wa shughuli katika sekta za kilimo, elimu na afya.
- Kusimamia uwekezaji na uzalishaji unaozingatia maendeleo endelevu na tathmini ya athari kwa mazingira.
- Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Sura 191.
- Kusimamia uandaaji wa kitabu maalumu cha miaka 60 ya Ofisi ya Makamu wa Rais (1964–2024).




▲

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizundua Mchakato wa Maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 katika Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete Dodoma, tarehe 3 Aprili, 2023.*




◄

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizindua Mpango wa Maendeleo Endelevu wa Ushirikiano (2022-2027) baina ya Tanzania na Umoja wa Mataifa, tarehe 17 Mei 2022. Kulia ni Mhe. Balozi Liberata Mulamula, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Masharik na Mha. Zena Said, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa SMZ, kushoto ni Bw. Zlatan Milisic, Mratibu Mkaazi wa Umoja wa Mataifa Nchini Tanzania na Mhe. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango.*





▲

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwasha Mwenge wa Uhuru wakati wa uzinduzi wa mbio za Mwenge, Uwanja wa Sabasaba, Mkoa wa Njombe, tarehe 2 Aprili, 2022.*




◀

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akifungua Maonesho ya Nanenane, Uwanja wa John Mwakangale Mkoa wa Mbeya, tarehe 1 Agosti, 2022. Kushoto kwake ni Mhe. Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo na kulia kwake ni Mhe. Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo.*



▲

*Mhe. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akisalimiana na Bw. Antonio Guterres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, kabla ya mazungumzo yao yaliyofanyika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa Jijini New York nchini Marekani, tarehe 21 Septemba, 2022.*



◄

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ikulu, Zanzibar alipofanya ziara ya kikazi Zanzibar tarehe 14 Juni, 2021*



▲

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizindua mradi wa maji wa Sibwesa, Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi, tarehe 23 Julai, 2022.*



◄

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Skuli ya Msingi ya Elimu Mjumuisho Jendele iliyopo Wilaya ya Kati, Unguja ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 11 Januari, 2024.*



▲

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizindua Kituo Kikuu cha Zimamoto na Uokoaji katika Wilaya ya Temeke Mkoa Dar es salaam, tarehe 28 Aprili, 2023. Kushoto ni Mhe. Mha. Hamad Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kulia ni Ndg. Kaspar K. Mmuya, Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.*



▲

*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akitoa maelekezo kwa viongozi wa Wizara ya Kilimo kuhusiana na zao la korosho alipotembelea mabanda ya maonesho katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Jijini Dar es salaam, tarehe 11 Oktoba, 2023.*

## Viongozi katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuanzia mwaka 2021 hadi sasa



MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO
Makamu wa Rais
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(2021 hadi sasa)



MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)
(Aprili 2021 hadi sasa)



MHE. HAMAD H. CHANDE
Naibu Waziri
Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)
(Aprili, 2021-Januari, 2022)



MHE. KHAMIS H. KHAMIS
Naibu Waziri
Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)
(Januari, 2022 hadi sasa)

# Viongozi katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuanzia mwaka 2021 hadi sasa (Inaendelea)



BI. MARY N. MAGANGA
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Machi, 2021 hadi sasa)



BW. MOHAMMED K. ABDULLA
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais
(Machi, 2021-Januari, 2022)



BW. EDWARD G. NYAMANGA
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira)
(Januari, 2022-Mei, 2022)



BW. ABDALLAH H. MITAWI
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)
(Januari, 2022 hadi sasa)



DKT. SWITBERT Z. MKAMA
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira)
(Mei, 2022-2023)



BI. CHRISTINA S. MNDEME
Naibu Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira)
(Machi, 2024 hadi sasa)

# VIONGOZI WALIOHUDUMU KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS NA KUPATA NYADHIFA ZA JUU

## Utangulizi

Ofisi ya Makamu wa Rais imebahatika kuwa na viongozi wengi waliohudumu na kupata nyadhifa za juu Kitaifa na Kimataifa. Viongozi hao ni pamoja na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan; Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi; Mhe. Ali Hassan Mwinyi; Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi; Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein; Mhe. Edward Moringe Sokoine; Mhe. Edward Ngoyai Lowassa; Mhe. Pius Chipanda Msekwa; Mhe. Anne Semamba Makinda; Mhe. Balozi Gertrude Ibengwe Mongella na Mhe. Mussa Azzan Zungu.



# Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alihudumu katika wadhifa wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kuanzia mwaka 2010 hadi 2015. Alishika wadhifa wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 5 Novemba, 2015 hadi 18 Machi, 2021. Ni mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kufuatia kifo cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichotokea tarehe 17 Machi 2021, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara 37(5) ambayo inasema "Endapo kiti cha Rais kitakuwa wazi kutokana na Rais kufariki dunia, kujiuzulu, kupoteza sifa za uchaguzi au kutomudu kazi zake kutokana na maradhi ya mwili au kushindwa kutekeleza kazi na shughuli za Rais, basi Makamu wa Rais ataapishwa na atakuwa Rais kwa muda uliobaki katika kipindi cha miaka mitano na kwa masharti yaliyoelekezwa katika Ibara ya 40, kisha baada ya kushauriana na chama cha siasa anachotoka Rais atapendekeza jina la mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura zisizopungua asilimia 50 ya Wabunge wote". Aidha, ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



▶

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anayemuapisha ni Mhe. Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania, Ikulu Dar es Salaam, tarehe 19 Machi, 2021.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kushoto kwake ni Mhe. Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 22 Agosti, 2021.*




◀

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Wakuu wa Nchi na Serikali, uliofanyika katika Mji wa Sharm El Sheikh nchini Misri, tarehe 7 Novemba, 2022.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam, tarehe 13 Januari, 2023.*




◀

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akikata utepe kuzindua kituo cha kupokea, kupooza na kusambaza umeme cha Mpomvu Geita tarehe 15 Oktoba, 2022. Kulia kwake ni Mhe. January Makamba, Waziri wa Nishati, anayefuata ni Mhandisi Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati na kushoto kwake ni Mhe. Martine Shigela, Mkuu wa Mkoa wa Geita.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (kulia), Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, baada ya uzinduzi wa Ofisi za Ikulu ya Chamwino, Mkoani Dodoma, tarehe 20 Mei, 2023.*



*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizungumza na viongozi pamoja na wageni mbalimbali wakati wa uzinduzi wa Filamu ya The Royal Tour katika ukumbi wa Mikutano wa Arusha International Conference Centre AICC, Jijini Arusha, tarehe 28 Aprili, 2022.*



*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akibonyeza Kitufe kuashiria Hatua ya Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme (Megawati 2115) la Julius Nyerere JNHPP kwenye Mto Rufiji Mkoani Pwani, tarehe 22 Desemba, 2022.*




*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wakati wakishiriki moja ya Mikutano, kando ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai-Falme za Kiarabu, tarehe 1 Desemba, 2023.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizungumza na Wafanyabiashara wadogo wa Samaki alipotembelea Soko la Wamachinga Parking, Mkoa wa Tabora, tarehe 18 Oktoba, 2023. Kushoto kwake ni Mhe. Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo.*



◀

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipotembelea Banda la Tanzania wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Dubai, tarehe 2 Desemba, 2023. Kushoto ni Bi. Mary Maganga, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais.*



◀

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akipanda mti Nchini Indonesia akiwa na Mhe. Joko Widodo, Rais wa Indonesia kwenye makazi ya Rais huyo, tarehe 25 Januari, 2024.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Jengo la Ikulu ya Chamwino, Jijini Dodoma, tarehe 20 Mei, 2023. Kushoto kwake ni Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akifuatiwa na Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kulia kwake ni Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akifuatiwa na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*



◀

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizungumza na viongozi mbalimbali mara baada ya kufungua Mkutano wa pembezoni wa "Agricultural Opportunities for Green Growth Transformation in Tanzania", Dubai, tarehe 3 Desemba, 2023.*



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na mgeni wake Mhe. Abiy Ahmed Ali, Waziri Mkuu wa Ethiopia alipofanya ziara nchini Tanzania, tarehe 1 Machi, 2024.*



# Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi

Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi alishika wadhifa wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kuanzia mwaka 2006 hadi 2008.

Mwaka 2008 Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi aliteuliwa kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wadhifa alioshika hadi mwaka 2012. Mwaka huo huo, Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliteuliwa kuwa Waziri wa Afya, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 2014 ambapo aliteuliwa tena kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwaka 2015, Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliteuliwa tena kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, akihudumu nafasi hiyo hadi mwaka 2020.

Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi anakuwa Waziri wa pili kushika wadhifa wa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kipindi kirefu cha miaka 10 kwa vipindi tofauti, ikilinganishwa na Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa aliyehudumu katika masuala ya ulinzi kwa miaka 15 kwa vipindi tofauti.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi aliteuliwa na CCM kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar ambapo chama hicho kilimpitisha. Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi alichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 30 Oktoba, 2020.



▶

*Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anayemuapisha ni Mhe. Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar. Anayeshuhudia ni Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar aliyemaliza muda wake (aliyekaa), aliyesimama katikati ni Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa SMZ, Uwanja wa Amaan Zanzibar, tarehe 2 Novemba, 2020.*



▲

*Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akiongoza kikao cha Baraza la Mapinduzi, kilichofanyika katika Ukumbi wa Ikulu, Zanzibar, tarehe 23 Desemba, 2020.*



*Picha ya kushoto: Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akihutubia Baraza la Kumi la Wawakilishi Zanzibar (picha ya kulia) wakati wa hafla ya ufunguzi wa Baraza hilo katika Ukumbi wa Baraza Chukwani Zanzibar, tarehe 11 Novemba, 2020.*






*Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akikaribishwa na Mhe. Nyeleti Brooke Mondlane, Waziri wa Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto wa Msumbiji katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Maputo nchini Msumbiji, akimwakilisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali, tarehe 27 Mei, 2021.*



*Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akiwahutubia wananchi wa Zanzibar, baada ya kufungua rasmi Uwanja wa michezo wa Amaan Zanzibar uliofanyiwa ukarabati mkubwa, tarehe 27 Desemba, 2023.*



*Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (kushoto aliyeshika kitambaa), akizindua Maonesho ya Kwanza ya Utalii kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jijini Arusha, ambapo alimwakilisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kulia aliyeshika kitambaa ni Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Maliasili na Utalii (SJMT), tarehe 12 Oktoba, 2021.*



*Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akiwapungia mkono wananchi waliohudhuria Sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika katika uwanja wa Amaan, tarehe 12 Januari, 2024.*



# Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi

Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, alishika wadhifa wa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1983 hadi 1984. Alishika wadhifa wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia Januari, 1984 hadi Oktoba, 1985. Aidha, mwezi Oktoba, 1985 alichaguliwa kushika wadhifa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano na mwezi Oktoba, 1990 alichaguliwa tena kushika wadhifa huo aliohudumu hadi mwezi Novemba, 1995. Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi ni Rais wa kwanza kushika nafasi hiyo kutokea Zanzibar na pia ni kiongozi wa kwanza kuhudumu nafasi za Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar.



*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais Mteule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), akiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais anayemaliza muda wake (kushoto) na Sheikh Idris Abdulwakil, Rais Mteule wa Zanzibar (kulia), Ikulu Dar es Salaam, Oktoba, 1985.*



*Mhe. Ali Hassan Mwinyi (kulia), akiapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayemuapisha ni Mhe. Francis Nyalali, Jaji Mkuu wa Tanzania (mwenye joho), wengine ni Mh. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyemaliza muda wake, akishuhudia uapisho, Uwanja wa Taifa-Dar es Salaam, tarehe 5 Novemba, 1985.*



*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa nne kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Kamati ya "Saidia Taifa Stars Ishinde" iliyowezesha Taifa Stars kushinda ubingwa wa Kombe la Chalenji la Afrika Mashariki, Ikulu Jijini Dar es Salaam, mwaka 1994. Waliosimama mbele toka kulia ni: Muhidin Issa Michuzi (Mwanahabari), Brigedia Moses Nnauye, Al-hajj Muhidin Ndolanga (Mwenyekiti wa Chama cha Soka-FAT), Profesa Philemon Sarungi (Waziri wa Afya), Bw. Reginald Mengi (Mwenyekiti wa Kamati), Mhe. Kuwayawaya S. Kuwayawaya (Mbunge wa Dodoma) na Richard Mwaikenda (Mwanahabari).*



*Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akimuaga Mwalimu Julius Nyerere, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam, Novemba 1985.*



# Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi

Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi, alihudumu katika wadhifa wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia tarehe 11 Aprili, 1972 hadi tarehe 29 Januari, 1984. Alikuwa kiongozi pekee aliyehudumu katika nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Rais wa Zanzibar kwa muda wa miaka 12 mfululizo.





*Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akiwa na Malkia Elizabeth II wa Uingereza alipotembelea Zanzibar, mwaka 1979.*



*Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi (kulia), akiapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar. Anayemuapisha ni Mhe. Augustino Ramadhani, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Ikulu Zanzibar, tarehe 30 Oktoba, 1980.*



# Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine

Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine, aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1972 hadi 1975. Mwaka 1977 hadi 1980 alishika wadhifa wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, tarehe 23 Februari, 1983 aliteuliwa tena kushika wadhifa wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi tarehe 12 Aprili 1984, alipofariki dunia kwa ajali ya gari Mkoani Morogoro.





▶

*Mhe. Edward Moringe Sokoine, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), alipotembelea uwanja wa vita Mutukula, Mkoani Kagera, kukagua hali ya usalama wakati wa vita vya Kagera, tarehe 23 Januari, 1979. Kushoto ni Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kulia ni Brigedia Mosses Nnauye.*



◀

*Mhe. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), akimuapisha Mhe. Edward Moringe Sokoine kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ikulu Dar es Salaam, mwaka 1977. Katikati ni Bw. Dickson A. Nkembo, Katibu Mkuu Kiongozi Ofisi ya Rais.*



# Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba

Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, baada ya kuitumikia nchi kwa nafasi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 5 Novemba, 1985 hadi tarehe 9 Novemba, 1990, aliteuliwa kushika wadhifa wa Jaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria ya Bahari, Jijini Hamburg, Ujerumani, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 1999. Mahakama hiyo ni matokeo ya kazi iliyotukuka iliyofanywa na Tume ya Umoja wa Mataifa ya Kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu (1983–1986) chini ya uenyekiti wa Jaji Warioba. Mwaka 2001, Jaji Warioba aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ), nafasi aliyohudumu hadi mwaka 2006. Mwaka 2002, aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Watu Mashuhuri Duniani *(Eminent Persons Group)* lililoanzishwa na Taasisi ya Global Coalition for Africa, Washington DC, Marekani, ili kuleta utangamano wa kikanda mashariki na kusini mwa Afrika wadhifa aliohudumu Uenyekiti wake ulidumu hadi mwaka 2004. Hata hivyo, wajumbe wa Jopo hilo hawakuwa wa kudumu bali waliteuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kushiriki kwenye shughuli mahsusi za Jopo. Aidha, alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2012–2014).



▲

*Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba (wa tatu kushoto), akiwa na majaji wenzake 20 wa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria ya Bahari, Jijini Hamburg, Ujerumani, mwaka 1996.*



# Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa

Mwaka 1990, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (Sera, Masuala ya Bunge na Uratibu wa Maafa) nafasi aliyohudumu hadi 1993. Mwaka 1997 Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi mwaka 2000. Aidha, mwezi Desemba, 2005 aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafasi aliyohudumu hadi Februari, 2008 alipojiuzulu.



▲

*Mhe. Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na Mhe. Nguyen Tan Dung, Waziri Mkuu wa Vietnam, wakikagua gwaride la heshima alipoanza ziara rasmi ya siku tano nchini Vietnam iliyolenga kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara, Jijini Hanoi, tarehe 5 Septemba, 2006.*



◀

*Mhe. Edward Ngoyai Lowassa akiapa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Dar es Salaam, tarehe 30 Desemba, 2005.*





▲

*Mhe. Edward Lowasa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 2007.*

*Mhe. Edward Lowasa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi wa Zanzibar wakielekea katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam kwa ajili ya kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Changamoto za Muungano, tarehe 22 Mei, 2006.*

▼





# Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein

Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein alihudumu nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2001 hadi 2010 na baadaye kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nafasi ambayo alihudumu kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2010 hadi 2020.

*Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, akiapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anayemuapisha ni Mhe. Hamid Mahamoud, Jaji Mkuu wa Zanzibar (mwenye joho), anayeshuhudia ni Mhe. Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar aliyemaliza muda wake, Uwanja wa Amaan Jijini Zanzibar, tarehe 3 Novemba, 2010.*





▲

*Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, akiwa katika Maonesho ya Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika katika Viwanja vya Chamanangwe, Pemba, tarehe 10 Oktoba, 2019.*



# Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa



▲

*Mhe. Pius Msekwa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto) akiwa na Mhe. Benjamin William Mkapa, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu wakiwa nje ya Ukumbi wa Karimjee, Jijini Dar es Salaam, mwaka 1995.*

Mwaka 1985 hadi 1989, Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwaka 1990, alistaafu utumishi wa umma Serikalini na aligombea na kushinda katika uchaguzi wa Ubunge katika Jimbo la Ukerewe. Mwaka huo huo alichaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhudumu katika nafasi hiyo hadi mwaka 1994. Aidha, mwezi Oktoba, 1994 alikuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi mwaka 2005.



▲

*Mhe. Pius Msekwa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto) akizungumza na Mhe. Dkt. Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma, Rais Mstaafu wa Zanzibar wakati wa sherehe za miaka 38 ya Muungano, mwaka 2002.*



# Mheshimiwa Anne Semamba Makinda

Mheshimiwa Anne Semamba Makinda alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Uratibu wa Shughuli za Serikali na Muungano), kuanzia mwaka 1983 hadi 1990. Aidha, alikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto kuanzia mwaka 1990 hadi 1995. Vilevile, alikuwa Mbunge wa Jimbo la Njombe Kusini na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2006 hadi 2010. Alikuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwezi Novemba, 2010 hadi Novemba, 2015.



▲

*Mhe. Anne Semamba Makinda, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongoza kikao cha Bunge la 10 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 28 Februari, 2012.*




◀

*Mhe. Anne Makinda, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (mbele kushoto), akishiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika Jijini Quebec, Canada, tarehe 21 hadi 26 Oktoba, 2012.*



*Mhe. Anne Makinda, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kushoto), akipokea tuzo ya African Influential Amazon Award kutoka kwa Dkt. Ida Odinga, Mke wa Waziri Mkuu wa Kenya, iliyotolewa na Taasisi ya Centre for Economic and Leadership Development, kutambua mchango wake katika kupigania masuala ya wanawake Barani Afrika, Jijini Nairobi Kenya, tarehe 25 Novemba, 2012.*

▼





# Mheshimiwa Gertrude Ibengwe Mongella

Mwaka 1982 hadi 1985, Mheshimiwa Gertrude Ibengwe Mongella alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Wanawake). Mwaka 1985 hadi 1987, alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Wanawake). Aidha, alishika nafasi nyingine za kitaifa na kimataifa zikiwemo: Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Katibu Mkuu wa Mkutano wa Nne wa Umoja wa Mataifa wa Masuala ya Wanawake, Beijing, China, mwaka 1993 hadi 1995; na Spika wa Bunge la Afrika, nafasi aliyohudumu kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia 2004 hadi 2009.




▲

*Mhe. Getrude Ibengwe Mongella, Katibu Mkuu wa Kongamano la Nne la Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake (wa kwanza kushoto) lililofanyika Beijing nchini China, mwaka 1995.*

*Mhe. Gertrude Ibengwe Mongella, Rais wa Bunge la Afrika (wa pili kulia mstari wa mbele) akiwa na Mhe. Muammar Gaddafi, Rais wa Libya (kushoto), na Mhe. Georgi Parvanov, Rais wa Bulgaria, katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali baina ya Umoja wa Ulaya na Bara la Afrika, uliofanyika Jijini Lisbon, Ureno, tarehe 8 Desemba, 2007.*

▼







# Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu alihudumu katika nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Muungano na Mazingira) kuanzia mwezi Januari hadi Oktoba, 2020 ambapo mwaka 2022 alishika wadhifa wa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi sasa.





▲

*Mhe. Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongoza Kikao cha Bunge kilichofanyika Jijini Dodoma, tarehe 8 Februari, 2022.*



◀

*Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia), akimuapisha Mhe. Mussa Azzan Zungu kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma, tarehe 11 Februari, 2022.*

# MUZIKI WA DANSI NA TAARAB ULIVYOIMARISHA MUUNGANO



Pamoja na kwamba makundi mbalimbali ya wananchi wa Tanzania yaliunga mkono Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa nderemo na vifijo, mwaka 1964 na kuendelea, tasnia ya muziki wa dansi, taarab na ngoma za asili imekuwa na mchango wa kipekee katika kuunga mkono, kuutangaza, kuulinda na kuuimarisha Muungano. Imefanya hivyo kwa tungo zake za mvuto zilizo midomoni mwa Watanzania na watumia Kiswahili wengi duniani.

Tungo hizo ziliwapongeza na kuwatia moyo waasisi wa Muungano, ziliwahamasisha Watanzania kuimarisha Muungano na kuwasuta wapinga Muungano. Ni dhahiri kuwa mbali na vitabu na majarida mbalimbali yaliyoandika kuhusu Muungano, bendi za muziki wa dansi, taarab na ngoma za asili katika mikoa mbalimbali zilichangia kwa kiasi kikubwa kuhifadhi historia na maendeleo ya Muungano kwa njia ya sauti. Mashairi yao yaliyotungwa kwa ustadi na kusindikizwa na ala mbalimbali za muziki zilizopigwa kwa ufundi mkubwa, yataendelea kuwa sehemu ya historia ya Muungano kwa karne nyingi zijazo.



Baadhi ya tungo kuhusu Muungano zilizohifadhiwa kwa sauti na maandishi na zisizochuja masikioni ni: 1. Nyerere na Karume (Western Jazz Band); 2. Sasa Tumeungana (Salum Abdallah, Cuban Marimba Jazz Band); 3. Muungano Wetu (Kilwa Jazz); 4. Twafurahia Muungano (Salum Abdallah, Cuban Marimba Jazz Band); 5. Muungano Miaka Mitatu (NUTA Jazz); 6. Muungano Umekamilika (Vijana Jazz); 7. Muungano Umekamilika (JKT Kimbunga); 8. Muungano Umefana (HK Makassy, Orchestre Makassy); 9. Muungano (Varda Arts); 10. Sheikh Karume (Mbaraka Mwinshehe, Morogoro Jazz); 11. Udumu Muungano Wetu Daima Milele (Culture Musical Club); na 12. Udumu Muungano Wetu Sehemu ya I na II (Abdullah Fereshi, Dar Modern Taarab).





▲

*Bw. Salum Abdallah Yazidu (picha ndogo kushoto) almaarufu SAY, Kiongozi na Mmiliki wa Bendi ya Cuban Marimba, mwaka 1965. Wengine ni wanamuziki wa bendi hiyo.*




▲

*Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (katikati), akizungumza na Mwanamuziki Mkongwe, Hyppolite Makassy (Mzee Makassy) kulia kwa Waziri Mkuu, nje ya viwanja vya Bunge Jijini Dodoma. Kushoto kwa Waziri Mkuu ni Mhe. Martha Mlata, Mbunge Viti Maalumu, tarehe 28 Juni, 2018.*

Tungo nyingi za mwanzo zilikuwa fupi zenye kiitikio kimoja kilichobeba maudhui ya Muungano na kilichorudiwa mara kwa mara. Mfano, wimbo maarufu ''Nyerere na Karume'' wa Western Jazz, una kiitikio kikuu kinachorudiwa mara kwa mara kisemacho: ''Nyerere na Karume wastahili kusifiwa na wananchi wote wa Tanzania aah, kwa kutuletea Muungano wa Tanzania''.

Wimbo mwingine maarufu ni ''Muungano wetu'' wa Kilwa Jazz, ulioanza kuimbwa miaka ya mwanzoni ya Muungano, unaanza na maneno yanayorudiwarudiwa ''Nyerere ameleta Muungano wa Tanzania, noooh; Karume ameleta Muungano wa Tanzania, oooh'', na kiitikio chake kinachorudiwa mara kadhaa ni ''Ooh Nyerere wee, Ooh Karume wee''. Kwa mujibu wa wataalamu wa mawasiliano ya umma na

wasanii wa muziki wa dansi, sifa kuu ya tungo fupi zenye maudhui yanayojirudia mara kwa mara ni kuhamasisha jambo jipya ili lisambae na kujikita katika jamii kwa urahisi na haraka. Tungo fupi hukaririwa na wasikilizaji bila kuumiza kichwa na hujikuta wakishiriki katika kuimba kila zikipigwa redioni, kipindi hicho redio pekee zilikuwa ni Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) na Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ). Aidha, mtu akiwa peke yake akiendelea na shughuli zake binafsi, hakosi kuziimba kwa sauti au kwa mluzi.

Tungo za baadaye ziliongezeka kwa maneno, yumkini kutokana na kuongezeka kwa kizazi kipya kilichohitaji maelezo zaidi kuhusu Muungano. Pamoja na ongezeko la maneno, mvuto wa nyimbo pia uliongezeka kutokana na ubora wa ala na weledi katika muziki. Mfano ni wimbo maarufu wa ''Muungano Umefana'' uliopigwa na Orchestre Makassy ambao ni shairi refu lililosindikizwa kwa ala za muziki za kisasa zilizopigwa kwa ustadi mkubwa na kuufanya wimbo huo kuwa kileleni kwa ubora kwa miongo mingi. Wimbo huo ulianza kupigwa mwaka 1978 mwaka mmoja baada ya kuungana kwa vyama vya ASP na TANU mwaka 1977. Shairi lake linasomeka:

*Mwaka sitini na nne, Tanganyika na Unguja,*
*Nyerere naye Karume, hawakutaka kungoja,*
*walifanya nchi iwe nene, Tanzania naitaja,*
*kuwepo kwa CCM, Muungano umefana.*

*Ni Muungano wa kweli, wa kuigwa Afrika,*
*Hauhitaji kibali, kwamba utaghalifika,*
*Mwanzoni ni Serikali, sasa ni chama kimoja,*
*CCM ni Serikali, lengo lake ni Umoja.*
*Nyerere naye Barani, hata kule visiwani,*
*Wamwamini makini, kiongozi wa kanuni,*
*CCM amebuni, Muungano kaidhini,*
*kuwepo kwa CCM, Muungano umefana.*

*Sasa ni Muungano kweli, Bara, Pwani na Unguja,*
*Baraza la Mapinduzi, hata kule visiwani,*
*limekataa upuuzi, Chama ndio darubini,*
*Jumbe mwanamapinduzi, yupo kwenye usukani.*

Taarab haikubaki nyuma katika kuusemea Muungano. Kikundi cha Dar Modern Taarab kilivunja ukimya katika kuadhimisha miaka 50 ya Muungano kwa shairi refu ''Muungano Wetu'' lililogawanyika sehemu mbili (Sehemu ya Kwanza na ya Pili ) na kusindikizwa na mdundo ambao daima unaowanyanyua watu vitini. Shairi linasema (Sehemu ya Kwanza):

*Sisi Watanzania twajisikia fahari,*
*Muungano wetu leo ni miaka hamsini.*
*Tunastahili kuwa na kimbelembele,*
*Hatungojei sisi tusifiwe, tumeamua tujisifu wenyewe.*

*Utuonavyo tuache kama tulivyo,*
*miaka na miaka tunaipwaga.*
*Haya haya na ituone dunia; haya, Muungano unang'ara.*

*Walimwengu msigeuze uso, wala nyie msitupe kisogo,*
*Bahati si kupata mpepeto, jinsi tunavyoupiga bao.*
*Twaiweza vita ya faulo, kwa uadui wa Muungano,*
*Vidole juu wote tunavyo, na umedumu wetu Muungano.*

*Kujizatiti si tumeweza, wala hakuna wa kutuzuia,*
*Kuimarisha wetu umoja, hapa nchini Tanzania.*
*Wote sie kwa pamoja, visiwani na bara,*
*Tumeamua kushikana, ndiyo maana umetimia.*

*Ni miaka hamsini sasa, Muungano imara Tanzania,*
*Waliodhani hatutaweza, nyongo zimewatumbukia.*
*Tutambe kwa raha zetu, hawatuwezi asilani,*
*Sisi kawaida yetu, kushikana kwa amani.*

*Watabaki na hangaiko, wataambulia ukoko,*
*Watavishika viuno, wabaki wazi midomo.*
*Kuuvunja Muungano, katu hatuwezi ng'o,*
*Kuuvunja Muungano, katu hatudiriki ng'o.*
*Inabidi wao kutulizana, shauku zao kuziwacha,*
*Wajue magwiji Tanzania, twavinjari Watanzania.*
*Twatesa kiroho mbaya, Afrika nzima tunameta,*
*Vishindo vyao wakome wao, kufisidi wetu Muungano.*
*Hawatutishi kwa mafumbo, mafumbo hapa ndio kwao,*
*Twatoka kwenye chimbuko, la mafumbo na matao.*
*Dunia ni mfano, Watanzania ni kiboko,*
*Twayaweza si kidogo, mahasidi watabloo.*

Sehemu ya pili ya wimbo huo ni ndefu kama ya kwanza ikiwa na ujumbe wa ziada kuhusu Muungano. Hata hivyo wapenzi wa mahadhi ya taarab, hasa wanawake, wanayaimba mashairi yote mawili kwa mtiririko na bashasha na kusambaza ujumbe kuhusu Muungano kila ambapo Dar Modern Taarab wanatumbuiza kwenye ukumbi wao wa miaka mingi, Magomeni Dar es Salaam.

Pengine mchango mkubwa katika kuutangaza na kuulinda Muungano unatoka kwenye ngoma zetu za utamaduni ambazo zipo katika kila mkoa. Juhudi za kuzinakili tungo mbalimbali za ngoma zetu kwa sauti na maandishi, na kuzitafsiri kwa Kiswahili zinafanyika na taasisi mbalimbali kwa ajili ya kumbukumbu za vizazi vijavyo. Kwa ujumla, muziki wa dansi, taarab na ngoma za utamaduni, siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni bali vilevile, sehemu muhimu ya maisha ya kila siku ya Watanzania na Waafrika kwa ujumla.

Mbali na kutoa burudani, muziki umekuwa ukitoa elimu na ujumbe wenye, furaha, majonzi, urafiki, undugu, ushindani, upatanishi n.k. katika historia ndefu ya Waafrika kabla ya kuingiliwa na mataifa ya nje. Ni katika muktadha huu, andiko hili linatambua mchango mkubwa wa tasnia ya muziki wa dansi, taarab na ngoma za asili kwa pamoja katika kuunga mkono, kuutangaza, kuulinda na kuuimarisha Muungano. Jitihada hizi ni zoezi endelevu katika kudumisha Muungano. Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alitamka mara kadhaa baada ya uhuru kuwa Taifa lisilo na utamaduni wake ni Taifa mfu!

Wananchi katika miji ya pwani ya Bagamoyo, Pangani, Tanga, Dar es Salaam na Unguja walikuwa na uhusiano wa muda mrefu wakitembeleana wakati wa Sikukuu mbalimbali, Klabu za Michezo zilikuwa na utaratibu wa kila mwaka kutembeleana kwa zamu.

Utaratibu huo, umeendelea hata baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambapo vikundi mbalimbali vya michezo katika pande zote mbili za Muungano vimeendeleza mahusiano hayo kupitia matamasha ya sikukuu.

Mbali na muziki wa dansi, taarab na ngoma za asili, wanamichezo mbalimbali nao wametoa mchango mkubwa katika kuimarisha na kudumisha Muungano ikiwemo ligi za mpira wa miguu na pete (Kombe la Muungano, Kombe la Mpira wa Pete na Riadha).



▲

*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakipiga ngoma kabla ya kuingia Rasmi katika Ofisi za Ikulu ya Chamwino, Mkoani Dodoma, tarehe 20 Mei, 2023.*

# HITIMISHO NA MATARAJIO

Ofisi ya Makamu wa Rais inapotimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake, imeshuhudia mafanikio makubwa katika awamu zote za uongozi. Mafanikio hayo yamejidhihirisha katika kuboresha hali ya nchi kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, Muungano umeendelea kudumishwa na hifadhi ya mazingira nchini imeimarika.

Kwa upande wa Muungano, Serikali zote mbili zimefanikiwa kusimamia utekelezaji wa masuala ya Muungano kwa ufanisi mkubwa na hivyo kuimarika kwa utaifa, umoja, amani, utulivu na hali ya maisha ya wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi wa pande zote mbili za Muungano.

Mahusiano ya kijamii baina ya watu wa pande mbili za Muungano yameendelea kuimarika. Aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeanzisha mfumo rasmi wa utatuzi wa changamoto za Muungano.

Vilevile, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeweka Mwongozo wa Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano kati ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za SJMT na SMZ ili kuendelea kuimarisha ushirikiano na mahusiano kwa pande mbili za Muungano. Hali kadhalika Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kuandaa kitabu cha ''Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo'' ambacho kimepata ithibati ya kutumika kama kitabu cha ziada katika shule zote za sekondari Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa upande wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira mafanikio yafuatayo yamepatikana; kuandaliwa kwa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo, Mikakati, Programu na mfumo wa kitaasisi, kwa lengo la kuimarisha hifadhi ya mazingira nchini ambayo ni pamoja na: Kuandaa Sera ya Mazingira ya mwaka 2021; kufanya mapitio ya Sheria ya Mazingira Sura 191; kuandaa kanuni na mwongozo wa udhibiti na usimamizi wa biashara ya kaboni; kuandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022–2032); kupiga marufuku uzalishaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki, na kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, changamoto kadhaa zimekuwa zikijitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi zikiwemo: uelewa mdogo kuhusu Muungano kwa baadhi ya Watanzania; na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu hifadhi ya mazingira na utegemezi wa maliasili katika kujikimu kimaisha.

Ofisi ya Makamu wa Rais inatarajia: kuendelea kutoa elimu ya Muungano kwa umma ili kuendelea kujenga ari ya kudumisha, kuulinda, kuutetea, kuuenzi na kuuimarisha na hivyo kuendeleza amani na utulivu wa Taifa; kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu za Mazingira kwa lengo la kutunza na kuhifadhi Mazingira; kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano ili kuharakisha utekelezaji wa maamuzi; na kuimarisha ushirikiano wa wizara/idara na taasisi zisizo za Muungano za SJMT na SMZ katika mambo yasiyo ya Muungano.

# REJEA


1. Ali Shaaban Juma (2013). *Abeid Amani Karume 1905–1972. Rafiki Publishers, Zanzibar.*
2. Ali Hassan Mwinyi, Mzee Rukhsa (2020). Safari ya Maisha Yangu. *Mkuki na Nyota Publishers Ltd, Dar es Salaam.*
3. Ali A. Mohamed (1979), Kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi. *Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.*
4. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2021). Majadiliano ya Bunge, Mkutano wa Tatu, Kikao cha Kwanza, Tarehe 30 Machi, 2021.
5. Halmashauri ya Uandishi wa Vitabu Zanzibar (1969). *Risala Muhimu kwa Mzee Abeid Aman Karume–Zanzibar*. Shirika la Upigaji Chapa Zanzibar.
6. John M. J. Magotti (2007). *Simba wa Vita katika Historia ya Tanzania: Rashidi Mfaume Kawawa. Central Printing Works, Ltd.*
7. Julius K. Nyerere (*Uhuru na Maendeleo). Printpak Tanzania Ltd., Dar es Salaam.*
8. Katiba ya Muda ya Tanzania ya Mwaka 1965
9. Ofisi ya Makamu wa Rais (2022). *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo. Mkuki na Nyota Publishers Ltd., Dar es Salaam.*
10. Ofisi ya Makamu wa Rais (2014). *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Historia katika Picha (1964–2014).*
11. Ofisi ya Rais (2014). *Taarifa ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (1964–2014).* Dar es Salaam.
12. Ofisi ya Makamu wa Rais (2011). *Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, 1961–2011*.
13. Ofisi ya Makamu wa Rais (2011). *Mafanikio ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara Katika Kudumisha Muungano na Hifadhi ya Mazingira Nchini (1961–2011).*
14. Ofisi ya Makamu wa Rais (2021). *Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021*.
15. Ofisi ya Waziri Mkuu (2011). Taarifa ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara (1961–2011).
16. Ofisi ya Makamu wa Rais. Hotuba za Bajeti Kuanzia Mwaka 1997–2022.
17. Ofisi ya Makamu wa Rais (2018). *Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Nchi.*
18. Pius Msekwa (2019), Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, *Tanzania Education Publishers Ltd.* Bukoba, Tanzania.
19. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (2014). *Miaka 50 ya Mapinduzi.*
20. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2005). *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977*. Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam.
21. Sheria Namba 22 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964–Tanganyika
22. Sheria ya Muungano wa Zanzibar na Tanganyika ya mwaka 1964–Zanzibar
23. Tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (www.vpo.go.tz)
24. Tovuti ya Ikulu (www.ikulu.go.tz)

## Hati ya Makubaliano ya Muungano Kati ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar



ARTICLES OF UNION

b e t w e e n

THE REPUBLIC OF TANGANYIKA AND THE PEOPLES' REPUBLIC OF ZANZIBAR

ARTICLES OF UNION

between

THE REPUBLIC OF TANGANYIKA AND THE PEOPLES' REPUBLIC OF ZANZIBAR

WHEREAS the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar, being mindful of the long association of the peoples of these lands and of their ties of kinship and amity, and being desirous of furthering that association and strengthening these ties and of furthering the unity of African peoples, have met and considered the union of the Republic of Tanganyika with the Peoples' Republic of Zanzibar:

AND WHEREAS the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar are desirous that the two Republics shall be united in one Sovereign Republic in accordance with the Articles hereinafter contained:-

It is therefore AGREED between the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar as follows:-

(i) The Republic of Tanganyika and the Peoples' Republic of Zanzibar shall be united in one Sovereign Republic.

(ii) During the period from the commencement of the union until the Constituent Assembly provided for in Article (vii) shall have met and adopted a Constitution for the united Republic [hereinafter referred to as the interim period] the united Republic shall be governed in accordance with the provisions of Articles (iii) to (vi).

(iii) During the interim period the Constitution of the united Republic shall be the Constitution of Tanganyika so modified as to provide for -

(a) a separate legislature and executive in and for Zanzibar as from time to time constituted in accordance with the existing law of Zanzibar and having exclusive authority within Zanzibar for matters other than those reserved to the Parliament and Executive of the united Republic;

(b) the offices of two Vice-Presidents one of whom (being a person normally resident in Zanzibar) shall be the head of the aforesaid executive in and for Zanzibar and shall be the principal assistant of the President of the United Republic in the discharge of his executive functions in relation to Zanzibar;

(c) the representation of Zanzibar in the Parliament of the united Republic;

(d) such other matters as may be expedient or desirable to give effect to the united Republic and to these Articles.

/ (iv)

- 2 -

(iv) There shall be reserved to the Parliament and Executive of the united Republic the following matters -

(a) The Constitution and Government of the united Republic
(b) External Affairs
(c) Defence
(d) Police
(e) Emergency Powers
(f) Citizenship
(g) Immigration
(h) External Trade and Borrowing
(i) The Public Service of the united Republic
(j) Income Tax, Corporation Tax, Customs and Excise
(k) Harbours, Civil Aviation, Posts and Telegraphs.

And the said Parliament and Executive shall have exclusive authority in such matters throughout and for the purposes of the united Republic and in addition exclusive authority in respect of all other matters in and for Tanganyika.

(v) The existing laws of Tanganyika and of Zanzibar shall remain in force in their respective territories subject -

(a) to any provision made hereafter by a competent legislature;

(b) to such provision as may be made by order of the President of the united Republic for the extension to Zanzibar of any law relating to any of the matters set out in Article (iv), and the revocation of any corresponding law of Zanzibar;

(c) to such amendments as may be expedient or desirable to give effect to the union and to these Articles.

(vi) (a) The first President of the united Republic shall be MWALIMU JULIUS K. NYERERE and he shall carry on the Government of the united Republic in accordance with the provisions of these Articles and with the assistance of the Vice-Presidents aforesaid and of such other ministers and officers as he may appoint from Tanganyika and Zanzibar and their respective public services.

(b) The first Vice-President from Zanzibar to be appointed in accordance with the modifications provided for in Article (iii) shall be SHEIKH ABEID KARUME.

(vii) The President of the united Republic in agreement with the Vice-President who is head of the Executive in Zanzibar shall -

(a) Appoint a Commission to make proposals for a Constitution for the united Republic.

- 3 -

(b) Summon a Constituent Assembly composed of Representatives from Tanganyika and from Zanzibar in such numbers as they may determine to meet within one year of the commencement of the union for the purpose of considering the proposals of the Commission aforesaid and to adopt a Constitution for the united Republic.

(viii) These Articles shall be subject to the enactment of laws by the Parliament of Tanganyika and by the Revolutionary Council of the Peoples' Republic of Zanzibar in conjunction with the Cabinet of Ministers thereof, ratifying the same and providing for the Government of the united Republic and of Zanzibar in accordance therewith.

IN WITNESS WHEREOF Julius K. Nyerere, the President of the Republic of Tanganyika, and Abeid Karume, the President of the Peoples' Republic of Zanzibar, have signed these Articles, in duplicate, at Zanzibar, on this 22nd. day of APRIL, , 1964.

Julius K. Nyerere

for the Republic of Tanganyika

Abeid Amani Karume

for the Peoples' Republic of Zanzibar

# KAMATI ILIYOANDAA KITABU CHA MIAKA 60 YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | **Bw. Rawson P. Yonazi** | Msaidizi wa Katibu wa Baraza la Mawaziri (Mstaafu) | Mwenyekiti |
| 2 | **Dkt. Harisson G. Mwakyembe** | Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sayansi na Afya Muhimbili (MUHAS) | Mwezeshaji |
| 3 | **Bi. Mary N. Maganga** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 4 | **Bw. Abdallah H. Mitawi** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 5 | **Dkt. Switbert Z. Mkama** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 6 | **Bw. Sigsbert R. Kavishe** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 7 | **Bi. Sarah M. Kibonde** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 8 | **Bi. Hanifa M. Selengu** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 9 | **Bi. Judith Y. Mhina** | Idara ya Habari Maelezo (SJMT) | Mjumbe |
| 10 | **Dkt. Juma M. Salum** | Idara ya Habari Maelezo (SMZ) | Mjumbe |
| 11 | **Bw. Ramadhan M. Ramadhan** | Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) | Mjumbe |
| 12 | **Bi. Cesilia D. Nkwamu** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 13 | **Bi. Martha R. Ngalowera** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 14 | **Bw. Jacob N. Bulemo** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 15 | **Bw. Julius E. Moshi** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 16 | **Bi. Joyce P. Mnunguli** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 17 | **Bi. Evansia A. Shirima** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 18 | **Bw. Kyamani K. Mugisha** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 19 | **Bw. Juvenary M. Byekwasho** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 20 | **Bw. Robert T. Hokororo** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 21 | **Bi. Zanipha T. Msangi** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 22 | **Bw. Said A. Said** | Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) | Mjumbe |
| 23 | **Bi. Gloria G. Shirima** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 24 | **Bw. Raphael Maziku** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 25 | **Bw. Abdulla Othman** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 26 | **Bw. Paulo S. Laiser** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 27 | **Bw. Daniel M. Sagata** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 28 | **Bi. Edna J. Nkulila** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Sekretarieti |
| 29 | **Bi. Fatuma A. Mwendo** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Sekretarieti |
| 30 | **Bi. Sheillah A.Mabakila** | Ofisi ya Makamu wa Rais | Sekretarieti |